ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe

18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 19 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2014/2015.

Naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2014/2015.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 70

Kupatiwa Msaada Wavuvi Walioacha Uvuvi Haramu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wavuvi wengi waliokuwa wakiendesha shughuli za uvuvi haramu katika visiwa vyetu vya Zanzibar wameitikia wito wa kuacha uvuvi haramu na kwa kuwa uvuvi huo ulitokana na kutokuwa na zana za kisiasa za uvuvi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wavuvi hao vifaa vya kisasa vya uvuvi ili waweze kuendesha shughuli zao kwa uhalali bila ya kuathiri mazingira ya viumbe vinavyoishi majini na nchi kavu.

(b) Serikali inatoa ushauri na usaidizi gani kwa vijana waliokuwa wavuvi baada ya kuacha uvuvi haramu na sasa wanazurura mitaani pasipo na shughuli.

(c) Kutokuangalia sekta hiyo kwa upana zaidi na kwa miaka mingi hivi sasa ni kuendeleza soko au kuua soko la uvuvi nchini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia leo kufika katika Baraza lako tukufu nikiwa katika hali ya uzima, lakini kwa idhini yako, naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni, swali lake nambari 70 lenye vifungu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara kuanzia mwaka 2007/2014 iliweka mpango wa kuwawezesha wavuvi wa vijiji mbali mbali kwa kuwapatia taaluma za Ujasiri amali kwa kushirikiana na walimu kutoka vyama vya ushirika, kuwapatia kazi mbadala mfano utalii, misitu, nakadhalika, pamoja na kuwapatia vifaa na zana mbali mbali za uvuvi. Hivi sasa Wizara yangu imo katika mchakato wa kuanzisha mradi ambao utaweza kuwaendeleza wavuvi kwa kuwapatia rasilimali mbali mbali ili waendelee shughuli zao.

Katika kuiangalia sekta ya uvuvi kwa hali ya juu zaidi, Wizara ina mpango wa kujenga diko na soko la kisasa la samaki katika eneo la Malindi kwa madhumuni ya kuboresha huduma za uvuvi na kuwapatia mazao ya baharini yaliyo bora kiafya yatokanayo na ajira zaidi kwa vijana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa sekta ya uvuvi ndio kimbilio la wananchi wanyonge kabisa katika kujipatia riziki, lakini bado nyenzo wanazotumia ni duni. Ni lini watawezeshwa zana za kisasa ili waweze kuvua katika bahari kuu, hilo moja.

Mhe. Spika, la pili, bajeti ya mwaka jana Wizara ya Kazi Uendeshaji ilieleza katika Baraza hili kuwa kuna boti mbili za kisasa, je, mpango ule bado upo maana yake huku wavuvi wanatuuliza, je, hizo boti zipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana, naomba swali la kwanza Mhe. Jaku, alirejee kwa sababu sikulisikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali la kwanza niliuliza, kwa kuwa sekta ya uvuvi ndio kimbilio la wananchi wanyonge kabisa katika kujipatia riziki, lakini bado nyenzo wanazotumia ni duni, ni lini watawezeshwa zana za kisasa ili waweze kuvua katika bahari kuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, Wizara yangu hivi karibuni imepeleka vijana 25 kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Kuu ili kuweza kujifunza uvuvi wa bahari kuu, lakini hiyo ni mwanzo kwa sababu tumetoa Zanzibar wavuvi 13 na Bara wametoa 12 ili tuweze kusafundisha kwenda kuvua bahari kuu. Sasa baada ya kujua mafunzo ya kuweza kuvua bahari kuu kukamilika, ndio sasa Wizara yangu itawawezesha ili hata zile meli za nje zinazokuja kuomba vibali kuwaingiza na kuweza kupata ajira kwa ukamilifu zaidi.

Mhe. Spika, lakini swali la pili, meli zile bado mchakato unaendelea na kwa sababu hiyo, basi wengi waliomba na tumepata sasa hivi mtu, lakini vile vile, bado pesa zile kutokana na boti hazikutosheleza. Zilikuwa zitosheleze boti mbili, lakini kwa mujibu wa pesa zilizowekwa ni kutosheleza boti moja tu kwa sasa hivi, lakini serikali bado inatafuta katika nchi ya Sri Lanka kuweza kujua ni kiasi gani boti itaweza kugharimu na kuweza kupata boti ambazo zitaweza kukidhi mahitaji kwa wananchi wetu.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante, kwa kunipa na mimi fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amesema kuanzia tangu 2007, Wizara yake ina mpango wa kuwawezesha wavuvi na kwa kuwa katika kijiji cha Tumbe kina wavuvi wengi ambao asilimia 70 wanategemea sekta hii ya uvuvi. Je, Mhe. Waziri, vingapi ambavyo umeviwezesha katika kijiji kile cha Tumbe, hasa katika mpango mulioufanya wa kuwajengea soko zuri la kisasa. Je, Mhe. Waziri, unanambia ni vikundi vingapi ulivyoviwezesha Tumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kutokana na swali lake Mhe. Bikame ni la takwimu na sasa hivi takwimu sitokuwa nazo na vile vile kwa sababu nimeviwezesha vikundi vingi, naomba mara tu baada ya kumaliza hapa niende kwenye mkoba ambavyo ninavyo hivyo niweze kumjibu kwa maandishi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante, kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa Kangani bado mara ya pili wapo wavuvi wa kike ambao wanavua uvuvi wa madagaa, lakini wanawake hao wameshindwa na vifaa vya kuvulia zikiwemo nyavu, vyombo vyengine vidogo vidogo pamoja na boti ya kusafiria. Je, Mhe. Naibu Waziri, unawaambia nini wananchi hao kwanza kwenda kuwaona na pili kuwapatia vifaa hivyo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza kabisa utakuwa wewe shahidi kabisa nilileta karatasi ili kila Mwakilishi ano nia ya kumtembelea jikoni niende na hiyo nimekwenda kwa Mhe. Mwanajuma Mdachi na nikawaona wavuvi hao, lakini jengine serikali sasa hivi kupitia Wizara yangu, bajeti ni ndogo sana haiwezi kuwasaidia chochote wavuvi wale, lakini hali itakaporuhusu na tutakapokuwa na bajeti nzuri tunaweza kuwasaidia.

Nam. 75

Vitendo vya Utovu wa Nidhamu vya Baadhi ya Watendaji wa ZAA

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana, kabla ya kuliondosha swali langu kwanza, nataka nitoe pole kwa Mhe. Waziri wa Fedha, kwa yaliyomkuta na ustahamilivu wake na umakini wake na kwa kuonewa kwake na Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege. Ninachoamini yeye ndie Waziri, dhamana anayewapa fedha hizi matokeo yake yakamkuta yeye yakamgeukia. Mhe. Waziri wa Fedha, pole sana kwa yaliyokutokea sio wewe tu, lakini na sisi wengine yametukuta.

Mhe. Spika, na ninachoamini kwa suala hili, sitopata jawabu na baada ya kushauriana na wenzangu, naomba kuliondoa suala hili.

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Spika: Swali limeondolewa na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Fedha, nazipokea hizo pole ulizozitoa.

Nam. 73

Kutekelezwa Ahadi ya Mhe. Waziri wa Ardhi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Muyuni limekuwa na migogoro ya mipaka ya Ardhi na Serikali iliweka ahadi Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Waziri, kwenda kwenye migogoro hiyo.

Je, serikali imefikia wapi juu ya utekekezaji ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati ndani ya chombo hiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Suala la mgogoro wa mpaka bado litachukua muda mrefu, kwa sababu bado tunaendelea kumalizia mipaka ya Wilaya. Hivi ni kwa sababu kitaalamu hatuwezi kuanza kwenye Shehia kwenda kwenye Mkoa. Lazima tuanze mikoa, wilaya, halafu ndipo tumalizie kwenye Shehia. Kwa hivyo, hili tutalishughulikia tutakapomaliza hatua ya Wilaya na kwa sasa tuko katika hatua nzuri za kumalizia mipaka ya wilaya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kuvunja moyo na ya kutokuridhisha katika chombo hiki hiki, suala hili ananambia nilitizame kwa muda mrefu, leo pana nguzo Pete imeanguka ambayo yeye ndie Naibu Waziri, dhamana miezi 6 ananambia hivi hivi atakwenda na atachukua. Hili suala la ardhi nimeahidiwa katika chombo hiki hiki, suala la nguzo miezi 6, usalama wa wananchi wa Pete uko hatarini, alinambia litachukuliwa. Kwa kuwa serikali itakuwa haina jawabu. Kwa kuwa migogoro siku zote ya ardhi ndio maendeleo ya wananchi kuchelewa kupima mipaka si kuwanyima haki wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali ina utaratibu na katika utaratibu mmoja wakupitia Wizara yangu, ni kuipima hii mipaka kama vile ambavyo nimeeleza hapo awali. Ni kweli kuna mgogoro kati ya mipaka ya Wilaya ya Kusini, ikiweko katika eneo hili la Pete, lakini Wizara yangu imechukua jitihada ya kulifatilia suala hili na tumeona hali halisi ya mgogoro ulivyo, lakini tuko katika hali ya kurekebisha migogoro hiyo, pamoja na kupima mipaka kwa misingi ambayo itakuwa mizuri zaidi.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali namba mbili hajajibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba Mhe. Jaku, alirejee swali lake la pili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, katika chombo hiki hiki hata wiki mbili hazijatimia, nilikuripotia katika swali langu la msingi kuhusu nguzo Pete imeanguka, miezi 6 utendaji wa Shirika lako na ukaniahidi utachukua hatua katika chombo hiki hiki cha wananchi, wananchi wa Pete wananisikia nguzo ile bado hujachukua hatua ni hatari kwa maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ahsante, pamoja na kwamba swali hili liko tofauti na swali alilouliza linalohusiana na mipaka, lakini suala linalohusiana na nguzo za umeme, basi tayari nimekaa na watendaji wangu na tutalishughulikia suala hili, wakati wowote nitaenda, lakini kama tunavyoelewa kwamba utaratibu wa kazi, basi unakwenda katika misingi ambayo inayostahiki. Si kwamba tatizo limekuja sasa hivi ikesha wakati ule ule tulishughulikie ni kwamba kuna matatizo mengine yaliyotangulia tunayaanzia yale na hatimaye tutamalizia. Kwa hivyo, Mhe. Jaku, kwa hili atustahamilie tuko katika harakati za kulishughulikia suala lake la kuziweka sawa nguzo zake za umeme.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, pamoja kuongezea aliyoyajibu Mhe. Naibu Waziri, ni kwamba sasa hivi tuko katika operesheni ya kushughulikia nguzo mbovu zote zilizoanguka na nyenginezo na hiyo kazi hivi nazungumza ndio inaendelea. Kwa hivyo, astahamili kidogo nguzo itawekwa. Hata hivi asubuhi kama watu walisikiliza redio ni kwamba leo wameanza kuziingilia nguzo za Mkoa wa Kusini. Tunatengeneza nguzo zote ambazo mbovu tunazizika upya nyengine ambazo ni nzima.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kama kustahamili, nimestahamili miezi 6, lakini naiambia Wizara yake haiko tayari kutumikia wananchi na hamnifanyii ihsani, ni wajibu wake. Leo miezi 6 swali limesharipotiwa, hakuna hatua iliyochukuliwa tunawaambia nini wananchi.

Mhe. Spika: Sasa sijui swali la nyongeza la ngapi. Ufafanuzi zaidi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Mhe. Jaku, ni mwanasiasa mwenzangu, Shirika linaendeshwa na watendaji hata kuninon'goneza hajaninon'goneza kama kuna tatizo hilo, wakati mimi ndio ninayeshughulika na masuala hayo mimi sina mashetani kujua mahala fulani kuna nguzo ishang'oka na mahala fulani kuna hivi, mimi ninajua kuna *program* ya kushughulika masuala ya nguzo mbovu. Kwa hivyo, yeye Mhe. Jaku, angekuja kunieleza mimi, ee bwana wee, watu wako wale wazembe hawajashughulikia nguzo kule, nishawaambia sasa hivi mwezi mmoja angeona kama ingekuwa mpaka leo ipo hiyo nguzo, ingekuwa ishatengenezwa zamani hiyo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku, nenda Ofisini mkanon'gonezane na Mhe. Waziri. Tunakushukuru Mhe. Waziri na Naibu Waziri, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kama kawaida yetu na leo tuna wageni ambao wako pale juu, wageni hawa ni wanafunzi kutoka Skuli ya *Alhidaaya,* iko katika eneo hili hili la Chukwani, wanafunzi hawa wamekuja Barazani kwa lengo la kujifunza mambo mbali mbali ya Baraza na kujionea shughuli za Baraza zinavyoendeshwa. Idadi ya wanafunzi hao ni 20. Aidha, wameongozwa na walimu wao wawili. Naomba tutambue kuwepo kwao wako pale juu, nawaomba wasimame. Wale pale hao ni wanafunzi wanakuja kujifunza kwa wazee wao namna shughuli tunavyoendesha kwa ajili yao. Vijana nawashukuru sana pamoja na walimu. Ahsanteni sana, karibuni. Baada ya hapo, sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa heshima naomba ruhusa yako kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu, likae kama Kamati ili lipokee, lijadili na lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana hapa leo tukiwa katika afya njema, amani na utulivu nchini kwetu. Kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein) kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa hekima na busara kwa mwaka wanne, sasa chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Pia, napenda kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad) na Makamu wa Pili wa Rais (Balozi Seif Ali Iddi) kwa ushauri wao katika kuiongoza na kuiletea maendeleo nchi yetu. Kwa kweli, umoja wetu wa kimaamuzi na kimatendo ni silaha kubwa kwa Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Mhe. Spika, aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa busara na juhudi zako za makusudi unazochukua kuliendesha Baraza hili tukufu kwa kusaidiana na Mhe. Naibu Spika, Katibu na Maafisa wa Baraza lako katika kutekeleza majukumu yako. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza pamoja na Wajumbe wote kwa michango yao na ushirikiano wao mzuri wanaotoa kwa Wizara yangu. Pongezi za pekee ziende kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa jinsi inavyotuongoza katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini kwa pamoja shughuli za kuziendeleza sekta za mifugo na uvuvi ili kuona sekta hizo zinatoa fursa zaidi za ajira na tija kwa Wajasiriamali waliomo katika sekta zetu hizi.

Mhe. Spika, maelekezo na ushauri wa Kamati yetu hii imekuwa ni chachu muhimu katika kushajihisha wafanyakazi wa wizara yangu pamoja na wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani na wadau wengine wa sekta hizi kufanya kazi kwa pamoja na kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii maalum kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Magogoni kwa kuendelea kushirikiana nami nikiwa Mwakilishi wao katika kuendeleza majukumu yetu ya kuleta maendeleo na kupunguza umasikini katika jimbo letu na Taifa kwa jumla. Napenda kutoa wito kwa wananchi wa jimbo langu hili, kuendelea kunipa mashirikiano na kufanyakazi kwa pamoja ili kuzidi kuondoa matatizo yanayolikabili jimbo letu. Kwani umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Mhe. Spika, azma kuu ya Wizara yangu ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa za mifugo, uvuvi, uzalishaji mwani na mazao mengine ya baharini ili kuleta tija kwa wadau husika na kuongeza pato la Taifa na kuchangia kuwepo uhakika wa chakula pamoja na kufanikisha malengo ya MKUZA II, Maendeleo ya Milenia, Mpango Mkakati na Mpango Kazi wa Wizara yangu katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

HALI YA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI NCHINI

SEKTA YA MIFUGO

Mafanikio katika sekta ya mifugo

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, sekta ya mifugo imeweza kupata mafanikio mbali mbali yakiwemo:-

i. Kuongezeka uzalishaji wa maziwa kutoka tani 24,343 mwaka 2012 hadi kufikia tani 27, 243 kwa mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka huu;

ii. Kuongezeka uzalishaji wa mayai kutoka tani 9,663 mwaka 2012 hadi kufikia tani 10,992 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 14 kwa mwaka huu;

iii. Kuongezeka uzalishaji wa nyama ya ng'ombe kutoka tani 4,338 mwaka 2012 hadi tani 4,966 mwaka 2013, ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 15 kwa mwaka; na

iv. Kudhibiti maradhi ya mifugo.

Mhe. Spika, Sekta ya Mifugo imeweza kukua kwa asilimia 3.1 na kuchangia asilimia 3.8 ya pato la Taifa kwa mwaka 2013 kwa kiwango kilekile cha pato la Taifa la asilimia 3.8 kwa mwaka 2012.

Changamoto katika Sekta ya Mifugo

Mhe. Spika, licha ya kuwepo kwa mafanikio hayo, sekta ya mifugo imekabiliwa na changamoto mbali mbali katika utekelezaji zikiwemo:-

i. Kutowafikia baadhi ya wananchi wanaohitaji huduma za ugani kutokana na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi, ikiwemo vyombo vya usafiri kwa watoa huduma za ugani;

ii. Ukosefu wa mitaji kwa Wajasiriamali wa mazao ya mifugo sambamba na ongezeko la bei kubwa ya mifugo bora kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wafugaji wapya;

iii. Uhaba wa malisho ya mifugo hasa wakati wa kiangazi na uchache wa maeneo ya malisho; na

iv. Kuongezeka kwa matukio ya wizi wa mifugo hali inayowarudisha nyuma wafugaji na kuwaongezea mzigo wa kazi kwa kuimarisha ulinzi.

Mwelekeo wa baadae katika sekta ya mifugo

i. Mhe. Spika, kwanza kuimarisha kazi za utafiti kwa kuzalisha ng'ombe bora na wanaostahamili mazingira ya Zanzibar;

ii. Kuandaa mazingira ya kuifanya sekta ya mifugo kuwa muajiri mkubwa kwa kundi la vijana kwa kuwapatia ng'ombe bora wenye faida kubwa, kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali ikiwemo *Heifer International* na wawekezaji;

iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za elimu kwa wafugaji kwa kuwapatia elimu na teknolojia mpya na rahisi; na

iv. Kuimarisha miundombinu ya mifugo kwa kujenga majosho mapya, vituo vya karantini, maabara za mifugo na kukarabati vituo vya kutolea huduma.

SEKTA YA UVUVI

Mafanikio katika sekta ya uvuvi

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya uvuvi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

i. Kuongezeka kwa shughuli za uvuvi kutokana na kuongezeka kwa wavuvi. Hivyo, kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa na wananchi wengi kushajiika na kujiingiza katika ufugaji wa mazao ya baharini;

ii. Kuvuliwa kwa tani 41,952 za samaki kwa kipindi cha miezi tisa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambazo zimewaingizia wavuvi jumla ya shilingi bilioni 153,460,624,506;

iii. Kukubaliwa mradi wa ujenzi wa Soko la Kisasa la Samaki Malindi ambao utagharamiwa na SMZ na Serikali ya Japan. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka 2014/2015 na kukamilika mwaka 2015/2016;

iv. Kufanyika kwa doria za anga katika bahari kuu kwa kushirikiana na Idara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, (JWTZ, KMKM);

v. Kufanyika kwa doria moja shirikishi ya majini iliyowahusisha maafisa wakaguzi wa bahari kuu kutoka

Tanzania, Comoro, Madagascar, Seychelles, Reunion na Mauritius. Meli ya doria ilikaa katika maji ya Tanzania kwa siku nane. Shughuli hii imesimamiwa na Mamlaka ya Bahari Kuu;

vi. Kusomesha wavuvi vijana 13 kwenye Chuo cha Uvuvi Mbegani kuhusiana na Uvuvi wa Bahari Kuu. Wavuvi wengine 12 watasomeshwa kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa fedha. Mafunzo haya yanadhaminiwa na Mamlaka ya Bahari Kuu;

vii. Kuanza kwa ujenzi wa bwawa moja la mfano kama bwawa darasa *(demonstration pond)* katika eneo la Donge Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo ujenzi umefikia asilimia 80;

viii. Kuwapatia wafugaji wa mazao ya baharini jumla ya vifaranga vya samaki 20,546 Unguja na Pemba ambapo vifaranga 19,750 vimetolewa kwa Pemba na 796 kwa Unguja, ili kuongeza uzalishaji wa samaki;

ix. Jumla ya kilo 2,116 za samaki wa kufugwa katika mabwawa wamevuliwa Unguja na Pemba ambapo kilo 1,650 kwa Pemba na Unguja kilo 466 na kuwaingizia wafugaji kiasi cha shilingi 9,195,000; na

x. Wizara imeendelea kushirikiana na Washirika mbali mbali wa Maendeleo kama vile *FAO, KOICA* na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta ya mazao ya baharini. Aidha, hati za makubaliano *(Memorandum of Understanding)* zimesainiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Wizara ya Mifugo na Uvuvi unaojumuisha uanzishwaji wa vituo vya utafiti wa viumbe vya baharini pamoja na ziara za kimafunzo kwa viongozi na maafisa wa sekta ya uvuvi nchini China.

Mhe. Spika, shughuli za uvuvi zimekuwa kwa asilimia 4.4 kwa mwaka 2013 kutoka asilimia 2.3 kwa mwaka 2012 na mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 7.1 mwaka 2012 hadi asilimia 7.2 mwaka 2013.

Changamoto Katika Sekta ya Uvuvi

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza sekta ya uvuvi katika mwaka wa fedha 2013/2014, sekta hii imekabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo:-

i. Kuongezeka kwa shindikizo la uvuvi katika maeneo ya hifadhi kutokana na vijana wengi kujiunga katika shughuli za uvuvi;

ii. Kuongezeka kwa uvuvi haramu kutokana na kuwepo kwa wavuvi kutoka nje ya Zanzibar na wavuvi vijana, wazawa katika maeneo ya hifadhi na kuvua uvuvi haramu na kusababisha uharibifu wa mazingira ya bahari;

iii. Kupauka kwa matumbawe *"Coral bleaching"* kunako sababishwa na mabadiliko ya tabianchi;

iv. Kupungua mazalio ya samaki kunakotokana na uharibifu wa ukataji wa mikoko fukweni, hali inayoathiri kuwepo kwa tatizo la vifaranga kwa wafugaji wa samaki;

v. Ukwamaji wa nyavu katika matumbawe baharini;

vi. Bei ndogo ya zao la mwani;

vii. Uhaba wa upatikanaji wa vifaranga vya samaki unakwamisha juhudi za wananchi wanaoingia katika shughuli ya ufugaji wa samaki;

viii. Uwezo mdogo wa jamii wa kuekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini kutokana na gharama kubwa za uwekezaji, uhaba wa taaluma na nyenzo za kufanyia kazi katika fani ya ufugaji wa mazao ya baharini;

ix. Kupungua kwa uzalishaji wa mwani Unguja kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa; na

x. Uhaba wa miundo mbinu ya ufugaji wa samaki.

Mwelekeo wa Baadae Katika Sekta ya Uvuvi

i. Kuendeleza miundombinu ya ufugaji wa samaki na kutoa taaluma kwa Wajasiriamali wa mazao ya baharini juu ya njia bora za ufugaji wa mazao ya baharini;

ii. Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kukuza na kuendeleza sekta ya ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo kuwekeza katika ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini;

iii. Kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake na kutoa ushauri wa kitaalamu katika harakati za ufugaji wa viumbe vya baharini;

iv. Kuongeza kipato cha samaki wa kufuga badala ya kutegemea samaki wanaovuliwa moja kwa moja kutoka baharini pekee;

v. Kutayarisha mpango wa kuvifanya vijiji vya Chwaka na Marumbi kuwa mfano wa vijiji vya uvuvi;

vi. Kuendeleza wavuvi vijana kuvua bahari kuu;

vii. Kuendeleza tafiti katika zao la mwani na matumbawe ya kienyeji; na

viii. Kuendelea na uwekaji wa matumbawe ya kienyeji katika maeneo ya hifadhi.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza malengo iliyojipangia kupitia Idara zake sita kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Majukumu ya Idara hii ni kuandaa, kutekeleza na kutathmini mipango, programu, sera na miradi ya maendeleo pamoja na kuratibu shughuli za utafiti katika sekta za mifugo na uvuvi na kuendeleza mashirikiano na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mipango ya utekelezaji wa malengo ya sekta ya mifugo na uvuvi;

ii. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo na uvuvi;

iii. Kuratibu kazi za utafiti wa mifugo na uvuvi;

iv. Kufanya mapitio ya Sera ya Uvuvi na mazao ya baharini; na

v. Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Mpango Kazi wa Wizara wa mwaka 2013/14, uliandaliwa pamoja na kutayarisha Ripoti za Utekelezaji wa Mpango huo kwa kila robo mwaka na mwaka mzima kwa jumla. Vile vile, Idara imeweza kuupitia Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2011/12- 2013/14 na kutayarisha Mpango Mkakati Mpya wa miaka miwili 2014/15 – 2015/16 ambao utakwenda sambamba na kukamilika kwa utekelezaji wa MKUZA II;

ii. Washiriki 62 Unguja na Pemba wakiwemo wafanyakazi na wavuvi wamepatiwa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi pamoja na kufuatilia kazi ya ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi katika vyanzo vyake mbali mbali ikiwemo madikoni, machinjioni na vituo vya uzalishaji na karantini. Aidha, Wizara yangu inashiriki katika utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Takwimu za Kilimo Tanzania (*Strengthening of Agricultural Statistics in Tanzania*) na mfanyakazi mmoja ameweza kushiriki katika ziara ya kimafunzo nchini Msumbiji kwa lengo la kuimarisha takwimu za kilimo kwa jumla zikiwemo za mifugo na uvuvi;

iii. Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Baharini kutoka China *"State Oceanic Administration",* imekubaliana kuendeleza shughuli za utafiti wa baharini. Aidha, utafiti wa maradhi ya kiwele kwa ng'ombe, na utafiti wa kuku chotara unaendelea;

iv. Utayarishaji wa Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini unaendelea kutekelezwa na Mradi wa *SMARTFish*; na

v. Mashirikiano na taasisi za ndani na nje yameendelezwa kwa kushiriki vikao tofauti vya ndani na nje ya nchi. Baadhi ya vikao hivyo ni pamoja na vile vya Tanzania na Afrika Kusini na vikao vya Afrika Mashariki. Ushiriki wetu katika vikao vyote hivi tumeweza kubadilisha uzoefu wa kiutendaji, kutoa mapendekezo yetu ya kisera na kimkakati katika kuendeleza sekta zetu za mifugo na uvuvi pamoja na kutafuta fursa za kupata misaada ya kusaidia utekelezaji wa malengo yetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya shilingi 206,026,000 kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya hizo, shilingi 73,328,000 ni kwa mishahara na shilingi 132,698,000 ni kwa matumizi mengineyo.Hadi kufikia mwezi Machi 2014, jumla ya shilingi 67,714,600 zimepatikana kwa kulipia mishahara na shilingi 31,300,000 sawa na asilimia 24 kwa matumizi mengineyo (Kiambatisho Nam. 1). Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Idara ilipangiwa kutumia shilingi 200,000,000 kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo (Kiambatisho Nam. 2) na hadi kufikia Aprili 2014 mradi huu ulishapatiwa shilingi 94,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 47 ya makadirio (Kiambatisho Nam. 2 na 3)

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inalenga yafuatayo:-

i. Kuimarisha mipango ya utekelezaji wa malengo ya sekta ya mifugo na uvuvi;

ii. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo na uvuvi;

iii. Kuchapisha nakala 1,000 za Jarida la Mvuvi na Mfugaji;

iv. Kuratibu kazi za utafiti; na

v. Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya shilingi 162,728,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 101,928,000 ni mishahara na shilingi 60,800,000 ni kwa matumizi mengineyo (Kiambatisho Nam. 4).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara pia itatekeleza Programu moja ya Kuendeleza

Miundombinu ya Ufugaji, ambayo inaombewa jumla ya shilingi 80,000,000 (Kiambatisho Nam. 2 na 5).

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepangiwa majukumu ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa kazi za kila siku za Wizara, kuweka kumbukumbu za wafanyakazi, kutunza mali za Serikali zilizokabidhiwa Wizara, kusimamia kupatikana kwa haki za wafanyakazi ambao nao wanalazimika kutimiza wajibu wao na kuhakikisha kwamba sheria, Kanuni na taratibu zote zinazohusu matumizi ya mali za Serikali ndani ya Wizara zinafuatwa. Idara inawajibika kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi, kuratibu kazi za uhasibu, manunuzi, ukaguzi wa ndani wa hesabu za Wizara na kusimamia Mambo Mtambuka kama Jinsia, UKIMWI, Mazingira, Ulemavu, Utawala bora na kadhalika.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili 2014, wizara hii ilikuwa na wafanyakazi 752. Wafanyakazi 526 wapo Unguja na 191 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi hawa, 226 sawa na asilimia 30 ni wanawake na 526 sawa na asilimia 70 ni wanaume (Kiambatanisho Nam. 6). Idadi hiyo ni pamoja na wafanyakazi wapya 7 walioajiriwa na Wizara kwa kujaza mapengo kwa nafasi zilizokuwa wazi. Wafanyakazi 3 wamestaafu, mmoja amefukuzwa kazi na mmoja (1) amefariki akiwa mtumishi wa umma. Mwenyezi Mungu amlaze Peponi, *Amin*.

Mhe. Spika, bado wizara yangu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi hasa wataalamu katika nyanja za utafiti, takwimu, elimu ya kuendesha uvuvi endelevu na madaktari wa mifugo. Hivi sasa wapo wafanyakazi 233 sawa na asilimia 31 waliohitimu kuanzia kiwango cha diploma na kuendelea ambapo mmoja (1) tu amefikia kiwango cha Shahada ya tatu (*PhD*) na mmoja mwengine yupo masomoni, 27 wamefuzu katika kiwango cha Shahada ya pili (*MSc*), 30 Shahada ya kwanza (*BSc*), 6 Stashahada ya uzamili (*PGD*), 5 Stashahada ya juu (*Advanced Diploma*) na 164 katika Stashahada ya kawaida - *Ordinary Diploma* (Kimbatanisho Nam. 7).

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi, kwa kuwapatia wafanyakazi nyenzo zitakazowezesha kufanyika kazi kwa ufanisi;

ii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Idara na Wizara kwa ujumla kwa viongozi wa wizara kutembelea na kukagua utendaji kazi katika vituo mbali mbali;

iii. Kuendelea kusimamia udhibiti wa mali za Serikali na kuyapatia hatimiliki maeneo ya Wizara;

iv. Kuendelea kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi; na

v. Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika nyanja mbali mbali za uzalishaji na utabibu wa mifugo, uzalishaji wa mazao ya baharini, uvuvi, utawala, uchumi na mambo mtambuka.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imewasiliana na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, imenunua na kuvitengeneza vifaa mbali mbali kama vile kompyuta na magari, imeendesha vikao vya kikazi pamoja na tathmini ya utendaji kazi, kulipia gharama za maji na umeme, kushiriki katika matokeo mbali mbali ya Kitaifa kama vile maonyesho ya kuadhimisha kutimia miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na kuhudhuria katika maonyesho ya nane nane Tanzania Bara kwa kujifunza kutokana na kazi za wenzetu tunaolingana nao. Aidha, Idara imesimamia ufungaji wa mahesabu ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kila robo mwaka, imeendesha vikao 2 vya Kamati ya Uongozi vya Wizara, imehudumia vikao vya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya

Baraza la Wawakilishi na *PAC* zinapotathmini kazi za Wizara na kuhakikisha kuwa Kamati hizo zinaweza kufanya kazi zake kama zilivyojipangia;

ii. Viongozi wa Wizara wamewatembelea na kushauriana na wadau mbali mbali wa sekta za Mifugo na Uvuvi. Vikundi 10 vya wazalishaji vimepatiwa misaada kwa kuendeleza shughuli zao na Wizara;

iii. Kwa kuendeleza mchakato wa kuyadhibiti maeneo ya serikali yanayosimamiwa na Wizara yangu, maeneo 4 yamepimwa, eneo 1 limelipiwa ada ya kupatiwa Hati Miliki ambapo maeneo hayo ni ikiwa pamoja na eneo la Ofisi ya Dunga, eneo la kuwekea ng'ombe wa kukamua mbegu bora kwa upandishaji kwa sindano (i) Mtoni, Karantini ya Kisakasaka na eneo la Karantini ya Nzi wengi Pemba;

iv. Wafanyakazi 34 wamerekebishiwa mishahara yao na kwa pale yalipojitokeza makosa taarifa za kufanyiwa marekebisho zimewasilishwa kwenye taasisi husika kwa kufanyiwa masahihisho. Wafanyakazi 15 wanalipwa fedha zao za likizo na posho ya kufanyakazi masaa ya ziada hasa kwa wafanyakazi wa ngazi za chini wanaostahiki kupewa maposho hayo; na

v. Wafanyakazi 25 wameendelezwa kwa kupatiwa na kulipiwa masomo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na 6 wamelipiwa ada na mahitaji mengine kwa masomo ya muda mfupi. Jumla ya wafanyakazi 13 wamepatiwa fursa ya kuhudhuria semina nje ya nchi hasa Uchina.Wafanyakazi 60 wamepatiwa warsha juu ya elimu na taarifa kuhusu UKIMWI.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, liombewa jumla ya shilingi 701,768,000 kwa kutekeleza shughuli za kawaida. Kati ya hizo shilingi 352,723,000 ni kwa mishahara na shilingi 349,045,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 shilingi 347,742,100 zimepatikana kwa kulipia mishahara na jumla ya shilingi 200,418,000 sawa na asilimia 57 zimepatikana kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 1)**

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea na uimarishwaji wa mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia wafanyakazi nyenzo zitakazowezesha kufanyika kazi kwa ufanisi;

ii. Kuendelea na ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji wa kazi za Idara na wizara kwa ujumla na kusaidia vikundi au watu binafsi;

iii. Kuendelea kusimamia udhibiti wa mali za serikali na kuyapatia hatimiliki maeneo yaliyobaki ya wizara;

iv. Kuendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za mapato na matumizi ya fedha na zana za serikali;

v. Kuendelea kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi;

vi. Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika nyanja mbali mbali za uzalishaji na utabibu wa mifugo, uzalishaji wa mazao ya baharini, uvuvi wa bahari ya kina kirefu, utawala, uchumi na mambo mtambuka;

vii. Kulipa gharama za madeni ikiwemo malipo ya matrekta na;

viii. Kushiriki katika maadhimisho mbali mbali ya kiserikali, taasisi za Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya shilingi 1,047,681,000 kutoka serikalini kwa kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 627,004,000 ni

kwa mishahara na shilingi 420,677,000 kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 4)**

IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO

Mhe. Spika, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu za maendeleo ya mifugo. Idara hii hutoa taaluma ya ufugaji bora wa mifugo na kufanya utafiti juu ya changamoto zinazojitokeza katika sekta ya mifugo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake, ili kuwa na ufugaji wenye tija kwa wafugaji, jamii na Taifa kwa ujumla. Pia, Idara hii ina jukumu la kuendeleza mifugo ya asili kwa kuimarisha koosafu za mifugo yetu ya asili ili iweze kuzalisha zaidi.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara ya Uzalishaji Mifugo ililenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuongeza uzalishaji mifugo na mazao yake kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

   i. Kuimarisha huduma za ugani (elimu kwa wafugaji);

   ii. Kuvijengea uwezo vituo vya utafiti wa mifugo; na

   iii. Kuongeza thamani na ubora wa mazao na bidhaa za mifugo.

b) Kuongeza mwamko wa matumizi mazuri ya samadi kama nishati mbadala kwa kutumia mikakati ifuatayo.

   i. Kuchangia ujenzi wa mitambo 14 ya *biogesi*;

   ii. Kuitangaza teknolojia ya *biogas* kwa jamii kupitia kipindi kimoja cha redio na kimoja cha Televisheni; na

   iii. Kutathmini ubora wa mitambo ya *biogesi* iliyofungwa;

c) Kuimarisha utoaji huduma za mifugo kwa jamii kwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

   i. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi; na

   ii. Kuimarisha ufuatiliaji wa kazi za Idara.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa malengo haya hatua mbali mbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na mambo yafuatayo:-

   i. Kazi ya kutoa elimu kwa wafugaji kwa kutumia njia mbali mbali iliendelea Unguja na Pemba. Idara ilitumia njia mbali mbali kutekeleza kazi hii ikiwa ni pamoja na kuwatembelea wafugaji au/na vikundi vya ufugaji katika mashamba yao, kutumia redio na televisheni, ziara za wafugaji kwa wafugaji miongoni mwao na mashamba darasa;

   ii. Jumla ya wafugaji 19,670 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa ufugaji kitaalamu ikiwa ni pamoja na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku na bata, hili ni ongezeko la asilimia 9% ya wafugaji waliofikiwa na kupatiwa ushauri ukilingasha na mwaka uliopita. Wafugaji 20 walipatiwa mafunzo ya kuhifadhi malisho na umuhimu wake. Aidha, kulifanyika ziara 3 za mafunzo ya kutembeleana baina ya wafugaji wa kisiwani Pemba;

iii. Idara kwa kushirikiana na Mwekezaji Ndugu Said Bakhresa walifanya uchambuzi yakinifu *(Feasibility study)* ya biashara ya maziwa nchini ili kujua uwezo wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya Kiwanda cha Maziwa kitachofunguliwa hivi karibuni huko Fumba. Kutokana na matokeo ya uchambuzi huo, Idara imeanzisha mkakati wa kuwataarifu wafugaji juu ya fursa hii ya kuwa na soko la uhakika wa maziwa yao na kuwaelimisha umuhimu wa kuzalisha bidhaa bora kwa soko hilo;

iv. Ili kufikia lengo la kuwa na ng'ombe wachache, lakini wanaozalisha maziwa mengi, Idara iliendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano ambapo hadi kufikia Aprili, 2014 jumla ya ng'ombe 2,385 walishapandishiwa, kati yao 1,623 wameshika mimba ikiwa ni asilimia 68 ya ng'ombe wote waliopandishiwa. Kati ya ndama waliozaliwa, ndama 409 wamewekewa kumbukumbu za wazazi wao na uzalishaji wa maziwa **(Kiambatisho Nam. 8);**

v. Idara iliendelea kuyapatia huduma muhimu mashamba na vituo vya mifugo ambapo ng'ombe na mbuzi walioko katika mashamba ya Pangeni, Kitumba na Chamanangwe walikingwa na kutibiwa magonjwa mbali mbali. Aidha, ukarabati wa Ofisi ya wafanyakazi katika Kituo cha Malisho Kizimbani na Banda la mbuzi katika shamba la Kitumba unaendelea. Jumla ya ekari 8 za majani ya aina mbali mbali amepandwa kwa ajili ya kuwapatia wafugaji mbegu bora za malisho;

vi. Wafugaji 7 walipatiwa ng'ombe bora wenye damu mchanganyiko kutoka katika Shamba la Kuzalisha Mitamba Pangeni;

vii. Kazi ya kuhamasisha na kujenga mitambo ya *biogesi* ya aina ya mahandaki inaendelea Unguja na Pemba. Kwa kushirikiana na Kampuni ya Kuendeleza *Biogesi* Tanzania na wafugaji waliohitaji huduma hiyo, jumla ya mitambo 10 imejengwa ambapo mitambo 7 imejegwa Unguja na mitambo 3 Pemba. Mitambo hiyo imejengwa katika maeneo ya Kazole (Kaskazini B), Mbuzini, Kiembe Samaki, Chuwini, Fuoni, Jumbi (Magharibi), Ubago (Kati) kwa Unguja na kwa upande wa Pemba mitambo hiyo imejengwa katika maeneo ya Gombani, Wawi na Nanguji; na

viii. Katika kuongeza ufanisi wa kazi za Idara, vijana 6 wameajiriwa, 5 wamepangiwa katika kitengo cha Elimu kwa Wafugaji kama Afisa Wasaidizi Mifugo na mmoja kama Afisa Msaidizi Manunuzi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii ilikadiriwa kukusanya mapato ya shillingi 9,000,000 yatokanayo na huduma za uzalishaji mifugo. Hadi kufikia mwezi wa March, 2014 jumla ya shilingi 1,143,500 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 13 ya lengo lililowekwa **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Idara ya Uzalishaji Mifugo iliombewa jumla ya shilingi 565,637,000 kutoka serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shillingi 452,689,000 ni kwa mishahara na shilingi 112,984,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi March 2014 shilingi 372,129,850 zimepatikana kwa kulipia mishahara na shilingi 29,600,000 sawa na asilimia 26 zimepatikana kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1).**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo imetekeleza mradi mmoja wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano ambao uliombewa shilingi 100,000,000 na hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, mradi huu ulishapata shilingi 46,860,000 sawa na asilimia 47 **(Kiambatisho Nam. 3 na 10).**

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2014/2015, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha shughuli za utafiti katika masuala ya mifugo kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

   i. Kuvipatia madawa na vitendea kazi vituo vitatu vya utafiti;

   ii. Kufanya utafiti wa kuangalia uzalishaji wa kuku chotara wa nyama na kabila ya kiasili ya kuchi; na

   iii. Kufanya utafiti juu ya vikwazo vya ufugaji mbuzi, Kiuyu Mbuyuni Wilaya ya Micheweni.

b) Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wafugaji katika nyanja zote za utunzaji, uzalishaji ,usarifu wa bidhaa za mifugo na masoko kwa kutekeleza shughuli zifuatazo;

   i. Kuwawezesha wasaidizi mabwana mifugo 20 kuwafikia wafugaji 20,000;

   ii. Kutengeneza vipeperushi 5,000 vya taaluma mbali mbali za ufugaji wa kisasa, utunzaji bora wa ndama, umuhimu wa kukinga maradhi ya kiwele kwa ng'ombe wa maziwa, utunzaji wa mifugo kibiashara, umuhimu wa uwekaji kumbukumbu na kuvisambaza kwa walengwa;

   iii. Kutengeneza na kurusha hewani vipindi 4 vya Televisheni na Redio juu ya usarifu na masoko;

   iv. Kutoa mafunzo kwa wafugaji 20 juu ya uhifadhi wa malisho na faida zake; na

   v. Kufanya mikutano minne na wafugaji kuzungumzia changamoto na jinsi ya kukabiliana nazo.

c) Kuongeza uzalishaji wa mifugo na matumizi bora ya mazao ya mifugo kwa kutekeleza shughuli zifuatayo:-

   i. Kuanzisha mashamba *(plots)* 40 ya malisho kwa mfano katika kituo cha malisho Kizimbani;

   ii. Kulima na kupanda jumla ya eka 5 za majani katika kituo cha malisho Kizimbani na 5 katika shamba la Chamanangwe;

   iii. Kuchangia gharama za ujenzi wa mitambo 10 ya *biogesi*;

   iv. Kuitangaza teknolojia ya *biogesi* kwa jamii kupitia kipindi kimoja cha redio na kimoja cha televisheni; na

   v. Kutathmini ubora wa mitambo 10 ya *biogesi* iliyojengwa.

d) Kuimarisha utoaji huduma za mifugo kwa jamii kwa kutekeleza shughuli zifuatayo:-

   i. Kuziwezesha Ofisi za Idara kupata huduma za umeme na maji;

   ii. Kuiwezesha Ofisi kupata huduma za vifaa vya kuandikia na vya usafi;

   iii. Kuiwezesha Ofisi kupata huduma za simu na mtandao;

   iv. Kuiwezesha Ofisi kupata huduma za usafiri;

   v. Kufanikisha haki na fursa kwa wafanyakazi; na

   vi. Kuimarisha ufuatiliaji wa kazi za Idara.

e) Kuongeza ujuzi wa kitaalamu kwa wafanyakazi 8 na

f) Kuimarisha mahusiano ya Kimataifa, kikanda na Kitaifa katika sekta ya mifugo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Uzalishaji Mifugo inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 9,000,000 yatokanayo na huduma za uzalishaji mifugo. **(Kiambatisho Nam. 9)**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15, Idara inaombewa jumla shilingi 604,237,000 kutoka serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 106,273,000 zinaombwa kwa matumizi mengineyo na shilingi 497,964,000 kwa ajili ya mishahara. **(Kiambatisho Nam. 4).**

Aidha, Idara itatekeleza Mradi mmoja wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano ambao unaombewa shilingi 90,000,000 **(Kiambatanisho Nam. 5 na 10).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto itaendelea kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Wafugaji Wadogo Wadogo katika programu ya pamoja ya Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Programme*) ambao unatarajiwa kuzalisha nafasi za ajira 120 kwa vijana ambapo ajira 80 ni kupitia ufugaji wa kuku na ajira 40 ni kupitia ufugaji wa mbuzi wa maziwa na wa kienyeji. Mradi huu umetengewa shilingi 100,000,000 kutoka katika Programu ya Ajira kwa Vijana inayosimamiwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

IDARA YA HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO

Mhe. Spika, maendeleo ya sekta ya mifugo yanategemea sana afya za mifugo yetu. Aidha, mifugo ndio chanzo kikubwa cha maambukizo ya maradhi kwa binaadamu. Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ina jukumu la kudhibiti maradhi kwa mifugo yetu kwa kutoa huduma za kinga na tiba za maradhi ya mifugo. Idara pia ina jukumu la kuhakikisha mifugo yetu haisambazi maradhi kwa binadamu na kuilinda nchi yetu isipate maambukizi ya maradhi ya mifugo kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa wanyama wanaoingizwa nchini.Vile vile, Idara hii inasaidia kushajihisha jamii ili iondokane na vitendo vya ukatili wa wanyama na kufanya uchunguzi wa mwenendo wa maradhi ya kuambukiza na yenye kuathiri mifugo yetu, kubuni mbinu za kukabiliana na maradhi hayo na kufanya utafiti wa maradhi ya mifugo.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ililenga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendeleza udhibiti wa maradhi ya mifugo kwa kuimarisha vituo vya Karantini, maabara na vituo vya huduma za mifugo;

ii. Kuendeleza huduma za ugani kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama na maradhi ya kuambukiza, kupe na kuhamasisha wananchi juu ya kuzuia ukatili kwa wanyama; na

iii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao na vitendea kazi; na

iv. Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji wa kazi vijijini na kuweka takwimu na tathmini ya maradhi mbali mbali ya mifugo.

Utekelezaji wa Malengo kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitekeleza yafuatayo:-

i. Wanyama 2,455,177 walikaguliwa na kuruhusiwa kuingia nchini kupitia vituo vya Karantini. Kati ya wanyama hao, ng'ombe ni 5190, mbuzi ni 316, kuku (vifaranga vya mayai na vya nyama) 2,449,622 na wanyama wengineo 49.Aidha, mayai ya kuku kwa ajili ya mbegu 2,237,080 yaliingizwa nchini. Wanyama 137,974 walichanjwa (Unguja 91,062 na Pemba 46,912) na wanyama 51,370 walikogeshwa (Unguja 20,548 na Pemba 30,822) kwa lengo la kuwakinga na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na maradhi yanayosambazwa na kupe na

wadudu wengine wanaoathiri mifugo. Vile vile, wanyama 120,077 wametibiwa kutokana na maradhi mbali mbali ya mifugo, kati yao ng'ombe ni 15,970, mbuzi 7,862, kuku na jamii ya ndege 89,799, punda 758, mbwa 3,292 na paka 2,396. Aidha, mbwa 161 na paka 330 walifungwa uzazi kwa lengo la kupunguza wanyama wazururaji;

ii. Jumla ya vijana 40 *(Community Animal Health Workers-CAHWs*) kutoka wilaya zote za Unguja na Pemba na madaktari wasaidizi wa mifugo 20 wamepatiwa taaluma ya kinga na tiba. Aidha; vipindi 14 vya kuhamasisha jamii juu ya athari za kichaa cha mbwa vilirushwa hewani katika Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC TV*);

iii. Wafanyakazi 22 walipatiwa stahiki zao za likizo na 7 walilipwa posho za saa za ziada. Aidha, vifaa na madawa ya mifugo yamenunuliwa na kusambazwa vituoni; na

iv. Ufuatiliaji na uwekaji wa takwimu za mwenendo wa maradhi mbali mbali ya mifugo umefanyika yakiwemo maradhi yanayoenezwa na kupe, kutupa mimba, minyoo, maradhi ya kiwele, kichaa cha mbwa, maradhi ya kuku na maradhi ya mifugo yasiyokuwa na mipaka. Sampuli 1,800 za maziwa, 573 za damu, 1,011 za kinyesi na sampuli za 70 za samaki zimekusanywa na kupelekwa maabara kwa uchunguzi wa *bacteria* na minyoo. Aidha, sampuli 3,000 za uoteshaji wa "*bacteria*" na "*fungas*" umefanyika. Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa asilimia 46 ya ng'ombe waligunduliwa kuathiriwa na ugonjwa wa Kiwele.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 59,000,000 yatakayotoka na ada za huduma za utabibu wa mifugo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014, jumla ya shilingi 37,931,700 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 64 ya lengo lililowekwa. **(Kiambatisho Nam. 9)**

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2013/2014, Idara ya Utabibu wa Mifugo iliombewa jumla ya shilingi 605,598,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 510,829,000 ni mishahara na 94,769,000 ni kwa matumizi mengineyo.Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 shilingi 409,526,900 zimepatikana kwa kulipia mishahara na shilingi 25,700,000 sawa na asilimia 27 zimepatikana kwa matumizi mengineo. **(Kiambatisho Nam. 1)**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliendelea kutekeleza miradi miwili, Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege na Maradhi ya mifugo yasiokuwa na mipaka *(Trans-boundary Animal Diseases)* uliombewa shilingi 70,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, shilingi 39,200,000 sawa na asilimia 56 zimepatikana. **(Kiambatisho Nam. 3 na 11)**

Mhe. Spika, mradi wa pili, ni mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ambao uliombewa jumla ya shilingi 160,000,000. Kati ya hizo shillingi 60,000,000 ni fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na shilingi 100,000,000 ni kutoka kwa mshirika wa maendeleo *"World Society for Protection of Animals"* (*WSPA*). Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, shilingi 44,280,500 sawa na asilimia 74 zilitolewa na serikali na shilingi 91,600,000 sawa na asilimia 92 zimepatikana kutoka kwa *WSPA.* **(Kiambatisho Nam. 3 na 12)**

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inalenga kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuendeleza udhibiti wa maradhi mbali mbali ya mifugo kwa kuimarisha vituo vya karantini, maabara na vituo vya huduma za mifugo;
(ii) Kuimarisha utoaji wa huduma za tiba, kinga na uchunguzi wa kimaabara kwa maradhi ya mifugo;
(iii) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji, takwimu na tathmini ya maradhi ya mifugo na;
(iv) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia wafanyakazi stahili zao na vitendea kazi vilivyo bora.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 59,000,000 yatakayotokana na ada za huduma za utabibu wa mifugo. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2014/2015, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya shilingi 703,984,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 593,484,000 ni mishahara na 110,500,000 ni kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 4).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii itaendelea kutekeleza miradi miwili. Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege na Maradhi ya Mifugo yasiyokuwa na mipaka *(Trans-boundary Animal Diseases)* ambao unaombewa shilingi 67,000,00. **(Kiambatisho Nam. 5 na 11).** Na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ambao unaombewa jumla ya shilingi 280,873,000. Kati ya fedha hizo shillingi 25,000,000 ni fedha za SMZ na shilingi 255,873,000 zitatoka kwa Mshirika wa Maendeleo *WSPA*. **(Kiambatisho Nam. 5 na 12).**

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ina majukumu ya kuwahudumia wavuvi pamoja na wadau mbali mbali wanaojishughulisha na uvuvi kwa namna moja au nyengine kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi. Idara hii pia ina jukumu la kuhakikisha kuwa rasilmali za baharini zinalindwa kwa kuzingatia matumizi bora na endelevu. Idara pia ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria na Kanuni za uvuvi kwa lengo la kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za bahari na kuendeleza kazi za utafiti wa masuala ya uvuvi.

Mhe. Spika, usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi yanatekelezwa na kusimamiwa na vitengo vya Mipango, Maendeleo ya Uvuvi wa Kienyeji, Kitengo cha Doria, Afisi ya Uvuvi Pemba. Aidha, Kitengo cha Hifadhi ya Bahari *(MCU)* kinasimamia maeneo matatu ya Hifadhi za Bahari, yaani Hifadhi ya Ghuba ya Menai *(MBCA),* Hifadhi ya Mnemba na Ghuba ya Chwaka *(MIMCA)* na Hifadhi ya Mkondo wa Pemba *(PECCA).*

Malengo ya mwaka 2013/14

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2013/2014, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake;
(ii) Kuendelea kutoa taaluma ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii ya ukanda wa pwani juu ya uvuvi endelevu;
(iii) Kuwashajihisha wavuvi vijana kuacha kuvua katika maeneo ya hifadhi na badala yake kwenda kuvua katika maji ya kina kirefu;
(iv) Kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya hifadhi kwa kushirikiana na jamii; na
(v) Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ndani na nje ya nchi katika kukuza sekta ya uvuvi.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilifanya mafunzo juu ya udhibiti na utatuzi wa migogoro kwa wavuvi wa maeneo ya Hifadhi ya *MIMCA*, MENAI na *PECCA*;

(ii) Aidha, mikutano mbali mbali imeendelea kufanyika kwa shehia zote za MENAI, *MIMCA* na *PECCA* kwa lengo la kuwahamasisha wanajamii juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani na athari ya matumizi ya nyavu katika maeneo ya uhifadhi;

(iii) Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, imeendelea kufanya doria za kawaida ambapo jumla ya doria 292 za kila siku za kudhibiti na ukaguzi wa leseni pamoja na kuangalia shughuli za kitalii zinazoendelea katika kisiwa cha Mnemba na eneo la hifadhi ya MENAI. Aidha, doria 45 maalum za kuzuia na kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo yetu ya hifadhi za *MIMCA*, MENAI zimefanyika kwa kushirikiana na wanajamii, askari Polisi pamoja na kikosi cha KMKM. Katika doria hizo vyombo vitatu vyenye wavuvi 18 walikamatwa na makosa, 15 walipewa onyo la

kutokurejea kosa lao na kutaifishwa mitego yao. Aidha, wavuvi 3 kesi zao zinaendelea Mahakamani; na

(iv) Ukusanyaji wa takwimu za samaki ulifanyika. Jumla ya tani 41,952 za samaki wenye thamani ya shilingi 153,460,624,506 zimevuliwa.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki, Idara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 30,000,000/= kutokana na mapato ya leseni za vyombo na za wavuvi. Mpaka kufikia mwezi wa Machi, 2014 jumla ya shilingi 16,698,500 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 56 ya lengo. **(Kiambatisho Nam. 9).**
Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, jumla ya shilingi 379,526,000 ziliombwa Serikalini kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo, shilingi 297,026,000 ni mishahara na 82,500,000 ni kwa matumizi mengineyo. Mpaka kufikia mwezi wa Machi, 2014 jumla ya shilingi 265,520,300 zimepatikana kulipia mishahara na jumla ya shilingi 28,200,000/= zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 34. **(Kiambatisho Nam. 1).**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imetekeleza mradi mmoja wa Kuimarisha Uvuvi wa Kina Kirefu cha Maji ambao uliombewa shilingi 100,000,000 kutoka SMZ na hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, mradi huu uliingiziwa jumla ya shillingi 1,660,000 ambazo ni sawa na asilimia 2 ya makadirio. **(Kiambatisho Nam. 3 na 13).**

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2014/2015, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii ya ukanda wa pwani juu ya uvuvi endelevu;

(ii) Kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya hifadhi kwa kushirikiana na jamii ili kudhibiti uvuvi haramu;

(iii) Kufanya utafiti juu ya kina cha maji na kuwepo kwa samaki katika maeneo ya maji ya ndani;

(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumbawe yaliyowekwa Chwaka na Marumbi;

(v) Kuongeza matumbawe ya kienyeji katika maeneo mapya ya hifadhi ili kuongeza mazalio na mafichio ya samaki;

(vi) Kusimamia maeneo yaliyopo pamoja na kuanzisha maeneo mapya ya hifadhi baada ya kuthibitishwa katika Kanuni za *MCU*; na

(vii) Kuainisha maeneo maalum yenye umuhimu kwa uhifadhi wa rasilimali za bahari.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 30,000,000/= kutokana na mapato ya leseni za vyombo na za wavuvi. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya 2014/2015, Idara inaombewa kuidhinishiwa jumla ya shilingi 504,984,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 395,484,000 ni kwa mishahara na shilingi 109,500,000 ni kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 4).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itasimamia utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza Uvuvi wa Kina Kirefu cha Maji ambao unajumuisha pia mradi wa kujenga diko na soko la samaki Malindi unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japani *(JICA).* Mradi huu unaombewa jumla ya shilingi 6,261,600,000. Kati ya fedha hizo shilingi 261,600,000 ni kutoka Serikalini na shilingi 6,000,000,000 kutoka kwa Mshirika wa Maendeleo - *JICA*. **(Kiambatisho Nam. 5 na 13).**

IDARA YA MAZAO YA BAHARINI

Mhe. Spika, Idara ya Mazao ya Baharini ina majukumu ya kuwahudumia wafugaji wa mazao ya baharini, wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine tofauti wanaojishughulisha na mazao ya baharini kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi na kuinua pato la Taifa. Idara pia ina jukumu la kuendeleza, kudhibiti na kufuatilia shughuli zote za ufugaji na ukulima wa mazao ya baharini kwa madhumuni ya kuwa na usimamizi bora, pamoja na kuimarisha ubora na thamani ya mazao ya baharini.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mazao ya Baharini ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na mazao mengine ya baharini;

(ii) Kuendelea na utoaji wa elimu kwa wakulima wa mwani juu ya ukulima bora wa mwani, uhifadhi na kuhamasisha matumizi ya mwani na bidhaa zitokanazo na zao la mwani kwa maslahi ya akina mama na vikundi vinavyozalisha mwani; na

(iii) Kuwahamasisha wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kujiunga na vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa ili kujipatia mitaji ambayo itawawezesha kuanzisha vyanzo vya ziada vya kujiongezea kipato.

Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mazao ya Baharini ilitekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Katika kuimarisha ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na mazao mengine ya baharini, Idara imeanza ujenzi wa bwawa la mfano huko Donge Mchangani, imeweza kusaidia vikundi vya ufugaji wa samaki mashine 5 za kuingizia na kutolea maji katika mabwawa ya samaki kwa vikundi vitano vya ufugaji samaki kisiwani Pemba. Jumla ya vifaranga 20,546 vya samaki vimetolewa kwa wafugaji ambapo vifaranga 19,750 vimetolewa Pemba na 796 Unguja kwa lengo la kusaidia kuinua uzalishaji wa samaki na kuwaongezea kipato wafugaji. Aidha, imeweza kutoa taaluma juu ya ufugaji bora na endelevu wa viumbe vya baharini wenye kuzingatia athari za kimazingira ambapo jumla ya vikundi 107 vimefaidika na taaluma hiyo Unguja na Pemba;

(ii) Katika kuendeleza na utoaji wa elimu kwa wakulima wa mwani juu ya ukulima bora wa mwani, jumla ya wakulima wa mwani wa vijiji 53 Unguja na Pemba wamepatiwa taaluma ya mbinu bora za kilimo cha mwani pamoja na uhifadhi wa mwani wakati wa kuuanika na kuongeza ubora na thamani ya zao hilo. Aidha, vijiji 10 vya Unguja vinavyojishughulisha na kilimo cha mwani vimesaidiwa boti 50 na kwa upande wa Pemba jumla ya vijiji 17 vimesaidiwa vifaa vya kulimia mwani beli 100 za kamba na tai tai beli 260; na

(iii) Wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini wameendelea kuhamasishwa kujiunga na vikundi vya ushirika vya kuweka nakukopa ili kujipatia mitaji ambayo itawawezesha kuanzisha vyanzo vya ziada vya kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini nje ya Zanzibar yalikadiriwa kuwa shilingi 70,000,000 kwa Unguja. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, jumla ya shilingi 52,233,150 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 75 ya lengo. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mazao ya Baharini Unguja iliidhinishiwa jumla ya shilingi 198,745,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 112,405,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 86,340,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 jumla ya shilingi 109,046,650 zimepatikana kwa mishahara na shilingi 25,700,000 zimepatikana kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 30. **(Kiambatisho Nam. 1).**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mazao ya Baharini imetekeleza mradi mmoja wa kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini ambao uliombewa shilingi 100,000,000 kutoka SMZ na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 mradi huu haukuingiziwa fedha. **(Kiambatisho Nam. 3 na 14).**

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Mazao ya Baharini imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendeleza ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na mazao mengine ya baharini, pamoja na samaki wa maji baridi;

(ii) Kuendeleza utoaji wa elimu kwa wakulima wa mwani juu ya ukulima bora wa mwani, uhifadhikuhamasisha matumizi ya mwani na bidhaa zitokanazo na zao la mwani kwa maslahi ya wakulima wa mwani na Taifa kwa jumla; na

(iii) Kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kukuza na kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo kuwekeza katika ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 70,000,000 kutokana na mazao ya baharini. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya shilingi 203,301,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizi, shilingi 155,136,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 48,165,000 ni kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 4).**
Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itasimamia utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Ufugaji wa Samaki ambao unaombewa jumla ya shilingi 561,080,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi huu. Kati ya fedha hizo shilingi 176,400,000 zinaombwa kutoka Serikalini na shilingi 384,680,000 kutoka kwa Mshirika wa Maendeleo *(FAO).* **(Kiambatisho Nam. 5 &14).**

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Pemba, ina jukumu la kusimamia na kuwaongoza waratibu wa Idara mbali mbali za Wizara ya Mifugo na Uvuvi waliopo Pemba. Utekelezaji wa malengo hayo ni kama vile ilivyokwisha elezwa chini ya Idara zote zilizomo katika Wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba ililenga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 45,000,000, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya shilingi 15,724,825 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 35 ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi Kuu Pemba inakadiria kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 45,000,000. Mapato haya yanatokana na huduma za utabibu wa mifugo shilingi 12,000,000, huduma za uzalishaji mifugo shilingi 6,000,000, leseni za uvuvi shilingi 6,000,000 na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini shilingi 21,000,000. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba iliombewa jumla ya shilingi 953,700,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizi, shilingi 527,000,000 ni mishahara na shilingi 426,700,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 shilingi 474,093,650 zimepatikana kwa mishahara na shilingi 123,000,000 zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 29. **(Kiambatisho Nam. 1).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi Kuu Pemba inaombewa kutumia jumla ya shilingi 1,023,585,000 kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika Idara mbali mbali. Kati ya fedha hizi, shilingi 732,300,000 ni kwa mishahara na shilingi 291,285,000 ni kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa matumizi mengineyo, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa kutumia shilingi 30,000,000, Idara ya Uendeshaji na Utumishi shilingi 59,700,000, Idara ya Mazao ya Baharini shilingi 40,425,000, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi shilingi 46,500,000 Idara

ya Uzalishaji wa Mifugo shilingi 63,960,000 na Idara ya Utabibu wa Mifugo shilingi 50,700,000. **(Kiambatisho Nam. 4).**

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2013/2014

Ukusanyaji wa Mapato 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya shilingi 613,000,000. Kati ya mapato hayo, shilingi 400,000,000 zitatokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na shilingi 213,000,000 zitatokana na mapato ya ndani ya Wizara (ikiwemo ada za leseni za uvuvi wa ndani, utibabu wa wanyama na ada ya mazao ya baharini). Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 Wizara ilikusanya mapato ya shilingi 252,504,928, sawa na asilimia 63 kutokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na shilingi 123,731,675 sawa na asilimia 58 kutokana na makusanyo ya ndani. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Matumizi ya Fedha 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,678,600,000 ambapo shilingi 3,611,000,000 zilikuwa ni kwa kazi za kawaida na shilingi 1,067,600,000 ni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kawaida shilingi 2,326,000,000 zilitengwa kwa mishahara na shilingi 1,285,000,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara ni shilingi 2,045,774,050 sawa na asilimia 88. Kwa upande wa matumizi mengineyo fedha zilizopatikana ni shilingi 463,918,000 sawa na asilimia 36 ya makadirio. **(Kiambatisho Nam. 1).**

Mhe. Spika, kwa kazi za maendeleo, jumla ya shilingi 630,000,000 ziliombwa Serikalini na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 shilingi 226,000,000 zilipatikana sawa na asilimia 36. Aidha, jumla ya shilingi 437,600,000 ziliombwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kutekeleza miradi miwili ya maendeleo (Kuimarisha Ufugaji wa Samaki na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa) ambapo hadi Machi, 2014 jumla ya shilingi 91,600,000 zilipatikana sawa na asilimia 21. **(Kiambatisho Nam. 3).**

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 613,000,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. **(Kiambatisho Nam. 9).**

Mhe. Spika, vile vile, Wizara yangu inatarajia kutumia jumla ya shilingi 4,250,500,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 3,103,300,000 ni kwa mishahara na shilingi 1,147,200,000 ni kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 4).**

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya shilingi 7,340,553,000 zimetengwa ambapo shilingi 6,640,553,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kutekeleza miradi mitatu (Mradi wa Kichaa cha Mbwa, Mradi wa Kushajihisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Mradi wa Kuendeleza Uvuvi wa Kina Kirefu cha Maji). Na shilingi 700,000,000 **(Kiambatisho Nam. 5),** ni kutoka Serikalini kutekeleza miradi sita ya maendeleo (Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo, Kudhibiti Maradhi ya Mafua ya Ndege na Maradhi Yasiyokuwa na Mipaka, Kudhibiti Kichaa cha Mbwa, Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano, Kuimarisha Ufugaji wa Samaki na Kuendeleza Uvuvi wa Kina Kirefu cha Maji).

HITIMISHO

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuzishukuru taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Serikali ya Japan, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Serikali ya Uingereza kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Aidha, napenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo yakiwemo *KOICA, SADC, UNICEF, WHO, WSPA, USAID,* Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika *(AU),* Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO),* Shirika la Kimataifa la Mpango wa Maendeleo

(UNDP), Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*, Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo *(IFAD)*, Jumuia ya Afrika Mashariki *(EAC)*, na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* kwa kusaidia maendeleo ya sekta za uvuvi na mifugo.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kuzishukuru taasisi binafsi hapa nchini, Wizara za SMZ, taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kama Taasisi ya Sayansi ya Baharini, *COSTECH, State Oceanic Administration (SOA)* ya China, *Indian Ocean Marine Affairs Society, ZAASO, ZSPA* na *WIOMSA* ambazo zimesaidia katika kuleta ufanisi na maendeleo katika sekta za uvuvi na mifugo.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza viongozi wa Wizara yangu wakiwemo Naibu Waziri Mhe. Mohammed Said Mohammed, Katibu Mkuu wa Wizara Dk. Kassim Gharib Juma, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Omar Ali Amir, Afisa Mdhamini Pemba Ndg. Mayasa Hamad Ali, Wakurugenzi, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walioko Unguja na Pemba kwa utendaji mzuri na kufanyakazi vizuri katika mazingira magumu. Aidha, napenda kuwapongeza wafugaji, wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wa mwani, na wadau wengine wa sekta ya mifugo na uvuvi kwa jitihada na mashirikiano yao wanayotoa katika kuendeleza sekta hizi pamoja na changamoto zinazowakabili. Napenda kuwahakikishia kwamba mchango wao tunauthamini sana na tutaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yanayojitokeza kulingana na vipaumbele na nyenzo zilizopo ili kuzidi kunufaika na rasilimali hizi.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii adhimu kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Vile vile, tunawashukuru wananchi wote kwa kuitikia wito wa kutumia mazao ya mifugo na uvuvi katika milo yao na tunazidi kuwashajihisha wale bidhaa za ndani ili kuwainua wazalishaji wetu kimapato na kuimarisha afya zao.

Mhe. Spika, naomba kumshukuru Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa miongozo mizuri waliyotupa katika kufanikisha malengo yetu tuliyojiwekea katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya nchi yetu. Miongozo tunayoipata imeweza kutatua changamoto nyingi zinazokabili maendeleo ya sekta hizi**.**

Mhe. Spika, mwisho nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili na kuikubali bajeti ya Wizara yangu. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, waendelee kutupa maoni, ushauri na mapendekezo yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa, naliomba Baraza lako tukufu lipitishe jumla ya shilingi 11,591,053,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015. Kati ya fedha hizo shilingi 4,250,500,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 7,340,553,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa neema na rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema na hatimaye kutuwezesha kumudu kukutana hapa leo ili kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, pia, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao mkubwa walioonesha wakati wote ambao Kamati yetu inafanya kazi za ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuhihoji serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji kwa serikali.

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Mohammed Ali	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5. Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
6. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
7. Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Mjumbe
8. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamadali	-	Mjumbe
9. Ndg. Himid Haji Choko	-	Katibu
10.Ndg. Rabia Juma Shaaban	-	Katibu

Mhe. Spika, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata fursa ya kulifikiria kwa kulifanyia uchambuzi wa kina fungu la makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama ambavyo imeelezwa katika Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2012.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo, nachukua nafasi hii kukutaarifu kuwa kazi hiyo tuliifanya na leo hii tupo hapa kukuwasilishia taarifa ya kazi tuliyofanya kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 93(9) ya Kanuni hii ya Baraza la Wawakilishi ambalo toleo lake la mwaka 2012.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo napenda sasa ninatoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tunapenda kuipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kuweka wizara inayoshughulikia masuala ya uvuvi na mifugo ambayo ndio njia kuu ya ajira kwa wananchi wetu. Tegemeo letu ni kuwa serikali iliona umuhimu mkubwa wa kuwepo wizara hii. Pamoja na nia hiyo njema ya serikali, Kamati yangu inaendelea kusononeshwa sana kuona kuwa wizara hii imekuwa kama Idara kutokana na kuekewa kasma ndogo inashangaza sana kiasi kwamba umuhimu ule wa mwanzo wa kuunda wizara hii haupo tena. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Kamati inaiomba serikali kuongeza fungu la wizara hii ili iweze kuwahudumia vyema na ipasavyo wavuvi na wafugaji wetu. Suala ambalo likifanikiwa litaweza kupunguza tatizo la ajira linalowakabili vijana wetu.

Mhe. Spika, karibu taasisi zote za wizara hii ambazo zinahusika na ukusanyaji wa mapato, makisio yao ya mwaka huu hayana tofauti na yale mwaka jana. Kamati inajiuliza, kwa nini kusiwe na ongezeko la mapato wakati ufanisi wa utendaji unaongezeka mwaka hadi mwaka. Ni vyema basi wizara ikaziimarisha vianzio vyake vya mapato ili makusanyo yaongezeke na hatimaye yaweze kusaidia uendeshaji wa taaasisi za wizara hiyo na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha unaomalizika, pamoja na mipango mengine ilikusudia kutayarisha sera ya uvuvi na mazao ya baharini. Lakini kazi hii haikufanyika kwa madai ya kukosa nyenzo ambapo Kamati imeelezwa kwamba kazi hii inatarajiwa kutekelezwa katika mradi wa *SMART FISH.* Kamati hairidhishwi kuona mipango kama hii inashindwa kutekelezwa kwa kukosa nyenzo. Hali hii inaonesha kuwa katika serikali yetu tunakuwa wazuri wa kupanga, lakini tunakosa umakini wa kutosha wa utekelezaji wa mipango yetu.

Mhe. Spika, Kamati pia inasikitishwa sana na mapungufu makubwa ya watalaamu katika nyanja za utafiti, takwimu, elimu ya kuendesha uvuvi endelevu, pamoja na madaktari wa mifugo. Hali hii inasikitisha sana kwa wizara kama hii inayotegemewa sana na wananchi na inachangia kurejesha nyuma juhudi za wafugaji na wavuvi. Tunaishauri wizara hii kuwaajiri wataalamu wengi zaidi katika fani hizo ili waweze kuwasaidia wafugaji na wavuvi na hatimaye waweze kukuza vipato vyao.

Aidha, Kamati inaitaka wizara kuongeza idadi ya wafugaji wanaowapatia mafunzo ya kuhifadhi malisho na umuhimu wake, kwani idadi ya wafugaji 20 waliopatiwa mafunzo mwaka huu ni ndogo sana. Aidha, ziara tatu za mafunzo ya kutembeleana baina ya wafugaji wa Kisiwa cha Pemba nazo ni kidogo sana. Tunaitaka wizara ifanye juhudi za makusudi ili iongeze fursa zaidi za mafunzo kwa wafugaji na wavuji wetu.

Mhe. Spika, Kamati imefurahishwa na malengo ya wizara ya kutaka kuongeza nafasi za uzalishaji za ajira 120 kwa vijana kupitia mradi wa kuendeleza wafugaji wadogo wadogo. Wafugaji wetu hasa wale waliopata mafunzo wanajitahidi sana kuendelea na shughuli za uzalishaji. Wafugaji hawa hasa wale wa kuku kuwa wanapata vifaranga vingi, lakini vifaranga hivyo baada ya muda hushambuliwa na ndui na mahepe. Kamati inaishauri wizara kuandaa mpango maalum utakaowezesha kujikinga na magonjwa hayo ili wafugaji wetu waweze kupata matunda mazuri ya mifugo yao.

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ina majukumu makubwa ya kuendeleza uvuvi na uhifadhi wa viumbe pamoja na mazingira ya bahari. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii imeombewa shilingi milioni mia tano na nne, laki tisa thamanini nne elfu. Kwa kweli fedha hizi ni kidogo mno ukilinganisha na majukumu ya idara hii. Tunaishauri serikali kuongeza bajeti kwa Idara hii ili malengo yake yaweze kufikiwa hasa ya kutoa elimu kwa wavuvi inayohusiana na utunzaji wa mazingira ya bahari, pamoja na mazao ya samaki na hata matumizi mazuri ya mitego inayotumiwa na wavuvi. Suala la utoaji wa elimu muhimu sana, kwani litasaidia kuwaelimisha wavuvi na wafugaji kufahamu nia nzuri ya serikali ya kutaka wafanye shughuli zao kwa mazingira mazuri na yenye tija.

Mhe. Spika, makadirio ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, serikali ilikusudia kuingia uvuvi wa kina kirefu cha maji ambapo ilitenga shilingi milioni mia tano kwa lengo la kununulia meli pamoja na kutoa mafunzo kwa wavuvi watakaotumia meli hizo. Hadi hivi sasa meli hiyo haijanunuliwa kwa vile gharama za ununuzi na uendeshaji wa meli hiyo zimekuwa kubwa zaidi. Kamati inashauri kwamba uamuzi wa kununua hiyo meli uangaliwe upya huku wataalamu wa Idara ya Uvuvi wakishirikishwa kikamilifu katika kuupitia upya mradi huo. Kamati inaamini kwamba huenda faida inayokusudiwa ikakosekana kutokana na kwamba mradi huu haukufanyiwa utafiti wa kina na wataalamu wahusika.

Mhe. Spika, Kamati inatoa angalizo hili ili serikali isije ikaingia katika hali ngumu na gharama kubwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo na lengo lililokusudiwa likashindwa kufikiwa. Hata hivyo, hali hii haimaanishi kuwa serikali iishie, hivi sasa kuna haja ya kufanya kila namna ya kuhakikisha kwamba tunaingia katika uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, miongoni mwa miradi ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ni pamoja na ujenzi wa soko la Malindi. Tunaiomba serikali kutoa sehemu ya mchango wake katika ujenzi huo na kwa wakati ili kuunganisha na nguvu za Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa, Kamati inaamini kwamba kujengwa kwa soko hilo kutasaidia sana wavuvi wetu kuwa na sehemu ya uhakika wa kuuza zao zikiwa katika hali nzuri ya usafi na mazingira mazuri ya kibiashara.

Mhe. Spika, aidha, kukamilika kwa soko hilo kutaongeza ajira kwa wananchi wetu ambao watakuwa na biashara mbali mbali katika sehemu hiyo ambapo pia Idara na serikali kwa ujumla inaweza kujiongezea mapato kwa kodi mbali mbali zitakazotozwa sokoni hapo. Kamati pia inaamini kwamba kukamilika kwa soko hili, pia kutapunguza mzigo kwa soko kongwe la Darajani ambapo kwa hakika inaonekana kwamba sehemu ya kuuzia samaki mazingira yake sio mazuri sana kwa wakati wa sasa.

Mhe. Spika, wakati wa kazi za kawaida za Kamati, Kamati yangu ilibahatika kutembelea kisiwa cha Chumbe ambacho kilikodishwa kwa mwekezaji ambaye anaendelea na shughuli za uhifadhi wa bahari na maeneo ya juu ya kisiwa hicho. Kamati inapongeza juhudi za uhifadhi zinazoendelea katika sehemu hiyo ambayo sasa imekuwa mfano mzuri na matunda yake yanaonekana. Hasa kwa upande wa uhifadhi wa matumbawe na sehemu hiyo, hivi sasa imekuwa na mazalio makubwa ya samaki. Hata hivyo, kumekuwa na ripoti zisizoridhisha katika eneo hilo, pamoja na sehemu nyengine ambapo bahari imekuwa ikiongezeka kwa kasi kuvamia ardhi. Suala ambalo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabia ya nchi duniani.

Mhe. Spika, tunaiomba serikali kuwa makini na jambo hili na kuchukua kila tahadhari ya kujikinga na janga hilo. Kwani ingawa hakuna tafiti za kisayansi kuhusiana na hili, lakini tumekuwa tukishuhudia kwa macho yetu sehemu nyingi za asili ambazo zilikuwa nchi kavu na hivi sasa tayari zimeshavamiwa na maji ya bahari hiyo.

Mhe. Spika, imearifiwa kwamba kila inapofika wakati wa pepo za kusi, wafanyakazi wa sehemu hiyo ya Kisiwa cha Chumbe wamekuwa wakishuhudia taka taka nyingi zinazotokana na shughuli za kihospitali, hasa mabomba ya sindano na sindano zenyewe pamoja na taka nyengine. Jambo hili linatia wasi wasi. Hivyo, si vyema kwa wahusika

kuacha taka taka za Hospitali kuzagaa baharini ama mitaani au sehemu nyengine yoyote, kwani huenda zikachangia kuoneza maradhi mbali mbali.

Mhe. Spika, kuhusu mradi wa majaribio ya matumbawe ya kienyeji katika maeneo ya Chwaka na Marumbi. Kamati imefurahishwa sana na mafanikio yaliyopatikana katika mradi huo. Kwani kuna taarifa kwamba samaki wameongezeka sana hasa katika maeneo ya Marumbi na wavuvi katika sehemu hiyo wamekuwa wakishuhudia samaki wengi katika eneo hilo.Tunaomba mpango huu wa matumbawe ya kienyeji upelekwe pia katika maeneo mbali mbali hapa nchini ili wavuvi wa sehemu zote waweze kufaidika na mradi huu.

Mhe. Spika, wakati Kamati yangu inatembelea Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Fumba iligundua kwamba mapato ya mamlaka hayo yanaongezeka hasa kutokana na mwamko wa wavuvi wa ndani na wa nje ya nchi kwa kukata leseni za uvuvi huo. Kwa taarifa tulizozipata ni kwamba hali hii inachangiwa na doria za mara kwa mara za majini pamoja na taaluma inayotolewa juu ya umuhimu wa kukata leseni za uvuvi huo. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na makadirio ya mapato ya shilingi milioni mia nne ambayo ni sawa na makisio ya mwaka jana, wakati mapato yanayokusanywa na mamlaka hiyo yamepanda sana mwaka huu.

Afisi Kuu Pemba:

Mhe. Spika, Kamati yangu haikufurahishwa hata kidogo wakati inapitia bajeti ya wizara hii ambapo hapakuwa na mtendaji yeyote katikia Afisi Kuu ya Pemba. Kamati inashauri wizara kuwashirikisha kikamilifu watendaji kutoka Afisi ya Pemba hasa kunapokuwa na jambo kubwa kama hili la bajeti ambapo mara nyengine Kamati huwa inapendelea kupata ufafanuzi wa moja kwa moja kutoka kwa wahusika wenyewe.

Mhe. Spika, napenda sasa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu. Pia, napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wanawake wote ninaunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Aidha, nawaomba Wajumbe wote wachangie na kuunga mkono makadirio ya bajeti ya wizara hii kwa ajili ya utekekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Sasa ni zamu ya uchangiaji wa jumla, nafasi ya kwanza naomba nimkaribishe Mhe. Ali Salum Haji, baadae Mhe. Asaa Othman Hamad, wakati Mhe. Hassan Hamad Omar anajitayarisha.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante kunipa fursa hii adhimu, nakushukuru kwa dhati kwa kuweza kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa siku hii ya leo katika bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, kwanza nataka nichangie kwenye kitabu hichi cha makadirio ya mapato na nataka nichangie katika ukurasa wa 115. Kabla ya sijatoa mchango wowote niishukuru tu wizara, kwa sababu katika yale mambo mengi ambayo huwa tunapigia kelele kwamba mafungu yamekuwa yamenona, mafungu ambayo huwa hayaleti tija zaidi kuliko tija za wananchi. Wizara hii kidogo wamejitahidi vya kutosha na niwape pole kwa sababu kila pahala unakuta kumepunguzwa kupita kiasi, lakini kuna maeneo kama mawili au matatu. Nataka nipate ufafanuzi, kwa sababu bado naona hayajaniridhisha. Mhe. Waziri, atakapokuja atanieleza sababu za msingi za maongezeko.

Mhe. Spika, moja ya eneo katika ukurasa wa 115, kuhusu gharama za mafuta na vilainisho, katika kifungu 220400. Nimepata mshtuko baada ya kuona ongezeko kubwa la gharama za *petrol*, fungu dogo 220401. Mwaka jana ilikuwa shilingi 660,000 na mwaka huu limetengewa milioni 3,381,000, Mhe. Waziri, atakapokuja atanisaidia sababu za msingi za kuongezeka mara dufu ni zaidi ya mara 5 ya bajeti ya mwaka jana.

Mhe. Spika, eneo jengine ni katika ukurasa wa 116, kuhusu ununuzi wa mashine, kwenye fungu 220900, fungu dogo 221100 kuhusu gharama za mafunzo *capacity building*. Hapa katika mafunzo ya ndani *Local training* kumetengwa milioni 14,820,000. Nataka Mhe. Waziri, atakapokuja anisaidie ni mafunzo ya aina gani yaliyotengewa

pesa hizo, lakini kinachonishangaza katika mafunzo hayo, kwenye kifungu kidogo cha 221199, vifaa vya mafunzo hapajatengwa pesa. Sasa napata mashaka, pesa nyingi zimetengwa za mafunzo ya ndani, lakini hakuna vifaa ambavyo vimetengewa mafunzo, nataka kujua mafunzo haya yatafanyika kwa namna gani.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuchangia ni kwenye ukurasa wa 120, kuhusu gharama za mafuta na vilainisho, kifungu cha 220401, gharama za *petrol*, mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 22,142,000, mwaka huu ni milioni 38,911,000 na *petrol* mwaka jana ilikuwa milioni 10,125,000 na mwaka huu ni karibuni milioni 22,540,000, Mhe. Waziri, atakuja kunisaidia sababu za ongezeko la karibuni mara mbili ya gharama za *petrol* kama wamenunua magari ya ziada au kitu gani, basi atakuja kunisaidia.

Mhe. Spika, vile vile, katika fungu hilo la *petrol* katika ukurasa wa 133, sasa napata mashaka kila kwenye *petrol* gharama zimezidi, sijajua kama kila Idara imeongeza magari. Katika ukurasa wa 133, gharama za mafuta na vilainisho, kifungu cha 220400, fungu dogo la 220402, gharama za *diesel* mwaka jana ilikuwa milioni 15,555,000 na mwaka huu ni milioni 28. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, atakapokuja atanisaidia katika hivi vifungu namna ya ongezeko lililoongezeka, pamoja na kwamba nimewapa pongezi kwa mafungu mengi na hususan mafungu ya vilainisho, vitafunio na vinywaji, kwamba wenzetu hawa wamejitahidi kuweza kupunguza hii bajeti yao na kuweza kuwapa pole kwa namna ambavyo pajeti wataifanya.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kitabu. nataka nije kwenye sekta ya uvuvi katika kitabu chake Mhe.Waziri, amesema kwamba ameweza kuvua tani 41,952, ambao wameweza kukusanya bilioni 153,460,624,506. Sasa mimi nilikuwa nataka maelezo hizi tani za uvuvi ambazo zimeelezwa hapa katika hiki kitabu ni uvuvi wetu wa ndani wa kawaida au ni uvuvi wa nje wa zile meli ambazo zinavua bahari kuu. Suala hili nataka Mhe. Waziri, atakapokuja anisaidie. Kama utakuwa ni uvuvi wa ndani nataka kujua vigezo vya kuweza kuzijua hizi tani, kwa sababu mara nyingi mimi napata mashaka, kwa sababu wenzetu wa uvuvi pamoja na watu wa kilimo, wanakutajia tani za uzalishaji, lakini hukuti kituo ambacho kinapima huo uzito wa hao wavuvi.

Mhe. Spika, sasa najiuliza hayo makisio wanayapataje na uvuvi wetu wa Kizanzibari mtu anavua na mashua yake anakwenda baharini, watu wanakwenda kuuza. Kwa hivyo, atakapokuja Mhe. Waziri, atanieleza. Kwanza nilitaka kujua ni uvuvi wa ndani wa wavuvi wetu wa kawaida au ni uvuvi wa nje. Kama ni uvuvi wa ndani vigezo vile ambavyo wamevitumia ili kuweza kujua hizi ni tani 41,952.

Mhe. Spika, katika sekta hiyo hiyo ya uvuvi, mimi nataka Mhe. Waziri, aje anipe taarifa za hivi karibuni tulipata kusikia kadhia ya wavuvi wa Kaskazini, kama sikosei ilikuwa Tumbatu na watu wa Mkwajuni na walifikia pahala watu wale kuanza kuchomeana madau katika pande zile mbili. Nilitaka kujua ni nini kiini cha mgogoro ule na kama wizara wamejiandaa vipi ili kuweza kutatua mgogoro ule. Ilikuwa ni mazoea na tulikuwa tumeshazoea kusikia kwamba migogoro kama ile kwa muda mrefu ilikuwa iko katika maeneo baina ya huba ya Chwaka na Uroa.

Mhe. Spika, nashukuru safari hii kwenye kitabu sikuliona hilo, sijui wenzetu walipata njia gani za mafanikio kuweza kuondosha migogoro ile na ikaweza kuondoka kutoka Wilaya ya Kati na kurukia katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, atakapokuja anieleze sababu za msingi na hatua, pamoja na wale ambao walihusika katika kuhujumiana hujuma zile, hatua za kisheria zimefikia hatua gani.

Mhe. Spika, jengine nilitaka kuzungumzia, pamoja na kwamba hata taarifa ya Mwenyekiti nilipokuwa nikisikiliza hapa, nilimsikia anavyozungumzia na hata kitabu kimeelezea juu ya namna ya ununuaji wa boti za kisasa katika kuvua bahari kuu. Hili wazo ni zuri na vijana wetu wameanza kupata matumaini, kwamba kutokana na ukwasi wa ajira Zanzibar, labda tungefikia pahala katika ununuzi wa boti hizi tungeweza kupunguza hizi vuguvugu za ajira.

Mhe. Spika, mwaka juzi ilipokuja bajeti hii kulikuwa kuna makisio ya milioni 400, tukapata taarifa kuwa pesa zile hazikuwa za kutosha. Hivyo, boti imeshindikana kununuliwa. Sasa mimi nataka kujua tu ile hatua iliyofikiwa, maana suala lililozungumzwa kuhusu boti za kisasa kwenda kuvua bahari kuu, imekuwa ni *story* baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha. Sasa ni suala ambalo linatupa tabu, hatujui tatizo liko wapi? Utakuja kusikia watu tayari wamekwisha kwenda kuangalia aina ya boti, lakini ukirudi huku, utaambiwa boti haikupatikana. Sasa hiki kitu kinatupa mashaka kabisa, hatujui tatizo liko wapi na hatujui nini kifanyike.

Mhe. Spika, pamoja na hilo, kwa sababu naona kwamba hata wizara yenyewe imeshaanza kuonesha jitihada ya kufundisha karibuni vijana 13, lakini unabaki kujiuliza kusomesha ni suala moja, lakini baada ya kusomesha

unaowasomesha wanahitaji ajira, sasa ikiwa huku sisi tunasomesha, halafu watu wanabakia na vyeti vyao majumbani, sioni kama suala hili litakuwa ni jema na ambalo litaweza kuisaidia wizara. Kwa hivyo, nataka kujua kwamba maendeleo ya ununuzi wa boti zile umefikia wapi, ili wale ambao tumewasomesha, basi tuweze kuwasaidia kuweza kuwapa ajira.

Mhe. Spika, jengine nilitaka nizungumzie katika kitabu chake Mhe. Waziri, katika ukurasa wa 8, amezungumzia masuala ya changamoto ya wizara. Moja ya changamoto iliyozungumzwa ni suala la bei ndogo ya zao la mwani. Unaweza kufikia pahala ukawa unachoka kusikia baadhi ya maneno, maana yake unapokuwa na changamoto, maana yake zinahitaji kupata ufumbuzi. Sasa ikiwa miaka nenda miaka rudi, kila kitabu kikija changamoto ya bei ya zao la mwani. Mwakajuzi changamoto hiyo ya bei ya zao la mwani, mwaka jana pia na mwaka huu zimo. Nilitaka kujua wizara inajipanga vipi?

Mhe. Spika, wananchi wetu katika kanda za bahari wanateseka kwa kuutumia muda mwingi kuweza kufanya mahitaji ya ulimaji wa mwani, lakini baada ya kulima wanachokipata kinakuwa ni kidogo. Kwa hivyo, tatizo linakuwa kwamba hali ya umaskini katika ukanda wa pwani, ndio linawapelekea watu walime mwani, lakini hali ile ile haiwafanyi wananchi kujikomboa kutokana na suala la ulimaji wa mwani. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, aje atusaidie ni mbinu gani ambazo umeanza kuzitafuta ili kuweza kukabiliana na hii changamoto au bado itaendelea kwamba aaah! kila mwaka wizara ikija changamoto ni changamoto tu. Wananchi wanateseka na wanafikia pahala wanaanza kukata tamaa na hatujui mwisho wake watafaidika na nini katika suala hili.

Mhe. Spika, jambo jengine ninalotaka kulizungumzia ni suala la nyumba za wizara. Kwa bahati nzuri serikali yetu ilikuwa na nia njema ya kuona kwamba kila wizara na kila *department* wanawekewa makazi maalum ili kurahisisha utendaji wa kazi. Wataalamu mara nyingi walikuwa wanatumia nyumba zile kukaa ili wanapohitajika, basi iwe rahisi kuweza kutoa zile huduma.

Mhe. Spika, Maruhubi *opposite* na *go down* la mfanyabiashara ndugu yetu Ali Hilali, kuna nyumba za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na nyumba, pia pana eneo ambalo lilikuwa kubwa ambalo lilivamiwa kwa kipindi kirefu na watu kujenga nyumba zao katika hilo eneo la wizara, hadi kufikia wizara kuwa na ufinyu wa eneo.

Mhe. Spika, nataka kujua nyumba zile, wizara maana yake wamefikia hatua gani katika kuziendeleza na kuweza kuzitumia kwa mahitaji ya wizara. Cha kusikitisha kwamba nyumba zile sijui wenyewe wizara kama wanafahamu hilo. Zile nyumba zimeanza kutumika kwa mahitaji yasiyokuwa mazuri, mahitaji yasiyokuwa salama ya vitendo viovu kwa wananchi wa eneo lile. Nyumba zile zimekuwa ni madanguro, zimekuwa ni maeneo ya kuvutia bangi. Kwa hivyo, wizara watuambie ni nini azma ya kuziendeleza nyumba zile ili ziendane na malengo ya serikali katika kuzijenga kwenye eneo lile. Vyenginevyo, kama hili eneo hawalihitaji, basi mimi nahisi kuna haja watafute njia ya kuweza kulibinafsisha au kuweza kuliuza, ili serikali ipate chochote, kuliko kuweka magofu ambayo watu wanatumia kwa vitendo viovu katika eneo lile.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilitaka nichangie katika wizara hii, ni kwenye sekta ya bahari kuu. Mwaka jana nilipochangia hapa nilimsifu sana Mkurugenzi Mkuu wa Bahari Kuu, kwa namna alivyojitahidi katika kuisaidia ile sekta ya bahari kuu katika kila nyanja na kuona kwamba serikali yetu inafaidika vipi katika kuingiza mapato kwenye eneo la bahari kuu.

Mhe. Spika, katika michango yangu ya mwaka jana pamoja na jitihada za waziri, nilizungumzia sakata la vibali bandia ambavyo viligharimu karibuni bilioni 1.7. Nilimpongeza sana Mkurugenzi kwa jitihada ambazo amezichukua za kufichua sakata lile na leo bado naendelea kumpongeza sana Mkurugenzi yule, kwa namna alivyotumia jitihada ya kuhakikisha suala hili wanalifikisha katika sehemu husika.

Mhe.Spika, bado napata mashaka namna ya mwenendo wa suala hili katika kupatiwa ufumbuzi. Sasa hivi tuna mwaka mmoja, Mhe. Waziri, atakapokuja nataka anieleze hatua zilizofikiwa kwa suala zima la sakata la vibali bandia vya uvuvi wa bahari kuu na hatua ambazo zimechukuliwa mpaka sasa hivi na kama wizara imeshindwa, leo nazungumza kwenye chombo hiki kwa mara nyengine, naomba vitengo vinavyohusika ikiwemo Taasisi ya Kuzuia Rushwa, basi kulifuatilia suala hili na kulifanyia kazi ili kuweza kupambana na watu wasiyoitakia mema nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni la kumalizia kabisa katika uchangiaji wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie juu ya suala zima la ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Kisakasaka. Uchinjaji wa

ng'ombe umekuwa sio salama kwa kipindi kirefu, machinjio yetu yamekuwa hayako katika mazingira mazuri, lakini wizara ilionesha jitihada ya kujenga machinjio ya kisasa kule Kisakasaka kwa kufanya marekebisho ya lile chinjio letu. Sasa nataka Mhe. Waziri, atakapokuja anieleze hatua zilizofikiwa katika ujenzi ule na lini ujenzi ule utakamilika, ili tuweze kuchinja wanyama wetu katika hali ya usalama na ubora zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono hotuba hii na pamoja na kuunga mkono, basi nasubiri majibu ya kina, majibu yenye ufasaha kwa Mhe. Waziri. Nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Ali Salum Haji, tunakushukuru pia na kwa kuokoa muda. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Asaa Othman Hamad, baadae Mhe. Hassan Hamad Omar, nimuombe na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ajitayarishe.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika siku hii ni kiwa na afya njema. Niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kukupa wewe Mhe. Spika, afya njema kuendelea kutuongoza, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, ni nia njema kabisa ya Mhe. Rais wa Zanzibar, alipoiondoa iliyokuwa Idara ya mifugo kule kilimo na kuifanya ni wizara kamili ya mifugo na uvuvi. Hii ni namna ilivyoonekanwa kwamba ina mchango na inaweza ikatoa mchango mkubwa zaidi kwa pato la Taifa, lakini pia, kwa kipato cha mtu mmoja mmoja na familia. Dhana hii bahati mbaya imekubwa na mkosi, nia njema ile haisaidii sana ama hatua inayochukuliwa na serikali, ili wizara hii iweze kufanya vizuri zaidi kwa maslahi ya nchi hii na wananchi wake. Nasema hivi kwa sababu pesa inayotolewa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tunashuhudia namna ya malengo yanavyo-*fail* mwaka hadi mwaka.

Mhe. Spika, sekta ya mifugo, mifugo kutokana na *geographer* yetu hatuna eneo la kuendeleza ufugaji huu tuliozowea. Wenzetu hawa wanataka kusaidie jamii namna ya ufugaji bora wenye tija, lakini wanashindwa kufanya hivyo kutokana na fedha inayotolewa na serikali. Kwa hivyo, serikali ifike mahali ione nia ile njema ya kuitakia wizara hii ichangie, basi iendelezwe, kuiendeleza wizara hii, basi tutakuwa tunaijenga jamii ya Wazanzibari kuwa na afya bora, watakuwa na lishe nzuri, watakula kwa wale walaji wa nyama, watakunywa wale wanywaji wa maziwa na watauza, lakini mazao yale ya mifugo ni lazima tufike mahali sasa iongeze ajira, ni vipi ajira itaongezeka. Mazao ya mifugo ni lazima yaongezwe thamani, tutaongezaje thamani, ni viwanda.

Mhe. Spika, tunamaliza mwaka wa 9 sasa, tunaiambia serikali hii sikivu kwamba bila ya viwanda tutaendelea kudanganyana, vijana ni bomu kubwa, wanamaliza vyuo na sekondari hatuna vya kuwafanya. Kwa hivyo, ni lazima tufike mahali serikali ibuni haya mambo na haya mambo kwa pato linalokusanywa na serikali, tukisema tuweze kujenga viwanda hivyo vidogo vidogo na vile vya kati basi ni tatizo jengine. Labda nisaidie kwa kutoa rai, hebu tuwaite wenzetu wawekezaji, tena wawekezaji halisia sio wababaishaji.

Mhe. Spika, tatizo la ajira linakua siku hadi siku na ni kero kubwa tunajidanganya sasa hivi na hawa watalii, tunasema utalii, lakini mtizame mtalii anavyonyang'anyiwa na vijana mpaka inakuwa ni kero, ni kwa sababu vijana hawana ajira, lakini Mwenyezi Mungu amejaalia Zanzibar hii hali nzuri ya hewa pamoja na matatizo ya tabi ya nchi, tunayo bahari na bado tutaendelea kusema wengine kwamba mgodi mkubwa tulionao ni bahari. Sasa kushindwa kwetu kuitumia, hilo ni tatizo letu tujiulize wenyewe.

Mhe. Spika, sekta hii imeelemewa na changamoto kwa wafugaji na wajasiriamali wanakosa mitaji, taasisi zetu za fedha hadi leo bado hazijaweza kusaidia au kuchangia katika sekta hii. Vile vile, tunalo tatizo la wafugaji wenyewe la uhaba wa malisho, ndio lile ninalolisema, kwamba tunaongezeka kwa kasi kubwa, maana yake mahitaji nayo yanaongezeka kutokana na hilo ongezeko hilo la watu, lakini ardhi tuliyonayo inapungua siku hadi siku. Hivyo, wenzetu watusi na watuelewe. Kwa kweli mabadiliko haya ya tabia ya nchi ni tatizo kubwa hivi sasa la mazingira, ardhi hii inamong'onyoka na taarifa hapa zimesomwa namna gani bahari inavyovila visiwa hivi na vyengine vina hali mbaya sana.

Mhe. Spika, ufugaji huu lazima ubadilike na utabadilikaje? Ni wafugaji kupata taaluma ya kufuga namna ya ufugaji bora. Ufugaji bora faida zake ni kubwa tutakuwa na mifugo michache, lakini yenye tija kubwa, wafugaji watafaidika pamoja na Taifa kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, tutapunguza maradhi kwa sababu tutakuwa na lishe bora na kukosekana hayo, tutaendelea kurundikana Hospitali ya Mnazimmoja na sehemu nyengine na kwenyewe hakuna dawa na wala kilichopo ni mashaka matupu. Sasa ni vyema tuchangie huku, ili watu wapate afya njema kwa ajili ya kupunguza ule msongomano kule. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pato la wafugaji bado halijaridhisha, Sekta Binafsi lazima nayo ifike mahala iweze kuekeza na ione umuhimu wa ufugaji. Kwa kweli wapo wenzetu ambao wao uwezo na wanahitaji taaluma, kwa ajili ya kuekeza kwenye maeneo haya, lakini bado watu wetu hawa wanajua Dubai, China na kwengineko kule kwa sababu wanapata kipato cha haraka haraka na kipato hichi huku kwenye maeneo haya wao watapata, watu wetu ambao ni wananchi watapata pamoja na Taifa kwa jumla. Kwa hivyo, lazima kuwe na dhamira ya makusudi katika hili. Sekta ya Uvuvi inafanana na sekta ya mifugo, kwa mfano shughuli zimetajwa zimeongezeka za uvuvi na wavuvi pia wanaongezeka, lakini kinachovuliwa nacho kinaongezeka ndio swali hilo. Mtu wa kawaida mwenye kipato cha chini hawezi kula samaki kila siku hapa Unguja na Pemba, pamoja na bahari hii ambayo imetuzunguka, lakini imegeuka sasa ni joka la mdimu na wale wanaokuja kutuibia, ndio wanaofaidika kuliko sisi wenyewe, pamoja na yaliyotajwa hapa kwamba kuna doria ambazo zinafanywa za angani na baharini, lakini bado wizi ni mkubwa mno kuliko tunachokipata. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wavuvi wetu wanaongezeka, kwa sababu vijana kazi hawana na hasa ambao wanaoishi kando ya bahari na hao ni wimbi kubwa linakuja kuvamia mjini. Kwa bahati mbaya Waheshimiwa Mawaziri waliomo ni yule mwenye sekta hii hivi sasa na mwenziwe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na sijui haya tunayoyasema yatakwenda vipi serikalini.*(Makofi)*

Mhe. Spika, hali hii inaonesha udhaifu, kwa sababu sisi tupo hapa tunasema pamoja na kuishauri serikali, sasa masuala ya kifedha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais viti tunaviona vilivyo vyeupe na jambo hili tunalisema siku hadi siku, lakini ni kama vile ni kutwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ujumbe huu utafikaje na wewe siye wa kupeleka, ni vyema serikali iwepo hapa ndani na tunaposema isikie. Mhe. Waziri wa Fedha, yupo ameingia, lakini yaliyotangulia huku labda ataambiwa na wenziwe. Kwa hivyo, tunasema taasisi za fedha zilizopo nchini, serikali ifike mahala sasa zichangie kwenye masuala ya uvuvi na mifugo, ili wananchi wetu waweze kupata tija, uwezo walionao na hata ule wa serikali haukidhi kuleta maendeleo ya sekta hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu changamoto za uvuvi. Uvuvi unavamiwa kwenye maeneo yetu ya hifadhi ni kwa sababu huko wanakofika wao baharini hakuna kitu na hakuna kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa kweli tutajichanganya sana kama hatutaki ama tutakuwa wakaidi kufuatana na hali halisi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wakubwa Duniani hiyo Kioto wao hawana habari nayo. Sasa kwa sababu hatuna uwezo wa kulazimisha wakubali "isiyo nkame yajikamua wenyewe". Nadhani ni vyema tuwe na dhamira za makusudi kwa ajili ya kupambana na tatizo la tabia ya nchi pamoja na mazingira kwa ujumla wake, vyenginevyo, vitabu vyetu hivi vitaendelea kuandika na kuandika, lakini jibu haliji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Uvuvi haramu, hawa watu wataendelea kufanya mabaya haya, kwa sababu dhamira zile za makusudi serikali bado haijakuwa nazo, ili hawa watu waachane na mambo haya, kwa mfano kujenga Kamati za Wilaya, Majimbo, pamoja na mambo mengine hazitoi jibu, isipokuwa jibu wapatiwe vifaa hawa watu wavue na kuongezeka kwao pia hakujasaidia kwamba kutaongezeka pato. Kwa kweli uvuvi tunaoutaka kwa kujivunia na wala sio kwa Bandari ya Malindi inayojengwa, kwa sababu itajenga itabaki pale itafanya vumbi kama wavuvi wetu hawajavua Bahari Kuu wao kama wao na kwa kukaribisha wenyewe uwezo, ambapo ni Kampuni za Uvuvi duniani zipo na watu wetu watapata ajira na tutapata fedha za ndani na nje.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, akae na watu wake wa uchumi na kuratibu haya mambo, ni vipi tutaondokana na umasikini huu uliokithiri na Mwenyezi Mungu alichotujaalia sisi ni bahari na wala hatuna pengine, kwa maana ya bahari tutambae ndani ya maji, twende chini ya maji, yaani twende chini ya ardhi ya bahari na kila kitu kipo, nawaomba wafanye hilo. Sasa tutaendelea kulalamika na kulalamika na hichi tulichopewa tunakifanyia nini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwenye suala la utumishi. Kuna Idara ya Utumishi ya Wizara hii, kitabu pamoja na mambo mengine anasema;

"… ni kusimamia kupatikana kwa haki za wafanyakazi na wafanyakazi wenyewe wawajibike".

Mhe. Spika, wafanyakazi kutokana na mabadiliko ya *Science and Technology* wanahitaji kupata mafunzo, masomo ya muda mrefu, muda wa kati, muda mfupi pamoja na matembezi kimasomo. Hivyo, *privileges* kama hizo zinawasaidia, lakini mafanikio yaliyotajwa kwenye kitabu hichi ni wao wafanyakazi wanaofanyakazi hizo katika mazingira magumu mno.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye ni ndugu yangu, zinapotokea zile nafasi za kutoka nje ya nchi na wao kwao ndio nafasi yao ya kujisikia, watizameni kwa jicho la huruma na maposho musikusanye nyiye wakubwa tu munapotoka na wao wanayahitaji. Wao ni wakubwa wanazo nafasi kubwa kubwa pamoja na maeneo mengi, kwa nini muwanyie viposho hivi vya kwenda China, Japan na sehemu nyengine, anaambiwa mtu kama anataka kwenda, panda ndege utakula na utalala, mbona yeye hataki kufanya hivyo na anachukua maposho na kwa nini iwe hivi Mhe. Waziri?

Mhe. Spika, hii ni wizara yangu, kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati, lakini namuomba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kupitia kwako, wakati atakapokuja hapa atueleze inakuwaje.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tatu tu.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nashukuru. Sasa badala ya kuwapa fursa hizi hawa wafanyakazi na kupata imani na nguvu ya kufanya kazi zao, mbona munawabena namna hii na wala hivi sivyo na hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aje aseme kwamba anao mpango gani kwa mwaka huu mpya wa bajeti hii, ili tuipitishe kwa hawa wafanyakazi wadogo, mishahara yao midogo hamtaki kuwaona kwamba wao wanadhalilika katika hali hii. Kwa kweli wamo munawasifu kwa kufanya vizuri na mbona wao hamutaki kuwafanyia vizuri, tutazuia mambo hapa na wala musijemukatuelewa vyengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la mwisho, kwa kumalizia namuomba Mhe. Waziri, wakati atakapokuja hapa aje kunipa maelezo kuhusu ule mtambo wa baridi kule Soko la Tumbe Pemba umefikia wapi, mwaka jana niliambia kwamba hakujamalizika kule kujengwa, hivi kumekwama kitu gani hadi leo. Nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Asaa Othman Hamad, ahsante sana umeokoa dakika mbili. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tayari anajitayarisha na Mhe. Kazija Khamis Kona naye ajitayarishe.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhanahu Wataala* aliyetujaalia katika hali ya uzima na afya ambayo inayoniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kufanya kazi ya wananchi wetu. Pili, nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Naibu Waziri wake, Mkurugenzi wa Uvuvi pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba hii ambayo leo tunaijadili hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mchango wangu, naomba nianze kwenye Sekta ya Uvuvi kwenye ukurasa wa 5 wa kitabu hichi cha Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, imeelezwa hapa kama wavuvi wanaongezeka na pato la Taifa kutokana na sekta hii, kama hali iko hivyo, tunashukuru sana, lakini bado mpaka hivi sasa hatujawatendea haki wavuvi inavyopaswa, kwa sababu za msingi, kwani tunataja tu hapa kwenye vitabu kwa maandishi na mimi naweza kusema kwamba hakuna chochote kinachofanyika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa itakumbukwa bajeti zilizopita mwaka juzi na mwaka jana na hata Kitabu cha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kilikuwa kinaeleza kuhusu uendelezaji wa wavuvi wadogo wadogo. Namuomba Mhe. Waziri, wakati

atakapokuja kufanya majumuisho, atueleze ni maendeleo gani yanayopatikana katika kuwaendelea wavuvi wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli sekta ya uvuvi inaajiri watu wengi ukiachana na mvuvi mwenyewe, watu wengi wanawasubiri wavuvi wakirudi baharini ambao tunasema ni wachuuzi na mpaka kufika kwa mlaji, inakuwa amepita katika mikono mingi za kuwapatia ajira wananchi wetu na hilo halipingiki.

Mhe. Spika, Hotuba ya Mhe. Waziri, imetolewa na Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Mhe. Mwenyekiti amezungumza hapa kama kulikuwa na utaratibu wa kununua meli na kwenda kuvua Bahari Kuu, lakini mpaka hivi sasa imesita kutokana na bei kubwa ya meli hiyo.

Mhe. Spika, nadhani tusifikie kununua meli moja kama tumeondoa tatizo kwa ajili ya kwenda Bahari Kuu, kwa sababu siku zote nazungumzia ndani ya Baraza hili la Wawakilishi hata tuwe na meli tano, bado hatujawaondolea usumbufu wavuvi, kwa kuzingatia kwamba meli ya uvuvi kwenda Bahari Kuu, baharia wake ni 30 mpaka 40. Sasa Mhe. Waziri, aangalie kwenye takwimu zake aona wavuvi wangapi waliomzunguka. Kwa hivyo, naomba kutoa ushauri wa bure bado ile hatua ya kuendelea wavuvi wadogo wadogo iwepo kinyume na hivyo, atatwanga maji kwenye kinu hayakai. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nimetokea kwenye fani hiyo na siku za nyuma hapa palikuwa na Duka la *Fisheries* na walikuwa wakiuza mitego, *machines* na hata wavuvi wakipata mikopo kwa ajili ya kujiendeleza. Sasa naomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwamba sekta hii inao mpango huo na kama hakuna mpango huo, utatajwa kwenye vitabu na malengo hayatofikiwa hata siku moja.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa huo wa 5 imeelezwa hapa kwamba;

> "kukubaliwa kwa mradi wa ujenzi wa soko la kisasa la Samaki Malindi, ambao utagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Spika, hapa ninapongeza sana, kwa sababu samaki ni chakula kama chakula chengine na kukiwa na mazingira mazuri wakati wanapotoka wavuvi baharini na wachuuzi wakawa na sehemu nzuri kwa ajili ya kuuzia inakuwa ni jambo jema, kwa mfano tukiangalia Soko la Malindi hivi sasa ni chafu sana na kile ni chakula na samaki wanauzwa chini sehemu yenye vimelea tofauti ambavyo vinaweza kutuharibia masuala ya mazingira. Sasa kama mradi huu utafanikiwa na tunaomba ufanikiwe, utaweka mazingira safi na kukuza pato letu la Taifa.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 6 kuhusu Sekta ya Uvuvi pia katika kitabu cha Mhe. Waziri, naomba ninukuu. Kitabu cha bajeti Wizara ya Mifugo na Uvuvi (2014/2015), ukurasa wa 6 unaeleza hivi;

> "Kusomesha wavuvi vijana 13 kwenye Chuo cha Uvuvi Ndegani, kuhusiana na Uvuvi wa Bahari Kuu na wavuvi wengine 12 watasomeshwa kabla ya kwisha kwa mwaka huu wa fedha na mafunzo haya yanayodhaminiwa na Mamlaka ya Bahari Kuu".

Mhe. Spika, kwa kweli hili ni jambo jema la mategemeo na meli tumeshaambiwa hainunuliwi lakini bado tunawasomesha kuweka hali ya tahadhari kabisa, lakini hapa nataka niseme aliyekuwa Waziri wa Uvuvi na Mifugo Mhe. Said Ali Mbarouk alipata kutembelea katika kisiwa cha Kojani na katika majumuisho yake ya ziara yake ile alitoa tamko munipatie vijana wawili waliofika Form IV, ili wakasomeshwe katika Chuo hiki cha Mbegani. Hii ilikuwa mwaka 2012, vijana walipatikana na majina yao yakapelekwa na Wizara ina habari na tumeambiwa pale kama vijana 12 watapelekwa basi sijajua kama hawa vijana wangu wamo au vipi.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika, hata ujifiche namna gani Wakojani katika uvuvi ni wazoefu kwa njia zote. Sasa vijana hawa kama hutowaendeleza hujawatendea haki, na hii kwenda kusoma kwa hawa Wakojani wataelimisha ndugu zao ambao hawana ufahamu wa kutosha katika mambo haya ya uvuvi. Kama kuna kero kuwakamata wavuvi haramu, wakija vijana hawa kuwaelimisha itakuwa vizuri kuliko watu wengine.

Mhe. Spika, tulipeleka majina hawa na tukakaa vikao na Waziri pamoja na katibu, vijana wenyewe naomba niwataje kwa majina na naomba Waziri utakapokuja hapa unieleze kama nafasi hii imepatikana au haikupatikana, tuanze kukamatana hapa hapa. Majina ya vijana hawa ni Asha Abdi Haji Mjaka na Hussein Jaka, na hawa waliambiwa

mustahamili kama hamtokwenda mwaka huu uliopita atakwenda mmoja na mukifanya subira watakwenda wawili sasa tumefanya subira tunaomba vijana wetu wote wawili waende katika Safari ya kusoma Mbegani hakuna sababu ya kuwazuia.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu Mheshimiwa huyu huyu Said Ali Mbarouk alipokuwa Waziri wa Uvuvi na Mifugo katika kutembelea shughuli zake za kikazi alitembelea jimbo la Kojani tena katika kijiji cha Tungoni, Mhe. Farida ni shahidi tulikuwa pamoja huyu alitoa ahadi katika kikundi cha watengeneza chumvi pamoja na wafugaji samaki; kikundi kinaitwa Kwakitunda *Salt and Fishing Carry A School Society* kiko jimbo la Kojani Kiongoni.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisema wafanye makisio ya kuwajengea bwawa kutokana na shughuli zao walizokuwa wanazifanya zilimpendezesha na yeye akataka kutoa mchango wake na walifanya makisio ikapatikana jumla ya shs. 1,894,000/= na wakapeleka katika Afisi zilizokuwepo kule Pemba makisio haya na mpaka leo, Mheshimiwa atakapokuja hapa nakuomba kwa dhati kabisa utueleze hatua ile imefikia wapi. Kwa sababu kama ilivyoelezwa kwenye kitabu chako hapa na naomba ninukuu katika ukurasa wa 39 unasemaje katika idara ya mazao ya baharini Mhe. Spika, naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

"Katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2013/2014 Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Mazao ya baharini ilitekeleza malengo yafuatayo, katika kuimarisha ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na mazao mengine ya baharini. Idara imeanza ujenzi wa bwawa la mfano huko Donge Mchangani imewezekana kusaidia vikundi vya ufugaji wa samaki, mashine tano za kuingizia na kutolea maji katika mabwawa ya samaki kwa vikundi vitano vya wafugaji".

Sawa lakini na hawa walioahidiwa kwa kutekelezewa mambo kama hayo bado hawajapatiwa naomba kwa jicho la huruma muwaangalie hawa. Mheshimiwa tumeshuhudia katika Wizara hii kufanya jitihada zake za kwenda kufundisha watu China isipokuwa mwaka huu hatujapata taarifa yoyote kwenda kujifunza mambo ya ufugaji, lakini mimi ningemuomba Waziri katika ziara iliyofanywa ndani ya miaka miwili anieleze kuna mafanikio gani na wale waliokwenda kusomea habari ya ufugaji wa samaki je, wenziwao wanawapa taaluma hiyo au tunaharibu pesa tu za wananchi. Kwa sababu kama hakuna taaluma yoyote wale kuwafundisha wenzao kwani sioni ukuwaji wa jambo hili, hapana matatizo kwa jambo hili.

Vile vile Mhe. Spika nimpongeze Mkurugenzi wa uvuvi katika kipindi cha mwaka mzima hiki sijaona kuwakamata wavuvi ovyo ovyo, hii ni kutokana na elimu inayotolewa kwa wavuvi nawapongeza sana na waendelee kutoa elimu ili wavuvi wafahamu hasa kwa kushirikiana na jumuiya ya wavuvi ya Wakojani hii kama unashirikiana nao utapata mambo mengi, na wao wamesaidia sana kutoa elimu lakini bahati mbaya hata kuwapongeza ndani ya Baraza hili tumeshindwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ninalotaka nizungumze kuna mradi mkubwa mwa *MACEMP* na mradi huu ulikuwa umefanya mambo mengi mazuri lakini vile vile kulikuwa na boti zimetolewa za uvuvi vijiji mbali mbali. Hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa naomba anieleze ni boti ngapi zimetolewa na mpaka sasa hivi zipo au tayari zimeshafanya manyago, atuelezee kwa sababu kumekuwa na uhalifu mkubwa sana watu wanajifanya zile boti ni za kwao binafsi.

Kwa hivyo tunaomba akija hapa atueleze ule ulikuwa ni mpango mkubwa na mpaka sasa hivi hatuoni matunda yake, hizo boti zimeshaanza kupotea. Sawa wewe ndio mwenye takwimu zote; wapi ulipeleka na wapi zipo, tunataka kujua, wananchi wetu wanalalamika sana.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu bado nazungumzia sheria ya uvuvi No.7 ya mwaka 2010 bado sheria mimi nasema ni kandamizi kwa wavuvi. Sheria hii bado haijaleta kuendeleza wavuvi isipokuwa ni kuwadhibiti wavuvi na kama kuna marekebisho ya sheria basi imefika muda hii sheria ya kuletwa hapa barazani tukaifanyia marekebisho.

Sheria nyingi tumefanya marekebisho na si jambo la aibu nayo kuletwa kufanyiwa marekebisho, mimi sioni mpango wa kuweza kuendeleza wavuvi isipokuwa labda kuwabana wavuvi. Imezungumzwa hapa kila siku kunaundwa kamati za kuwadhibiti wavuvi na sehemu zote zinatiwa *parking* tunasema ni sehemu za hifadhi.

Wao wavuvi wetu watakwenda wapi, sehemu zote tukisema ni sehemu za hifadhi, kufanya kazi zao na bahari kuu hatuwezi kufikia. Hili ni jambo la kuliangalia kwa kina wala si jambo la utashi; ni jambo la kuwekewa utaratibu mzuri na kuwekewa mazingira mazuri kwa wavuvi wetu.

Leo ifike kusema kama umzuie mvuvi kutumia kioo unamtakia mema weye au umzuie mvuvi kutumia viatu vya kuogolea unamtakia mema au uzuie nyavu za kuvulia dagaa unawatakia mema wavuvi. Kwanza mimi nawaambia nchi yetu hii ni ya visiwa na wavuvi wadogo wadogo milele na milele watakuwa hawaondoki, na tujaribu kuwazuia siku moja tuangalie iyo habari itakayokuwepo. Maana huzuii mvuvi tu watu wote umewazuia.

Sasa leo unazuia nyavu za kuvulia dagaa si ndio tunalokula siku zote hilo dagaa na dagaa ni bora *vitamin* kuliko samaki mkubwa kwa kujenga mwili, nikuweka mipango mizuri tu ya kufuata hawa, lakini nasema Serikali na Wizara haijawa tayari kabisa na siku itakayokuwa tayari basi mafanikio yataonekana na wenzetu watafikia malengo. Mimi naona uvuvi wa bahari kuu utakuwa ni ndoto tu, tuwatengenezeeni boti ndogo ndogo hizi za kisasa waweze kufikia, mfano upo pale Malindi kwa boti zile zinaingia mpaka watu sabiini wanaovua; ndugu zangu wa Kikojani pale na Alhamdullillahi riziki inapatikana. Hivyo hivyo na kidogo wanajitahidi kwenda maji mengi kuliko wavuvi wengine wote, sote ni mashahidi tunakutana nao miambani huko. Mie hakuna mwamba hata mmoja utakaoniambia nisiujue hapa.

Kwa hivyo tuweke mazingira mazuri, sio mazingira ya kuwadhibiti tutakuwa na wavuvi wazuri wenye kuleta tija na taifa litafaidika. Mimi siku ya leo sitaki nizungumze sana kwa sababu naona mambo hayajabadilika na kama mambo hayajabadilika. Nawaomba Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake mutembee, kwa kukaa tu humo maofisini hamutaona mafanikio na changamoto ziliopo. Msikubali tu kuandikiwa makabrasha mkatuletea hapa siye tunapima. Mwaka jana imezungumzwa vipi na maendeleo yake hatuyaoni.

Mhe. Spika, nilikuwa na mengi ya kusema lakini kutokana na hali hiyo bado kuna utata mkubwa sana naomba niishie hapo na siungi mkono mpaka Mhe. Waziri anieletee majibu mazuri ya kunitosheleza, na mimi nitamwambia apititishiwe hela yake, lakini *bighairi* ya hivyo mambo mazito. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii ya leo kuweza kuchangia Wizara hii vizuri sana. Kwanza kabla sijaendelea nasema naiunga mkono asilimia kwa mia na madhumuni ya kuunga mkono nnayo makubwa. Mimi nimtafiti na katika utafiti wangu nimegundua kumbe ninatumia *energy* sana kuzungumza na katika Wizara husika kumbe napoteza bure, imekuwa ile *energy* yangu inakwenda bure bila ya mafanikio, na kumbe kuna sehemu ningeitumia *energy* ile kuzungumza basi ingekuwa vizuri sana. Sasa hapa leo sitaki kutumia *energy* yangu kuzungumza ikani-*cost* baadae, lakini wapi nitazungumza Mheshimiwa kwenye Wizara ya Fedha ndipo nitaweza kuzungumza kiburi changu kuhusu Wizara hii.

Mhe. Waziri ameomba fedha 11 bilioni; fedha hizi amezigawa katika mafungu mawili; mafungu mawili haya bilioni nne kwa ajili ya kazi za kawaida na bilioni saba kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Mhe. Fedha hizi kama nitazichukua mie basi kwa suma nimemaliza kabisa. Suma hizi ananinyang'anya kabisa wala sioni kama nimekwenda kununua vitu vingi, nimeweka kwenye *package* ya kuchukua angalau nikatafute yule mchukuzi. Ni fedha ndogo sana Mheshimiwa na hasa kwa Wizara hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri naomba sana turudi tena tukae kitako tuwafikirie hawa watu, kwa sababu mimi siku zote huwa natoa ushauri wangu wa bure Mhe. Spika, kwa kuangalia tunataka miradi mingi Serikali ifanye kazi, lakini midari yenyewe inakuwa ya kipaumbele hasa hawaiangalii hii Wizara si mchezo Mheshimiwa. Wizara hii ndio mkombozi wa masikini kwa mifugo na kwa uvuvi.

Mheshimiwa leo tunakwenda kuwapa fedha hizi bilioni 11, hatufikirii kwa sababu Mheshimiwa ajira ndani ya Serikali hakuna sio siri hiyo, lakini ukimuwezesha mwananchi mimi nataka kukueleza kitu kimoja. Nimefanya *example* ndogo tu na nimewaendea hawa, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mkurugenzi wa uvuvi alikuwa anatoka na nilipokwenda na hoja yangu alirudi ndani hilo lazima nimpongeze. Nilipofika ndani nikamueleza hoja yangu akamtafuta Mkurugenzi mwenzake wa Mazao baharini akamtoa ndani kwenye kikao cha kupanga bajeti akaona hili nililokuja nalo la msingi akaacha yake akaja zake tukakaa.

Mheshimiwa nilikuwa na hoja nzuri Mheshimiwa yule kampa mwenzake kijiti na kijiti kile kakikimbiza na kaita wataalamu wake nimegundua hawa watu ambao wanatumia elimu yao, walivyosomeshwa na Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili ienee kwa faida kubwa na ni kweli.

Mhe. Spika, katika bajeti iliyopita Mhe. Said Ali Mbarouk nilimwambia mambo mawili na namshukuru sana japo atajisifu yeye lakini na mimi nimechangia katika fikra zangu; nilimwambia Mheshimiwa toa vijana wapeleke China alikuja kujibu Mheshimiwa mpango huo upo na kweli kapeleka vijana na mimi mpiga debe nimenufaika jimboni kwangu kapeleka watu China nashukuru kajiwekea jina na ndio hivyo aendelee kujiwekea jina kwenye Wizara yake ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo ziara yetu tutakwenda kesho kutwa kuvunja jungu kama anavyoniambia mwenyewe.

Mheshimiwa vile vile nilimwambia Mheshimiwa sasa hivi tusiangalie uvuvi wa baharini naomba sana tuangalie uvuvi wa nchi kavu utaleta tija, Mheshimiwa huyu kaacha *reference* katika ofisi yake Alhamdulillahi niseme ukweli baada ya muda mchache njo nitakuuzia samaki tani kwa tani.

Waheshimiwa wametoa lugha nzuri wamenipa wataalamu wametufundisha alhamdullillahi leo hodhi langu nachukua elfu moja mia saba samaki sihangaiki na vihori. Sitohangaika na maboti, sitohangaika na masuala mengine Mheshimiwa, wamefanya jambo la msingi wametuletea mbegu nzuri za kisasa zinakwenda na wakati. Haya ndiyo tunayosema na haya ndiyo tunayoyataka, lazima wajipongeze kwa sababu hawana bajeti kubwa; hii bajeti haitotimia asilimia hii waliyoiomba wao siku moja.

Sasa leo mie naona haya sana kuwakamata kusema Waziri utanionesha leo sijui nitazuia fungu, isipokuwa nakuteteya wewe sasa ili uweze kukamilisha masuala haya utusaidie wanyonge katika hizo *activities* mbili nilizosema. Mheshimiwa walitupa mbegu za mbuzi wa kisasa leo nina maziwa mengi sana ya mbuzi, sina pa kuuziya jitihada zao hawa mwenyewe Katibu Mkuu yupo namshukuru sana anajitahidi kutokana na taaluma yake. Nimeanza mbuzi kidogo sasa wanapukutika wanakuwa wengi, hivi ndivyo tunavyotaka Mheshimiwa niwashukuru sana pamoja na umasikini wenu tusaidieni hivyo hivyo na inshaallah Mwenyezi Mungu iko siku Mhe. Waziri anakubali na namshukuru kwa hilo, Waziri atakuoneni na mimi nina imani hiyo atakuoneni na mara hii atakupeni asilimia inayotakiwa. Kwa sababu kwa vilio vya Waheshimiwa mara nyingi sana vinakubalika.

Mhe. Spika, nina taaluma sasa hivi ya kufuga samaki katika hii minai mimi nishukuru sana na hivi ndivyo inavyotakiwa sheria lazima tuzifuate kwa mujibu wa utaratibu. Kwa sababu kuna watu wengine wanachukua vigezo vya kwenda kuharibu kwa makusudi lakini kumbe imekuwa ule ufugaji wenu wa kuzuiya sehemu ambayo isiyohusika msende kuvua kumbe kwa mantiki sio kumuua mtu masikini. Kwa sababu tunavuruga, tunawaua, sasa hivi samaki kwa mabaruti tunachukua nyavu ndogo ambazo huwa hazistahiki hilo tuliseme tusilifumbie macho.

Sasa hivi leo tukiangalia kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa sasa hivi samaki wako mbali sana tofauti na zamani, zamani mimi nikienda Kizingo tu kwa mishipi nikirusha tu napata samaki leo hupati pale samaki, lakini kumbe kutokana na hali halisi ilivyo kuwa tunawavuruga kutokana na kutumia makemikali yaliyokuwa hayastahiki kutumia mule ndani, tunaondoa mazalio kutokana na haistahiki kuendelea kule ndani hili tukitaka tusitake lazima tulikubali.

Lakini ukiangalia nchi za wenzetu au sehemu za wenzetu leo wanakwenda watu bamvua mbali mbali wanakwambia huko tunakokwenda sijui Kisiju, wanakwenda Mafia, wanakwenda kule kuweka madawa na wana kambi zao kule itakuwa hawapati shida kwa sababu tayari bamvua kule lishawiva, wanakwenda kuchota samaki tu. Mheshimiwa kule sasa na sisi tungekuwa mmoja katika vigezo vya aina moja tukubaliane tu tuweke *special programm;* tuseme mara hii tunazuia ukanda huu na tunakwenda kuvua upande huu, mimi nafikiria tusingefika pahali tukalazimishwa kuwa lazima tuwe na maboti ya hali ya juu hatuyapati hata tukilazimisha bure tu, Mheshimiwa hilo ukweli tuseme, na tulikuwa na maboti mengi sana mimi shuhuda. Lakini leo ukifaya *research* maboti yale yako wapi, sijui kama hayajaingia jikoni kwa kuvunjwa. Njoo unipe idadi angalau zipo 60 sasa hivi zinafanya kazi, fedha chungunzima tulipoteza. Nyavu tulitoa nyingi sana leo ziko wapi na kwa nini utanipa wewe jibu, kwa sababu nipate *reference* ya maelezo yaliyokuwa mazuri sana.

Kwa sababu Mkurugenzi huyu alijitahidi sana ku- *organize* masuala kama haya alijitahidi sana tu, alihangaika sana kijana huyu si mwili wake ule mwembamba basi tu shida ya kazi lakini angekuwa katulia mwili wake angekuwa mnene. Alijikubalisha kufanya *physically* ili kuwaondoa watu katika umaskini, lakini Mheshimiwa tume-*disappear*

tumeiwacha ile *knowledge* ya mwenyewe Mkurugenzi alivyotukusudia. Alikuwa na *plan* ya kutuondolea umaskini kwa kupitia njia hizo hatimae Mheshimiwa hatukuweza kuendeleza *knowledge* hiyo.

Sasa Mhe. niende katika mifugo. Ninashukuru sana tulipiga kelele miaka mingi sana ile mitambo yetu pale lakini ninashukuru mtambo ule unafanya kazi vizuri, na kuna kijana mmoja ambae ni mzuri sana ninaweza kusema na huyo lazima mumuenzi na mumsaidie japo mafuta, wenyewe wafugaji wanamsaidia kijana Khamis, ukimpigia simu tu anakwenda katika sehemu husika. Sasa tunaomba maofisa kama wale wengine wajitokeze wajitume kama yeye. Kwa sababu Mheshimiwa kuna watu wengine hawana taaluma ya uzalishaji, naomba tutoe taaluma *special* kwa wazalishaji, ili waweze kujua jinsi gani vya kufanya hata akifika *doctor* awahi kuweza kumuokoa yule myama anaetaka kuja duniani.

Sasa nalo hilo naomba sana waelimishwe wananchi na wawe na *first aid* ndogo ya kuweza kuwasaidia, ili kuweza kuwapunguzia *distance* ya kuonana na *doctor*. Ningeomba hilo tungejaribu kufanya shehia hadi shehia tukawa-*train* pale akawepo *local doctor* ili kuweza kusaidia. Hiyo ninafikiria itasaidia kupunguza mtu kwenda mbali sana.

Halafu la pili, ningeomba sana tujaribu kutafuta mbegu ambazo zilizokuwa sasa hivi ni za kisasa ambazo kwa mfano utakuta kuku wa Kiswahili, unaambiwa huyu ni kuku wa Kiswahili lakini huwezi kuamini kutokana na ile *modality* aliyokuwa nayo yeye, ni *heavy weight.* Ningeomba nalo hilo tungejaribu kuwatafutia wafugaji wetu zile mbegu za kisasa ambazo zinaweza zikapata soko haraka sana katika maeneo yetu ya utalii.

Mhe. Spika, lakini mwaka jana tuliuliza suali kuhusiana na nyumba; nyumba zenu zile nakumbuka mimi kama tatu tu, hebu leo niambie ziko wapi zile nyumba na mpaka leo mmefikia wapi, ili tukipata wataalam tuweze kuwaweka sio ukawakodie hoteli. Naomba sana hilo uweze kunitafutia.

Mhe. Spika, tuendelee na mbegu za kisasa za mbuzi anaozaa mbuzi wawili wawili na maziwa mengi. Hili nalo mungeliweka *special programm* sasa hivi, katika hii keki mtakayogaiwa gaiwa kidogo ningeomba sana mungeendelea kuweka *special programm* ya kutafuta hawa mkawekeza hasa pale sasa hivi tuwe serious katika suala hili. Ninaomba sana Mheshimiwa kwa sababu hili ndani yake lina tija kabisa. Ninaomba sana Mhe. Spika, kuwa Katibu Mkuu tutakapomkabidhi fedha hizi mimi naomba sana, mimi hili halina tatizo kupitisha tutapitisha tu, lakini ninamuomba sana pamoja na ufinyu wake wa bajeti basi aangalie mara hii katika sehemu hiyo ya kutafuta mbuzi ambao wa kisa, ambao tunakweda nao na wakati. Hapa leo ninasikia lita moja umeitupa shs. 1500 ya maziwa ya mbuzi kuliko maziwa ya ng'ombe.

Halafu Mhe. Spika, nimegundua kuwa wakipata tiba na wakipata malisho mazuri basi hawa mara moja wanaweza kukupatia utajiri kwa yule mnyonge kwa sababu leo mbuzi mmoja angali kidogo anafika si chini ya laki nne mpaka laki tano. Akiwa mkubwa si chini ya laki saba na kuendelea. Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri wangu tena ninamshukuru sana na ninamsifu sana pamoja na Naibu wake Waziri kutokana na uelewano wao. Hii ni adimu kabisa, hakuna siri kwanza ni vijana kabisa *including* na Katibu wao.

Maana yake Mhe. Spika, ukweli Dkt. Sheni amepanga hasa ile *surf* ya wizara hii, ni mpya lakini na utendaji wao unafurahisha, ukweli tuseme. Tufike pahali tuwape *relief* na wao sio tuwatie kitanzi cha roho tu. Panapo kitanzi cha roho tutapiga wala hatutoogopa. Lakini hawa wangali new katika Ofisi hii, lakini jitihada zao tumeziona jinsi gani wanazofanya.

Vile vile nazungumza tena mara hii, naomba sana sijui katika bajeti yako una *programm* gani za kuwapeleka China vijana ambao tayari wamekuwa sasa hivi, nataka ufanye *two groups*, maofisa na wao uwachukue kama 5 na wakulima wende kama 5. Ninaomba sana hilo nayo hiyo itakupa sifa nzuri sana. Kwa mfano kama mimi sikwenda China wala sikwenda Marekani lakini leo ukinambia mbuzi huyu anafanywa vipi nitakufundisha, samaki huyu nitamfuga kwa misingi gani nitakufundisha. Sasa tuwatafute wale watu wenye akili kama hizo ili tuwapeleke kule waje waeneze kwa akili za watu wengine.

Mhe. Spika, naomba nimege wakati wangu narudia tena wala si aibu wala si dhambi, ninaishukuru sana Wizara hii naiunga mkono asilimia mia kwa mia na ninawashawishi wenzangu, wapenzi wangu wa *back bencher* tuwasaidieni kabisa hawa, nawaomba sana, sana. Ahsante sana.

M**he. Kazija Khamis Kona:** Ahsante Mhe. Spika, nami kunipa nafasi ya kuweza kuchangia machache katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi katika mwaka huu wa 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa kuanzia mchango wangu naanza na ukurasa wa 6 kuna changamoto katika Sekta ya Uvuvi, ambayo ni changamoto ya uvuvi haramu kutoka watu wa nchi za nje na vijana wazawa wa Zanzibar. Mimi niseme hili haliepukiki. Kwa sababu gani nikasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu bado serikali yetu haijawa tayari kuwaendeleza wavuvi wetu kama inavyojipangia katika vitabu vyao.

Mhe. Spika, linajionesha hilo wazi katika ukurasa wa 36, unaonesha fedha zilizotengewa katika Idara hiyo sijauona lakini ndio ninautafuta, ni jumla ya shilingi 100,000,000 lakini hadi sasa hivi fedha zilizoingizwa ni 1,660,000. Sasa hapa mimi ninajiuliza hii serikali kweli iko tayari kuwaendeleza wavuvi au vijana wetu waondokane na umaskini.

Mhe. Waziri serikali yetu hii hapa inatucheza shere haijawa tayari na vijana wengi sasa hivi hawana ajira, na kama hawana ajira. Vijana hawa tunategemea ni taifa letu la kesho au pia wafanye miradi kupitia uvuvi ili taifa letu liende mbele.

Mhe. Spika, mpaka muda huu tunaimbiwa nyimbo tu uvuvi wa bahari kuu, uvuvi wa bahari kuu. Lakini kimsingi bado serikali haijawa tayari ni maneno tu yanayotoka mdomoni, kwa kuwa mdomo ni nyumba ya maneno basi utatoa maneno.

Mhe. Spika, hapa niiombe serikali siionei Wizara ninaionea serikali sasa hivi kwani hawa watu wa Wizara an Idara hii wanajipangia vizuri lakini kutokana na ukosefu wa kuingiziwa fedha wanakuwa hawawezi kufanya kazi zao ipasavyo, wala kuwaendeleza hawawezi. Lakini ninaisemea serikali kwa sababu serikali ndio baba ndio mama. Sasa serikali ninaiomba kama kweli ina nia njema ya kuendeleza wavuvi waondokane na uvuvi haramu basi serikali ijikite na suala hili, angalau waende uvuvi wa kina kirefu na hatimae uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, nikiendelea na Idara hiyo hiyo ya uvuvi kuna kamati hizi za wavuvi zilizoundwa, kamati hizi zinafanya kazi nzuri kuwaelimisha wavuvi kuondokana na uvuvi wa haramu. Lakini cha kusikitisha kamati hizi huwa hazigaiwi hata ile pesa ya sabuni, tunawatuma tu. Sasa Mhe. Waziri hapa nataka aje anambie je, Wizara yake hizi kamati za wavuvi atazisaidia vipi ili wafanye kazi kwa pamoja kusaidiana katika Wizara yao na wavuvi wao.

Mhe. Spika, nakuja kwenye Idara Mifugo hapa inasema inataka kuwaendeleza wafugaji wadogo wadogo, hasa wa kuku. Lakini hapa nataka niseme Mhe. Spika, kabla ya kuwaendeleza au kuwapatia vifaranga au mifugo ya kuku ijikite sana na suala la kuwapa taaluma wafugaji wetu. Kwa sababu suala hili linakosekana hata kama wanaitoa taaluma lakini inakuwa haitoshelezi. Sasa niwaombe tu waendelee na kuitoa taaluma ili mifugo yao wafugaji wetu wapate faida yenye tija.

Pia Mhe. Spika, wafugaji wetu hasa wa kuku tulipotembelea na wakatupa malalamiko yao kwamba kuku wao wanajitahidi kutaga lakini kuangua ndio tatizo. Sasa Mhe. Waziri sijui atawasaidia nini wafugaji hawa ili kuwapatia mashine ya kutotolea vifaranga.

Pia wafugaji wetu huwa hawaangaliwi wanapopewa ile mifugo; sehemu ya kuwekea mifugo yao inakuwa hairidhishi, sasa na hapa niiombe Wizara kabla haijawapa basi iwaandae namna ya kuiweka mifugo yao vizuri, hali ya usafi na usalama. Kwa sababu maradhi mengine pia yanasababishwa na sehemu zile ambazo kuku tunawaweka hasa kwa vifaranga vidogo vidogo huwa vinapoteza maisha yao.

Mhe. Spika, kwa kuendelea niende upande wa masoko, tunaipongeza serikali kwa kupitia mradi ule wa MASEMP kutujengea masoko ya kisasa, mazuri lakini masoko yale hayajajengewa vyoo. Watu wanapotoka baharini huwa wanataka kubadilisha nguo zao, kujiosha mwili wao. Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri afanye utaratibu basi angalau kujengewa vyoo kwa utaratibu ambao ataona unafa katika haya masoko yetu.

Mhe. Spika, kuna changamoto nyengine kutokana na bei ndogo ya mwani. Hapa serikali ninaiomba iwasaidie akina mama kilimo chao cha mwani. Huwa wanategemewa sana na familia zao na kilimo cha mwani bado kina changamoto ya bei. Sasa Wizara ije inambie itafanya utaratibu gani ili kuwasaidia wakulima wa mwani. Kwa sababu wakulima wa mwani vifaa vyote wananunua ikiwemo taitai kamba na bado huku bei ya mwani ni ndogo. Sasa sijui Wizara itachukua juhudi gani ya kuwasaidia wakulima wetu wa mwani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi *mia fil mia* huku nikisisitiza serikali ijikite katika sekta ya uvuvi kwa kuwapatia fedha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ili kuwaendeleza vijana wetu katika uvuvi wa kina kirefu. Ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii nikatoa mchango wangu mfupi sana katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdillahi Jihad Hassan.

Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia na kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad Salallahu Alayhi Wasalam kwa kutujaalia tukaweza kukutana hapa tukiwa na hali ya afya njema na kama kuna wenzetu hawakufika hapa leo kwa ugonjwa basi Mwenyezi Mungu awajaalie awaponyeshe upesi, ili muda mwengine tushirikiane nao.

Mhe. Spika, kwanza sina budi nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa ujumla kwa juhudi zao wanazozifanya katika kutuendeleza wananchi wa Zanzibar hatuna budi tuwashukuru.

Mimi mchango wangu wa mwanzo kuna suala moja ambalo sijalikuta katika kitabu hiki, sijui niende katika kitabu gani suala hili nilikute kwa sababu suala la uvunaji wa chumvi ni suala la mazao ya baharini. Sasa katika kitabu cha Mhe. Waziri hamna kabisa masuala yale ya kuwawezesha wananchi wenye mabwawa ya chumvi.

Suala hili mwaka jana Mhe. Spika, lilileta mzozo kidogo kupitia mchango wa Mhe. Salma, lilionekana suala la chumvi halijulikani likae wapi. Ukija Waziri wa Uvuvi na Mifugo anakwambia yeye hahusikani na suala hili, ukija Wizara ya Biashara yeye anasema ni mtu wa biashara tu. Lakini Kilimo na yeye kwa kweli Mhe. Spika, hatulijui suala hili liko wapi. Sasa leo katika hotuba hii ya kitabu hiki angekuwepo Waziri wa Kilimo na Waziri wa Biashara leo ingebidi leo tuwasimamishe hapa watupe ufumbuzi suala hili liko wapi. Kwa sababu hawa na wao ni wazalishaji wa mazao ya baharini. Sasa pia ni ajira wanajiajiri pia wananchi tunatakiwa tutumie chumvi iliyokuwa ina uhakika wa madini joto. Sasa kama hatujui tukimbilie wapi katika suala hili. Hilo ni moja.

Jengine Mhe. Spika, asubuhi hapa niliuliza suala la nyongeza kupitia wizara ambapo alisema Mhe. Naibu Waziri tangu kuanzia 2007 kuna vikundi ambavyo wanaviwezesha katika shughuli mbali mbali za uvuvi. Sasa si miaka kidogo hiyo kuanzia 2007 mpaka leo kufikia 2014. Katika suala langu la nyongeza nilimuuliza kwa sababu ni mtu wa baharini na tuna bahari nzuri na kuna vikundi ambavyo ameshaenda kuviwezesha, lakini kama hajenda basi aniahidi ni lini atakwenda kuviwezesha vikundi vilivyopo eneo lile. Kwa hiyo, kanambia atanijibu kwa maandishi hajanijibu amenipa orodha ya vikundi lakini haipo Tumbe, kwa hiyo naliingiza tena hapa, ili Mhe. Waziri aje anieleze Tumbe kuna vikundi vingapi ambavyo anaviwezesha katika masuala ya uvuvi. Ukitizama Tumbe ni bahari kubwa; bahari iliyokuwa na wavuvi wengi, bahari iliyokuwa na wachuuzi wengi wanaofika pale. Kwa hiyo, tangu wameyafanya masuala haya ina maana wanafanya mambo yao ambayo hawazingatii yale maeneo ya kuwapa kipaumbele katika shughuli zao. Hilo ni jengine Mhe. Spika.

Suala jengine kwenye sekta za mifugo na uvuvi nchini hapa ameandika mafanikio katika sekta ya mifugo. La kwanza kuongeza uzalishaji wa maziwa kufikia lita 24,343 kwa mwaka 2012 hadi kufikia lita 27, 244. Lakini kuna ongezeko tena la uzalishaji wa mayai tani amezitaja hapa nyingi tu, lakini kuna ongezeko tena la tani ya uzalishaji wa nyama ya ng'ombe. Kwa hiyo, haya ni mafanikio mazuri kwa kweli yanayopatikana lakini mimi nataka aje hapa Mhe. Waziri anifahamishe mafanikio haya ni miongoni mwa uzalishaji wa Zanzibar au ni nyama zinazotoka Bara na kuja huku kwetu. Kwa sababu kama zinatoka Bara na kuletwa hapa hayajawa mafanikio yakujisifu sisi, ni ulaji tu huo tunaletewa. Mafanikio mazuri katika sekta hii ingelikuwa mambo haya yanatoka Zanzibar. Tusiringie cha watu, watu wakija na biashara zao tukajifanya sisi ndio tunaozalisha na ndio wauzaji wa nyama, aa!

Mhe. Spika, akija Mhe. Waziri anieleze ufafanuzi huo, lakini kama haya ni mafanikio kuna Mwekezaji huyu Said Bakhreska, yeye anataka kuanzisha kiwanda cha maziwa huko Fumba, kwa nini hatujaambiwa mradi umefikia wapi kama haya ni mafanikio yaliyopatikana kwa sekta hii ya uvuvi na sekta ya mifugo. Kwa hiyo, aje atueleze Mhe. Waziri tusiandikiwe kwenye vitabu mafanikio tumepata hapa kumbe tunaringia mayai yanayotoka Mombasa, ng'ombe watokao Bara wanaoletwa hapa halafu sisi tunasema kama tunaongeza uzalishaji.

Mhe. Spika, kuna changamoto hii moja inayoelezea kutowafikia baadhi ya wananchi wanaohitaji huduma kutokana na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi. Mheshimiwa hii changamoto naona ni ya muda mrefu nayo kitabu cha

mwaka jana imo, kitabu hiki imo lakini hawajatwambia changamoto hii kama wizara wanaikabiliana vipi. Kwa sababu hizi ni sekta muhimu na kama hujawafikia wananchi ina maana bado hujafanya kazi. Sasa haya masuala yote wanayotueleza humu sijui vikundi, sijui ufugaji na wao wanasema kama wanaupungufu na changamoto hii inawakabili. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kama wizara wana muelekeo gani katika kulipatia ufumbuzi suala hili.

Suala jengine ni mwelekeo wa baadae katika sekta ya mifugo, amesema kama kuandaa mazingira ya kuifanyia sekta ya mifugo kuwa mwajiri mkubwa wa kundi la vijana kwa kuwapatia ng'ombe na kuendelea.

Mheshimiwa hii ndio hali halisi ilivyo kuwa sekta hii tutegemee kupata ajira na ni ukweli usiopinga. Mhe. Waziri hapa kwa sababu sekta hii kuna maeneo maalum ambayo kila eneo pengine Mwenyezi Mungu kajaalia kuna fani yake, na nakumbuka mwaka jana au mwaka juzi nilipochangia niliomba sana Mhe. Waziri kuwaendeleza wale wafugaji wa Micheweni katika ule ufugaji wa mbuzi wa maziwa, kwa sababu wana ufugaji wa wale mbuzi.

Nikaomba hili suala wawaendeleze wale wafugaji wa maeneo yale kule kwa sababu ni fani yao, lakini hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi ili na mimi nielewe hivyo vikwazo vinavyojitokeza.

Pia nichukue fursa hii kuwapongeza katika wafugaji wa mazao ya baharini, jumla ya vifaranga vya samaki 20,546 Unguja na Pemba sitaki niendelee hapo. Mheshimiwa mimi niwapongeze sana kwa suala hili kwa kupeleka hivi vifaranga kwa wafugaji wa samaki.

Suala jengine Mhe. Spika, katika changamoto moja anayoisema kama kuna bei ndogo ya zao la mwani nayo pia ishakuwa ni hadithi ya muda mrefu, kwa hiyo sasa atwambie hii wizara wao wanachukua jitihada gani katika kulitafutia ufumbuzi suala hili. Naomba Mhe. Waziri atueleze kwa sababu siku zote tusiambiwe bei ndogo lakini na ufuatiliaji nao unakuwa ni mdogo kiasi fulani.

Mhe. Spika, jengine ambalo pengine litakuwa la mwisho ni la ujenzi wa soko la Tumbe. Mhe. Spika, watu wa Tumbe tulifanya matumaini makubwa sana yakujengewa soko lile. Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Uvuvi wa mwanzo alitwambia tutajengewa soko la kisasa, tutiliwe vyumba vya baridi, tujengewe na mahodhi, tujengewe na kila kitu kwa hiyo tukajenga matumaini. Lakini kwa kweli Mhe. Spika, soko hili limefeli kabisa, na sasa hivi hata wizara wenyewe hata kulizungumza hawalizungumzi ndio lishapita lile.

Mhe. Spika, zile ni pesa zilizotolewa kama ni wafadhili, kama ni walipa kodi wa nchi hii, kwa hiyo hatuwezi kuziachia pesa zile zikateketea. Soko lile limejengwa lakini soko halina kina cha kirefu halifai, kama wao walikwenda mle wakatoa zile *tiles* lakini hata kina cha urefu wa lile soko halifai, ina maana mkandarasi waliyempa hana sifa za kuwa mkandarasi inavyoonekana hawakufanya utafiti. Kwa hiyo, Mhe. Spika, mradi huu ulianza tangu tarehe 27 January 2011 muda mrefu sana jambo ambalo tungekuwa lile soko tushalitumia. Hivi sasa pengine ingekuwa linataka kufanyiwa ukarabati mwengine. Lakini mpaka leo cha kusikitisha soko lile hata haliulizwi tena hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe majibu mazuri ya soko hili.

Pia Mhe. Waziri kama nilivyokwambia Mhe. Spika, kwamba hawana ufuatiliaji kuna kitabu hiki ambacho ni ripoti ya mkaguzi kwa miradi na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012. Ripoti hii si ya leo, ripoti hii mimi nataka niisome huku mwisho kama wana ufuatiliaji watakuwa wanacho hiki kitabu kwa sababu nao ni jumla ya mradi.

Kitabu kinasema ''ukaguzi uliofanywa haukuridhishwa na hali halisi ya ujenzi huo ukilinganisha na fedha zilizotolewa na kutumika hadi tukakamilisha ukaguzi wa ujenzi wa sehemu ya soko hilo haujakamilika. Hali halisi ya utekelezaji wa sehemu ya soko la Tumbe Pemba ambao haukukamilika na kama inavyoonekana hapa jadweli…'' limeandikwa na wao kama ni wizara wanaofuatilia suala hili bila shaka matatizo haya wanayajajua. Kwa hiyo sitaki niwatajie hata pesa moja, nataka aje Mhe. Waziri aniambie ni kiasi gani cha fedha kinachotumika katika ujenzi wa soko lile. Sitaji, mpaka pesa zimo lakini nataka aje aniambie yeye na soko lile halikufanikiwa. Hilo ni moja.

Suala jengine Mhe. Spika, kuna deni ambalo wananchi wa kijiji kile pale walitumia nguvu zao na mpaka leo hii hawajalipwa pesa zao walizofanyia kazi pale. Mhe. Naibu Waziri ukimuuliza anakwambia kwamba tuna pesa ambazo hatujailipa hii kampuni kwa hiyo tunategemea tuwalipe pesa hizi lakini hakuna ufuatiliaji. Kwa hiyo, Mhe.

Spika, kwa suala hili leo basi naomba Mhe. Waziri alete majibu yatakayonifariji ili na mimi nimpitishie bajeti yake. Kwa hayo machache Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii kukutana hapa kujadili wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/2015.

La pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii ili na mimi kusema machache katika hotuba hii.

Kwa kuanzia Mhe. Spika, kabla sijaingia kwenye bajeti hii naomba nitoe masikitiko yangu kidogo kwa wachapaji wa vitabu hivi kwa sababu inaonekana hizi *machines* mpya sijui hazifanyi kazi vizuri au vipi. Mheshimiwa kitabu cha leo hiki chote karatasi zinanyambuka, na si hiki tu hata cha bajeti iliyopita ilikuwa kazi ndio hii hii, sasa sijui kuna matatizo gani hizi *machines* mpya ambazo zimekuja.

Mhe. Spika, kwa kuendelea naomba nianze na sekta ya mifugo, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri pamoja na msaidizi wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lakini pongezi za pekee ziende kwa watendaji ambao wao ndio wamehakikisha kwamba waziri anawasilisha hii hotuba nzuri ambayo ameiwasilisha leo.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Ali Salum Haji anazungumza aliomba maelezo kuhusu machinjio ya Kisakasaka, na mimi naomba Mhe. Waziri kwa sababu humu sijaona akija atueleze matengenezo yake na maboresho ya machinjio yale yamefikia wapi. Wakati Mhe. Waziri anawasilisha hotuba yake alitueleza kuwa sekta ya mifugo imeweza kukua kwa asilimia 3.1 na kuchangia asilimia 3.8 ya pato la taifa kwa mwaka 2013.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, nilikuwa naiomba serikali iangalie sekta hii ili kuona kwamba inachangia kiwango cha juu zaidi na kuiangalia kwenyewe maana yake ni pamoja na kuboresha miundombinu ya maeneo ya sekta ya mifugo. Miundombinu hiyo ikiwemo barabara ili kuwe na urahisi wa kufikia maeneo hayo.

Mhe. Spika, nasema hili nitolee mfano wa barabara ya Kisakasaka ile ya kilomita 4 kuelekea kwenye machinjio. Kilomita 4 sio nyingi lakini kwa vile barabara ilivyo ni vigumu sana inakuwa mara nyengine wale wanaokwenda kupata mahitaji katika machinjio kufika. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana serikali iangalie barabara ile ili kuona kwamba kunakuwa na *access* ya kufika machinjioni na ile sekta ya mifugo ambayo inaongeza pato katika pato la taifa iongeze zaidi ya kile ambacho kinaiongeza hivi sasa.

Mhe. Spika, najua wizara hii haihusiani na mambo ya barabara lakini najua kwamba serikali inafanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba akija hapa Mhe. Waziri kufanya majumuisho nipate angalau kauli ya serikali kwamba ina mpango gani wa kuiboresha barabara ile hata sio kwa kiwango cha lami angalau iparwe ikae sawa.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu sekta ya uvuvi; sekta hii na mimi naungana na Mhe. Kazija kwa masikitiko kwamba serikali haijawa tayari kuwezesha vijana wetu kuona kwamba wanajiajiri wenyewe katika sekta hii ya uvuvi.

Mhe. Spika, wakati naangalia kiambatanisho Nam. 3 ambacho ndio kinazungumzia mradi wa kuimarisha uvuvi wa kina kirefu cha maji, nilipendezeshwa na malengo ambayo mradi huu yaliyokuwa nayo kwa sababu katika mwaka 2013/2014 walijipangia kubomoa jengo kongwe la *ZAFICO*, kuendesha mafunzo ya uvuvi wa kina kirefu cha maji kwa vijana 30 na kukimu mahitaji ya vyombo kama boti zitakazonunuliwa kupitia mradi wa ajira kwa vijana, ili kuwawezesha vijana kuvua maji ya kina kirefu. Lakini nikashangazwa sana na maelezo ya utekelezaji halisi kwamba kazi zilizopangwa hazikufanyika.

Mhe. Spika, kuangalia vizuri nikaona kwamba mradi huu uliombewa milioni 100,000,000 lakini matokeo yake ukaingiziwa milioni 1,660,000. Kwa kweli serikali haijawa tayari kuwawezesha vijana hawa kuona kwamba wanavua uvuvi ulio halali, lakini pia wanajipatia ajira kwa sababu serikali haina uwezo wa kuajiri vijana wote, na hao ambao wanajiajiri inashindwa kuwawezesha, ili kuona kwamba ile ajira wanayojiajiri inawapatia kipato.

Mhe. Spika, ndio maana sishangai katika *page* ya 8 walipoandika changamoto katika sekta ya uvuvi; changamoto Nam.2 nikuongezeka kwa uvuvi haramu kutokana na kuwepo kwa wavuvi kutoka nje ya Zanzibar na wavuvi vijana wazawa katika maeneo ya hifadhi, na kuvua uvuvi haramu na kusababisha uharibifu wa mazingira ya bahari.

Sishangai kwamba kuna changamoto hii kwa sababu lengo ambalo lilipangwa kuwaelimisha vijana hawa halikufanyika. Pia vifaa ambavyo vingewawezesha kwenda kuvua kina kirefu havijanunuliwa. Kwa hiyo, serikali ione ni jinsi gani kwamba inaposhindwa kutekeleza kitu kimoja inasababisha *costs* nyengine zisizo za lazima.

Mhe. Spika, nikimaliza mradi wa kuimarisha uvuvi naomba kidogo nizungumzie uvuvi haramu ambao unaendelea hivi sasa. Sisi vijana mara nyingi tunakuwa kwenye mitandao na *recently* nilikutana na *link or network* moja ya vijana ambao wanazungumzia ongezeko la uvuvi wa baruti katika Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, naomba hili wizara waliangalie sana pengine ni ule ule upungufu wa bajeti waliokuwanao hawakuweza kufika Pemba na kuona jinsi gani uvuvi unavyoendeshwa, lakini tuliombwa sana katika mtandao ule na nafikiri Mhe. Mahmoud Thabit Kombo nae alikuwemo, walituomba sana tulifikishe hapa ili serikali iangalie namna yaku-*deal* na ile *issue.* Kwa sababu wanasema imekuwa ni kubwa mno kwamba inatishia hata uhai wa viumbe wa baharini wa baadae.

Mhe. Spika, mimi sina mengi kwa sababu sio mtaalamu sana wa mifugo na uvuvi naomba kuishia hapo. Ahsante sana, nashukuru.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza na mimi sina budi kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na pia niwapongeze watendaji wake kwa kushirkiana nae kwa kuleta hotuba hii katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Spika, na mimi sitokuwa na mchango mkubwa, kwa sababu niliaga kwenda kunywa chai lakini kwa bahati sikuwahi. Kwa hiyo, mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana, lakini kwanza nije katika Sekta ya Mifugo.

Mhe. Spika, sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi walioko vijijini, kwani ukiangalia wananchi wengi wa vijijini hutegemea sana mifugo kwa ajili ya kuendeleza maisha yao, lakini wananchi hao wana matatizo makubwa sana ya ukosefu wa wataalamu wa ufugaji na pia kukosa mahitaji ya kununulia vifaa.

Mhe. Spika, niseme kwamba wafugaji hawa husumbuliwa sana na ushauri wa kitaalamu kutokana na usumbufu mkubwa wa maafisa wa mifugo; jambo ambalo hupelekea kufuga mifugo yao kienyeji. Kutokana na hili, mifugo mingi husumbuliwa na maradhi ambapo hupelekea mifugo hiyo kushindwa kudhibiti maradhi hayo. Pia ukosefu wa kupata mikopo kwa wafugaji hawa kuendeleza shughuli zao.

Mhe. Spika, kuhusu soko; soko limekuwa ni tatizo kubwa kwa wafugaji hawa vijijini, wakati mwengine hulazimika kuuza mazao yao kwa bei nafuu jambo ambalo linawapelekea kuuza kwa hasara. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri aangalie sana wafugaji kwani hawa ndio kioo chetu sisi sote hapa nchini.

Vile vile nikija katika Sekta ya Uvuvi; sekta hii wananchi wengi huwekeza lakini wananchi hawa hukumbana na matatizo mengi sana au matatizo mbali mbali. Kwa hiyo, wananchi hawa wana haki ya kuangaliwa sana kuhusu sekta hii ya uvuvi kama vile vifaa vya kuvulia, inakuwa ni tatizo zikiwemo boti, nyavu na zana nyengine.

Pia wavuvi hawa wamekuwa wakipambana sana na tatizo la soko la kuuzia bidhaa zao. Kwa sababu kuna baadhi ya wavuvi hawa huvua kwa msimu, unapofika msimu wa kiza wavuvi hawa wanapata samaki wengi, sasa hushindwa kuwauza na ikabidi samaki wale aidha waoze au wauze kwa bei ya kutupa tu. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri awaangalie wavuvi wetu hawa.

Mhe. Spika, wakati mwengine samaki hao huharibika kutokana na kuwa hawana soko jambo ambalo hutia hasara kubwa kwa wavuvi wetu. Niishauri serikali kwamba ijenge vyumba katika sehemu za madiko kwa zile sehemu ambazo huwa zinatoa samaki wengi, ili wavuvi hawa wanapovua samaki wale waweze kuwahifadhi.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mazao ya Baharini. Akinamama wengi hujishughulisha na shughuli za mazao ya baharini kama vile mwani, chaza na kadhalika. Kwa hivyo, nikija katika kilimo cha chaza niseme kwamba akinamama wa Wilaya ya Mkoani ambao wanatoka Kijiji cha Makombeni hawa wanajishughulisha sana na kilimo hiki. Akinamama hawa wamekuwa wakikabiliwa na matatizo kadhaa kama vile vifaa vya kufanyia kazi, vikiwemo *gloves*, visu pamoja na miwani hata na viatu vya baharini.

Vile vile niseme kwamba hawana soko wana ushirika hawa la kuuzia bidhaa zao. Ni matatizo makubwa sana ambayo huwakumba watu hawa. Kwanza hawa ni wafugaji wa chaza sasa hizi chaza huwa zinatoa lulu na lulu zile huwa zinafanyiwa vitu kadhaa kama vile hereni, bangili, pete na kila kitu. Kwa hiyo, wanakuwa na matatizo yao ya kuwa hawana soko la kwenda kuuzia hivyo vitu. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie suala hili la kinamama kuwapatia soko la kuuzia bidhaa zao.

Mhe. Spika, nikija katika kilimo cha mwani; wananchi wengi wa Pemba wanajishughulisha na kilimo cha mwani, lakini bado wakulima hawa wana matatizo mengi sana kama vile vifaa vya taitai na kamba za kufungia mwani, hata usafiri wa chombo cha kuchukulia mwani pale wanapovua pia ni tatizo. Lakini niseme kwamba hata bei bado inakuwa ni ndogo kutokana na bidhaa hii na kamba wanazonunua ni ghali na bei ya mwani nayo ni ndogo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili la kinamama kuwaongezea pesa wananchi hawa ili waweze kuzalisha vizuri.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ahsante.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuvuta pumzi zake na kufika katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na mwenyekiti, hotuba ambazo zina mambo mengi sana. Lazima tukiri kwamba hili suala ni letu lakini haya yote yanatokana na umasikini wa bajeti na umasikini wa uchumi wetu. Kwa sababu hawa wenzetu uwezo wanao watendaji wote pamoja na Katibu Mkuu na wakurugenzi wote, naamini uwezo wa kufanya kazi wanao. Lakini mara nyingi panapokuwa na bajeti kama hizi wakati mwengine inakuwa haitekelezeki kutokana na ruzuku wanazozipata. Humu muna vitu vingi lakini vyote vinahitaji vitendea kazi, ukisema uvuvi haramu namna ya kuulinda baharini mwetu lazima tuwe na maboti ya kisasa, ukienda katika utekelezaji mwengine wa kushughulikia nako vile vile.

Mhe. Spika, kwanza nawaunga mkono sina matatizo nayo bajeti hii, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini kwa asilimia zaidi ya mia moja. Ningeliomba wenzangu kwa sababu ni vijana wenzangu wawe na hekima, busara na usikivu wakati anapokuja waziri ku-*wind up*. Kwa sababu hili Baraza ni la wananchi na hapa hatuko skuli kwa sababu ukiwa skuli mwanafunzi anapewa karatasi anaweza kuandika tu *yes*, *no*, *yes*, *no*, ndio skuli; lakini hili ni Baraza la wananchi.

Sasa naomba wenzangu katika kuja kuweka sawa majibu basi busara zitumike sana kwa sababu mimi nakiri bajeti hii vifaa vyao kama maboti, bajeti yenyewe, ruzuku wakati mwengine huchelewa. Sasa nikitaka wawe wakweli pahala ambapo hapafanyiki jambo katika kuelezea jinsi gani ya kuweza kushirikiana. Mimi niungane na wenzangu kwamba nawapongeza, bajeti hii na nawaomba watendaji wote wa wizara hii wawe waangalifu kwa maslahi ya wananchi na kwa wavuvi wetu pamoja na mifugo.

Mhe. Spika, hawa wenzetu wa mifugo na uvuvi wanataka elimu, wanataka wabadilike na kama wanataka kubadilika lazima kuwe na utaratibu nzuri wa kukaa kwa pamoja na kufanya mashirikiano, ndiko tulikotokea sisi. Mimi mmoja wapo ndiko nilikoanzia kule, kwa hivyo ni vizuri tukawapa vitu vya kuwawezesha, kuwaelimisha, kusaidia mifugo yao. Natoa wito kwa wenzangu kwamba tuwe na utamaduni sasa kila mwenye kuchukua jukumu basi angalau kufika katika sehemu mbali mbali kuona jinsi gani hali ilivyo, kuliko mtu kuambiwa kwamba skuli hii ina tatizo wakati hata siku moja hajafika na akaja akatoa jawabu wakati.

Sasa ningeliomba wahusika kwamba kila wanapotaka kutoa maelezo wajaribu kufika katika maeneo yale na kuona.

Mhe. Spika, mimi naomba kwa heshima zote tubadilikeni mambo haya yetu sisi na pahala palipokuwa na matatizo wenzangu wahusika waliochukua dhamana ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa wafike katika maeneo yao hata kama Bara. Kwa sababu kumekuwa na utamaduni, isiwe tumemaliza Baraza watu wakafika pwaaa! Maana yake ndio tushapumzika. Ni vitu vya kufuatilia mtu kaona kuna tatizo basi afike kwenye eneo lile ambalo hajafika akalione na ajue kilichozungumzwa, kilichopigwa buti na wawakilishi kweli walipiga buti kwa maana yao.

Mhe. Spika, mimi nimalizie hayo ahsante sana naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango au maoni yangu katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.
Pili, napenda nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru yeye mwenyewe Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwasaidia wananchi katika maendeleo yao.

Baada ya hapo mimi nataka niseme tu kwamba, sisi Wazanzibari tulioko katika nchi hii sote kwa jumla tutakuwa lazima tuna sehemu maalum ambayo tunaitegemea. Kwa hivyo, kwa watu wa nchi hii ya Unguja na Pemba tegemeo letu zaidi au kubwa kabisa ni kilimo pamoja na mifugo na uvuvi wetu wa bahari ambao imetuzunguka.

Kilimo kama kawaida kinaendelea na jumla ya watu wetu asilimia 80 shughuli zao nyingi zinakwenda katika kilimo, lakini utakuta kilimo na uvuvi kina mnasaba mkubwa sana. Kwa sababu yule yule mkulima baada ya kulima asubuhi na mapema wakati fulani ndio anaondoka kwenda katika shughuli zake za uvuvi; hivyo kuna maingiliano makubwa katika shughuli zetu za kawaida za kila siku, hivyo tutajikuta kwamba tunafanya kazi mbili kwa wakati mmoja; tunafanya kazi ya kilimo lakini pia tunafanya kazi ya uvuvi.

Kwa hivyo, ni lazima sisi tujisifu kwa sababu sisi ni watu wa visiwa tumezungukwa na bahari na hatuna budi kuitumilia bahari ambayo sisi imetuzunguka. Tukiizungumza hii sekta ya uvuvi inavyoonesha kiuhalisia ni kwamba siku hadi siku idadi ya wavuvi inaongezeka kwa sababu watu wa nchi hii hawana kazi nyengine zaidi ya kulima na kuvua, kilichobakia ni kazi za biashara au ni huduma tu za ndani ya nchi yetu, lakini kazi kubwa itakuwa ni kilimo na uvuvi. Kwa hivyo, ongezeko lazima litakuwa kubwa kwa wavuvi wetu na hii inawafanya watu waingie katika kazi hii kwa sababu wanatafuta *self employment,* ajira katika serikali hazipo.

Kwa hivyo, wananchi wanaona bora waingie katika kazi ya uvuvi *tabaan* idadi ya watu kila siku itakuwa inaongezeka na hivyo uzalishaji wa samaki utakuwa unaongezeka, pato la mwananchi linapatikana na pato la taifa linapatikana.

Mhe. Spika, inavyoonesha hapa kwamba pato la taifa linaongezeka, lakini ili kulifanya pato hili la taifa liongezeke kwa kiwango kikubwa, hatuna budi katika wizara yetu hii ya Mifugo na Uvuvi ni lazima tuongeze mahitaji.

Mahitaji ni kitu cha lazima kwa sababu watu wetu asilimia kubwa 80 au 90 ni wavuvi, wakulima na wafugaji sasa ni lazima serikali ishughulikie, ijikite zaidi kwa wananchi. Kwa sababu serikali haiwezi kuwapa watu wote ajira lakini watu wanatafuta ajira zao wenyewe kila mtu anajiajiri mwenyewe. Kwa hivyo, ikiwa sehemu kubwa ya watu wetu wanajiajiri wenyewe basi hapana budi serikali iwashughulikie hawa wananchi kwa kuwapa mahitaji yao na mahitaji makubwa katika uvuvi ni kuweza kupatiwa nyezo za kufanyia kazi.

Mhe. Spika, katika hili la uvuvi wetu utakuta tunafanya kazi ya uvuvi katika maji haba na tunatakiwa tufanye uvuvi katika maji makubwa. Lakini kwa sababu ya kuwa sisi uwezo wetu ni mdogo hatuwezi kufanya uvuvi katika bahari kuu, inabidi sasa uvuvi wetu uwe wa kurambazarambaza tu pwani pwani kwenye *shallow water*, hatuwezi kwenda kwenye *deep sea,* kwa sababu hatuna uwezo wa kufika huko. Kufika kwenye bahari kubwa yenye kina kikubwa cha maji ni lazima tuweze kupata vyombo vya kuweza kustahamili bahari kubwa. Kwa hivyo, hapa serikali iangalie aina mbili za watu wanohitaji kusaidiwa. Wale ambao uwezo wao ni mdogo ni lazima wasaidiwe kwa hali zozote kutokana na kwa sababu uwezo wao ni mdogo, hawana uwezo wa kwenda kuvua katika bahari kubwa.

Sasa tuangalie hawa wakiwa bahari ambayo wanavua maji madogo mahitaji yao makubwa ni nyavu. Hapa pamejitokeza uvuvi haramu, kwa nini watu wanafanya uvuvi haramu. Uvuvi haramu unafanyika kwa sababu uwezo wa kununua nyavu ambazo za kwenda bahari kuu hawana. Kwa hivyo, ikiwa hawana uwezo wa kwenda bahari kubwa ni lazima watanunua nyavu ndogo na hii imeshajitokeza mara nyingi. Huu uvuvi haramu maana yake ni kutumia nyavu zenye macho madogo na hapa hatimae unaua wale samaki wadogo wadogo ambao ni mategemeo ya samaki wa baadae.

Kwa hivyo, wizara inajitahidi katika kuwaelimisha watu na inajaribu kunyang'anya zile nyavu zenye macho madogo. Mhe. Spika, ningemuomba Waziri hali ya wananchi wetu unawafahamu kwa nini wananunua nyavu

ndogo, kwa sababu ni rahisi zaidi kuzinunua. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba katika suala hili la wavuvi wetu uwasaidie.

Mhe. Spika, kama tunataka kuongeza pato la taifa na pato la mtu mmoja mmoja katika uvuvi wa bahari kuu hapa ni lazima Serikali ijikite sana katika kuwasaidia wananchi wake. Mimi naamini kwamba haina uwezo labda wa kuwasaidia watu kuleta vyombo vikubwa. Sasa tuangalie nchi nyengine zinavofaidika katika bahari zao, sisi uchumi tunao lakini tumeukalia. Kwa sababu tuna mambo mawili, uchumi katika bahari kuu huo ni mmoja ambao unaweza kutupatia, na uchumi wa pili wa mafuta tunayo ndani ya bahari tumeyakalia. Chumi zote mbili tunazo, tangu tulipoanza kuzungumza mafuta katika ardhi mpaka leo kimya hapajazungumzwa chochote.

Tuna masamaki ambayo sasa hivi wana umri mkubwa bado mpaka leo wameshindikana kuvuliwa. Serikali haina uwezo wa kuwawezesha watu wetu kwenda kuvua bahari kuu. Serikali haijawa na uwezo wa kuonesha fikra ya kuchimba mafuta.

Mhe. Spika, kama yote hayo hatuwezi basi tutafute wawekezaji waje wawekeze katika bahari kuu, wavue wao wapate na sisi tupate, hiyo ndio hali, nusu kwa nusu. Wao wanavua wanapata mtaji, wanapata pesa za kigeni na sisi tutapata pesa za madafu tutatumia. Hatutaki pesa za kigeni sisi hapa, Serikali ndio inataka pesa za kigeni kununua malighafi nje. Mimi nahisi kwamba Serikali zaidi ijikite kama kweli tunataka kuimarisha uvuvi Zanzibar, itafute wawekezaji sisi hatuna uwezo wa kuvua bahari kuu. Mhe. Spika, nasema hilo ni jambo zuri na liendelezwe ili kuongeza pato la taifa.

Mhe. Spika, hata hivyo ninachotaka kusema suala hili uwekezaji ni mgumu sana, kwa hivyo watu wetu wasaidiwe. Watu wetu wanakuwa wana shida kubwa sana kwa sababu gharama zile za kufanyia shughuli hizi ni kubwa sana.

Jambo la pili ni uhaba wa taaluma ya watu wetu. Hawana taaluma nzuri, kwani kila kitu ni lazima ujifundishe au ufundishwe. Huwezi tu kuwa fundi mzuri ukasema wewe fundi unajenga vipimo vyako vizuri, kazi zako ni nzuri, hivi vitu kwa kuwa wewe uliokotea ufundi ule. Maana upo ufundi wa kuokotea unamwona fundi anakamata kijiko na wewe unakamata kijiko, lakini si wa kitaalam anaweza akajenga pengine ukuta ukakaa upande, plasta haitokuwa nzuri. Anajua kujenga lakini si fundi, si mtaalam.

Kwa hivyo na yeye huyo anaweza kuwa ni mvuvi lakini haelewi mazingira ya kibahari. Lakini kwa sababu anatafuta maisha basi atakwenda. Kwa hivyo, nafikiri hii taaluma ni suala la msingi sana na nyenzo za kufanyia kazi waweze kusaidiwa.

Jengine ambalo nililokuwa nimejifunza hapa ni kwamba hii Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi ina upungufu wa wafanyakazi. Nilivyosema kwamba wizara hii sasa hivi shughuli zake zimekuwa kubwa sana imetanuka na kila kitu kikiwa katika hali ya kupanuka namna hiyo ni lazima mahitaji yataongezeka. Kwa hivyo, tuna upungufu mkubwa sana wa watendaji katika wizara hii. Tunahitaji watu madhubuti ambao wataweza kufanya utafiti wa masuala yetu ya uvuvi ya bahari ya maji haba na bahari kubwa. Tunahitaji tupate watafiti, watu wa takwimu.

Siku zote nalisemea suala hili la takwimu *(database)*, hili ni suala muhimu sana ni lazima lipatikane kila wizara iwe na takwimu zake. Kwa hivyo, ni lazima tupate watu ambao wa kuweza kutoa takwimu zilizokuwa sahihi kabisa. Halafu tuweze kutoa elimu kwa ajili ya hawa wavuvi wetu. Hilo ni jambo la busara, ni jambo zuri, kwa sababu tunahitaji uvuvi uwe ni uvuvi endelevu kila siku.

Pamoja na hayo yote, ni lazima tunahitaji tupate madaktari. Madaktari ni watu muhimu na umuhimu wake upo katika namna mbili. Katika kufuatilia kazi zao kuona hali halisi ya kazi zinavyokwenda. Lakini la pili madaktari kuweza kuwachunguza wanyama wetu wakati tunapokula ile *red meat*, ingawa tunakatazwa sana tusile *red meat* kwa matatizo yake. Tunatakiwa tule *white chicken,* hii *red meat* ina matatizo yake kwa afya ya binadamu. Lakini kwa sababu ng'ombe tunao tutawala, tunaletewa tutakula. Lakini hasa tunatakiwa tule *white chicken* hivi vikuku vidogo vidogo havina matatizo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, madaktari hawa tunao ni muhimu sana kuweza kuzichunguza hizi nyama kwa sababu huyu ng'ombe ana matumizi ya ardhini kama binadamu, anakula majani yaliyopo katika maeneo yetu, haya yanapata *infection* ya namna kwa namna, yanaathirika kwa mambo kadhaa wa kadhaa. Anapokula yale majani anapotia katika mwili wake yeye anapata hasara na sisi tunapata hasara kwa kuila ile nyama yake. Kwa hivyo, mimi ningesema tu

kwamba hii wizara inahitaji kuwa na madaktari wengi sana waweze kusambazwa kila pahala, ili wakati ng'ombe hawa wakishachinjwa waweze kuchunguzwa maradhi, kwa sababu ngombe wana maradhi mengi. Hii *red meat* mbaya, ina hatari kwa hivyo ichunguzwe sana kabla hatujaila, itatuletea maradhi chungu nzima.

Mhe. Spika, hii tunasema watu wengi nawaambia mimi hapa, hawa watu wanaopenda kula hii mishkaki, sisi tunasema *any half cooked meat is dangerous*. Watu wanakwenda kula mishkaki pale haijaiva wanakula matokeo yake ile si wanatafuta *hook worms*. Kwa hivyo, ng'ombe wakati wowote ana matatizo, lazima uhakikishe nyama yake imeiva kwa *high temperature*, vyenginevyo inaweza kutuathiri.

Kwa hivyo, hapa ndio inatakiwa lazima tuwe na madaktari maeneo yote, wanapochinjwa ng'ombe wetu madaktari wawepo kuangalia athari zilizomo kwenye maini wayachunguze vizuri, zipo sehemu *cells* zile wazichunguze vizuri ndio kwenye maradhi waangalie. Sasa madaktari wetu mtu anakaa huko anamwambia haya endelea mimi niletee kilo yangu moja ya maini biashara imekwisha. Mbaya hii *business as usual*, itatupeleka pabaya. Kwa hivyo, hapa mimi naomba hii wizara iwe na madaktari wengi.

Mhe. Spika, kwa kweli ng'ombe tunao, mbuzi tunao na kuku tunao, mimi nataka kumalizia hapa katika suala la kuku. Mhe. Spika, ufugaji ni moja katika maendeleo ya watu wetu, kila mmoja anataka kufuga. Lakini kuna mambo mazito kidogo ni lazima watu wetu wa ufugaji wapatiwe *incubators* kwa ajili ya kuzalisha *chicken* wale wadogo wadogo. Tunaambiwa tule *white chicken.* Kwa hivyo, hii wizara naiambia ifanye jitihada ya kuwawezesha hawa wafugaji ili tule kuku kwa wingi, tusile *red meat.*

Sasa mimi nataka nitoe mfano tu wa hivi karibuni. Tulizungumza hapa tukasema kwanza yalikuja matatizo kwamba sisi tunaagizia kuku kutoka Brazil, makuku yenyewe hayana *taste*, hayana chochote yameshakaa ndani ya barafu muda mrefu na tunakula hivyo hivyo. Kwa sababu ni rahisi tunawala, haidhuru. Lakini nasema tunahitaji tutengeneze kuku wetu sisi wenyewe. Tukasema kwa sababu tunayo mahoteli mengi sana Zanzibar, *along the coast* wote yamejaa mahoteli. Wana mahitaji ya kutafuta mayai, kuku, lakini kuku hawapatikani, mayai hayapatikani. Mimi ninachokiona hii takwimu ya mayai si yetu. Hii takwimu inatoka huko ikaingizwa humu ndani. Mhe. Spika, hapa bado uzalishaji ni mdogo sana.

Sasa mimi nauliza, hii wizara itawasaidia kiasi gani hawa wafugaji ili tupunguze ile idadi ya tani za kuku tunazoagizia kutoka Brazil kuja Zanzibar. Makuku yenyewe hayana ladha yoyote lakini tunayala. Kwa sababu ukenda marikiti kuku kama yule ni shilingi elfu kumi na mbili mpaka elfu kumi, lakini yule hafiki elfu nane, elfu tano unapata. Bado ukenda marikiti kule limetiwa masalo limeivishwa pale utasema hili kuku... Lile sio kuku pale unajitia mashaka tu ya bure. Mhe. Spika, hapa nakumbushia hao wafugaji wetu tuliosema wawezeshwe.

Mhe. Spika, mimi nilisema dagaa tunalo kwa wingi, tunaweza kufanya mahindi, kunde tunazo tunaweza tukasaga hapa wenyewe kwa wingi tukachanganya. Ukishatia dagaa pale ukampa kuku kesho atazalisha mayai mengi. Sasa haya mambo tangu tulipozungumza mpaka leo Mhe. Waziri amechukua hatua gani kuwezeshwa hawa wafugaji wetu ili waweze kutoa mayai kwa wingi na kuuza kuku kwa hao watalii. Watalii sasa hawachukui vitu hapa.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu. Naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana tumepokea wasia wako kuhusu kupunguza kula nyama nyekundu. Tutajitahidi tule nyama nyeupe. Kwa hivyo, tumesikia wasia wako.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, ingawa muda umekwisha lakini nitazungumza haraka haraka kuweza kuichangia bajeti hii wakati mimi mwenyewe nimo katika Kamati hii.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 5 kifungu cha 2 kuhusu Sekta ya Uvuvi. Mhe. Spika, ni muda mrefu sana tuna matatizo kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Wananchi wetu kwa kipindi kirefu wanapata matatizo ya kushikwa katika uvuvi wa bahari ndogo ndogo na nyavu wanazozitumia ni ndogo ndogo, kutokana na kwamba hawana usafiri wa kuweza kufika katika bahari kuu.

Mhe. Spika, hivi sasa Mhe. Waziri anawaumiza sana wananchi wetu kwa sababu hawana vyombo vya kuweza kufika bahari kuu ili kuvua samaki wale wanaotakikana. Kwa hivi sasa wanavua maji madogo na ndio sababu ya kuwa na nyavu ndogo ndogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa sasa labda awaachie wananchi wakati hana uwezo wa kuwapa mashine ama vyombo vya kufika katika bahari kuu, hadi hapo atakapokuwa na uwezo wa kuwapa vyombo vya kwenda kwenye bahari kuu ili kujipatia maslahi ya uvuvi unaotakiwa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri akija kujumuisha naomba anipe maelezo ni lini atahakikisha kwamba wananchi wetu ameweza kuwapatia vyombo vya kuweza kufika kuvua katika bahari kuu.

Mhe. Spika, naomba nichangie zaidi kifungu cha 27 kuhusu ukatili wa wanyama. Mhe. Spika, hivi sasa kuna baadhi ya wananchi wanafuga wanyama kwa hiari zao lakini wanawadhalilisha katika maisha yao. Sijui kwa sababu ni wanyama ama vipi. Utakuta mwananchi anafuga ng'ombe, ng'ombe kawaida yake kuliwa nyama. Lakini utakuta mwananchi yule ng'ombe huyo anamtumia kwa kubeba mizigo, halafu anachukua rungu kubwa sana anampiga nalo na wakati ng'ombe yule ana mzigo mkubwa sana. Kwa kweli sijui Mhe. Waziri wakati ndie Waziri wa Mifugo na Uvuvi anachukua hatua gani kwa wananchi kama hao ambao wanawadhalilisha wanyama na sio kazi yao kuchukua mizigo.

Mhe. Spika, kuna matatizo mengi ya wananchi wetu ambao hivi sasa wanaitumia bahari hasa kwa mambo ya kilimo, kwa mfano mwani. Utakuta wananchi hao wanafanya kazi kubwa, nzito, lakini wanadhalilika sana kutokana na bei ya mwani. Namuomba Mhe. Waziri anihakikishie ni lini atapandisha bei ya mwani kwa wananchi wetu hasa akinamama ambao ndio shughuli zao kubwa.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri hii kazi ni ngumu kwake, Wawakilishi wa majimbo tupo na tunaona wananchi wetu tunaona jinsi wanavyoumia, atupe nafasi hii kwenda huko nje ya nchi kuwatafutia bei ambayo inaendana na wakati, na sio bei ya shilingi mia tano kwa kilo ya mwani mkavu. Hio bei inadhalilisha sana wananchi wetu, wanaumia sana, wanazeeka kabla ya wakati, wengine wanafariki.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wanaonunua mwani wanawadhalilisha wananchi na wanaficha bei ya ukweli inayokuwa huko nje. Duniani kwa kweli mwani unafanyiwa mengi sana; mwani ndio dawa, mwani ni sabuni, mwani ni kila kitu, hata supu ya kunywa binadamu ni nzuri. Haiwezekani kilo nzima ikauzwa kwa shilingi mia tano. Hilo naona tunafichwa na Mhe. Waziri sijui kama na yeye hana kipato ambacho anachukua kutoka kwa wanunuzi wa mwani.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atoe nafasi hasa kwa sisi wenye kamati hii kwenda nje ya nchi kuhakikisha kwamba mwani unauzwa bei gani nchi za nje. Mhe. Waziri mwaka huu wa fedha utenge fedha maalum za Wawakilishi wa Majimbo kwenda nje na kuileta bei ya mwani katika majimbo yetu na wananchi wafaidike na maisha ambayo tunayapata sisi Wawakilishi wao.

Mhe. Spika, sijamuona mkulima wa mwani hata mmoja akavaa suti wakati wa kwenda kuchukua mwani. Lakini Waziri namuona anavaa suti kwa ajili ya wananchi ambao wamekwenda kuchukua mwani. Nataka Mhe. Waziri anihakikishie hilo analichukulia hatua gani na anapokuja anijibu lini bei ya mwani itapanda, ama lini Wawakilishi wa Majimbo tutakwenda nje kutafuta bei ya mwani ya uhakika kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, najali muda wako na muda umekwisha. Kwa hayo machache naomba Mhe. Waziri anihakikishie mambo muhimu hayo kuanzia vyombo vya bahari kuu pamoja na mwani, wananchi wetu wafaidike hasa wa Jimbo la Koani. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mussa Ali Hassan kwa kutumia muda mfupi lakini kwa maelezo mazuri ya kutosha. Waheshimiwa Wajumbe, jioni tutaendelea kwa kuanza kumsikiliza Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Saleh Nassor Juma, pamoja na Mhe. Salim Abdalla Hamad. Bila ya kumsahau Mhe. Salma Mussa Bilal. Kwa hivyo, tufike mapema ili tuendelee na shughuli yetu kama kawaida. Tusitishe shughuli hadi saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yaendelee ingawaje ndio Wajumbe wanaingia ingia, walioko nje wajitahidi kuingia upesi ili shughuli hizi zisikwame, ziendelee kama zilivyopangwa.

Mhe. Ali Mzee Ali anaongoza pale, wanaingia kwa kasi. Majadiliano yanaendelea na kwa jioni hii nitangulie kumualika Mhe. Ashura Sharif Ali achangie wakati Mhe. Mohammed Haji Khalid anajitayarisha na Mhe. Salim Abdalla Hamad naye anajitayarisha.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante sana. Awali ya yote sinabudi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetulijaalia uhai lakini pia akatupa na uzima, akatuwezesha kuwemo humu kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kutoa mchango wangu katika mada iliopo mezani wakati huu.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake lakini pia niwapongeze watendaji wake.

Mhe. Spika, nianze na utangulizi wangu kwa kusema kwamba nchi yetu ni kisiwa na kwa kweli imezungukwa na bahari ambayo ni moja katika neema ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia katika taifa letu. Wengi wa watu wake ni wavuvi, wafugaji na wakulima. Hivyo wizara hii ni wizara ambayo kwa kweli inabeba jukumu la kujenga afya ya jamii ya Wazanzibari. Tunazunguka kwingi lakini hatimae ukitaka kujenga afya ya jamii ya Wazanzibari waiguse sekta hii ya uvuvi na mifugo kwa ajili ya kukamilisha afya na kujenga miili na kupata wananchi wenye afya imara kwa ajili ya kulijenga taifa lao.

Baada ya utangulizi huo, niseme kwamba Mwenyezi Mungu ametujaalia hiyo raslimali bahari lakini pia akatupa na raslimali watu. Viwili hivyo Mwenyezi Mungu ametupa bahari na watu, lakini kwa kweli tumekosa niseme labda miundombinu ya kufikika hiyo bahari na kutumika hasa ipasavyo kwa maslahi ya Wazanzibari na kwa maslahi ya mzunguko wa taifa letu katika njia za kiuchumi.

Mhe. Spika, mimi wizara hii ningeambiwa nitoe jina, ningeiita ni Wizara ya Kitoweo. Kwa sababu kila utakapozunguka na kuiangalia mifugo na uvuvi, mzunguko wake mkubwa hasa basi unaukuta kwamba ni mambo hayo zaidi kwa upande wetu. Maana raslimali ya mafuta na gesi kwa wakati huu imekuwa ngumu kuweza kuelezeka kwamba ipo au laa.

Mhe. Spika, nitoe mchango wangu kwa masikitiko kidogo. Mimi niseme nilikuwa ninatamani wakati nikiwa ninachangia serikali yote iwepo mbele kuweza kusikiliza labda ni michango gani tunaitoa kwa serikali, ili tuweze kufikia malengo ya kufanikisha maendeleo ya taifa letu, lakini pia kuongeza kipato kwa watu wetu na kupunguza umaskini.

Serikali kwa bahati mbaya sana sekta hii bado hawajaipa nafasi inayostahiki. Hili linanithibitishia katika kiambatanisho Nambari 52 na 53, kinachoonesha namna ya upatikanaji wa fedha za maendeleo katika kitabu hiki. Mhe. Spika, ukiangalia hiki kiambatanisho kinasema kwamba katika kazi za maendeleo, fedha za maendeleo hizi zinasema kwamba kuna mradi huu wa kuimarisha uvuvi wa bahari kuu, maendeleo ya uvuvi haya.

Mradi kwa makadirio ya mwaka 2013/2014, ulitengewa shilingi milioni 100 lakini fedha zilizopatikana katika mradi huu ni shilingi milioni 1,660,000. Ukiwa utakuwa unaangalia na jinsi ya jina lilivyotajwa na kuitwa, ukiangalia hiyo fedha iliyopatikana, halafu ukijumulisha kwa pamoja fedha za serikali pamoja na za wahisani ni asilimia 30. Asilimia 30 ukitaka kuniambia ili mradi wetu ukamilike kwa mwaka mmoja, maana yake miaka mitatu labda na miezi minne ndio utaweza kupata ile fedha ya mwaka huu mmoja. Hiyo inaonesha dhahiri kwamba serikali katika jambo hili haijawa tayari. Mimi nilizungumza sana wakati wa bajeti ya serikali nikiwaambiwa kwamba umefika wakati wa kupanga mipango yetu ya maendeleo kupitia miradi ya serikali, lakini ile ambayo imechaguliwa iwe ni yenye kutekelezeka.

Mradi huu ambao umekusudiwa umepewa asilimia 2 ya fedha. Ni kusema kwamba hiyo asilimia 100 iliyoekwa ni miaka mitatu kuingia wa nne ndio inawezekana kwamba mradi huo ukapata asilimia 100 ya mwaka mmoja ambao kwa humu umeekwa ndio kigezo. Hili ni tatizo. Ni kusema kwamba hatuwezi kufikia tunakokusudia. Fedha zote kabisa za serikali na washirika wa maendeleo katika fedha ambazo zilikusudiwa basi kilichopatikana kwa kweli hata robo hakikutimia. Ni jambo la kusikitisha sana.

Mhe. Spika, kusithibitisha hayo ni kusema kwamba kuna mradi wa kuimarisha ufugaji wa samaki. Nagusia uvuvi makusudi ili nioneshe kwamba kama serikali ingelijipanga ikaaamua inakusudia kweli kufikia maendeleo hayo, basi ingelichagua ni mradi gani kwa idadi ya fedha tulizonazo unaweza ukatekelezeka na ukakamilika katika muda muafaka, kwa kupatikana fedha ambazo zimekusudiwa kwa ajili ya mradi huo.

Katika mradi huu, nao ulitengewa shilingi milioni mia moja. Kwa bahati mbaya sana hakuna kilichopatikana na mradi huu umeingizwa tena na mradi wa kuimarisha tena uvuvi wa bahari kuu nao umeingizwa. Nikusema kwamba, siku moja nilimsikia Waziri wa Fedha akisema kuwa kupanga ni kuchagua. Tuchague basi katika mambo mawili lakini almuradi liweze kutekelezeka kwa ufanisi kabisa.

Nilisema si aibu lakini tutakukwa tumejipanga na kuweza kufikia kile ambacho tunapanga kinatekelezeka na kinaonekana na tunaepukana na yale mambo ya kuleta hesabu za mdomo au hadithi za Alinacha. Kwa sababu nimeona kwamba kuna miradi mingi ambayo imepangwa lakini miradi hii yote ina sufuri sufuri. Kwa hivyo sidhani kwamba tunaweza tukaiboresha sekta hii kama hatukua na nia ya kweli. Tunajua wananchi wetu na raslimali bahari tunayo na watu wengi wanapata pato lao kupitia ile bahari.

Ni vyema tungeangalia uvuvi wa bahari kuu sasa limekuwa tatizo. Ni kweli kabisa unahitaji gharama na nyenzo zake ni kubwa na ngumu kufikia kwa urahisi. Hebu tungefanya jambo ambalo linafikika, tungekuwa tumeamua kweli. Tungeangalia zaidi namna ya ufugaji wa samaki ambao pengine kwa gharama zake unaweza ukafikika kwa urahisi zaidi na wananchi wetu wanaweza kuutekeleza pale ambapo watapatiwa taaluma na kufuatiliwa na kupewa nyenzo, ili kuona kwamba wanaweza kuzalisha.

Kwa sababu mzunguko wa uvuvi wa karibu, sasa imekuwa ni tatizo samaki hawapatikani. Lakini pia bahari kuu hatuwezi kufika huko kwa sababu ukitaka kuvua uvuvi wa bahari kuu, lazima uwe na nyenzo. Nyenzo imekuwa ni tatizo. Ni vyema tukaangalia hilo, tukaliona kwamba hii imekuwa ni ya kutisha, haipendezi na kwa kweli haipo vizuri.

Mhe. Spika, nikiendelea niseme kwamba kuna mradi mwengine huu; ninaitaja miradi, huu ni mradi wa kuimarisha miundombinu mifugo. Mradi huu Mhe. Spika, umeanza mwaka 2011/2012 na unatarajiwa kumalizika 2014/2015, ambapo kimsingi umepangiwa bilioni saba na milioni mia mbili.

Mhe. Waziri mradi huu ni matarajio yangu kwamba katika awamu hii utakuwa unamalizika. Mwaka uliokwisha ulidai milioni mia mbili na mwaka huu umeweka milioni thamanini. Ningependa kuelewa kwamba, je, hizo fedha za nyuma zote zimeweza kupatikana na je, umepata ufanisi gani katika mradi huu.

Jengine Mhe. Spika, katika mradi huu huu, mulijiwekea malengo. Lakini tukumbuke kwamba kuna na utekelezaji halisi. Utekelezaji halisi mumezungumzia hapa katika kitabu kwamba huku mutajenga josho kwenye Kijiji cha Mjimbini, Mkoani Pemba. Lakini utekelezaji halisi mumesema mumefanya matayarisho ya awali ya ujenzi wa josho hilo, yamefanyika ikiwemo shughuli ya kusafisha eneo la ujenzi na kuchora ramani.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha, mradi huo umejirudia lakini kilichokuwa kimenishangaza, kule mumesema kwamba huo mradi upo na mumeanza na hili. Lakini huku katika utekelezaji malengo yenu ya 2014/2015, munasema kwamba ni kumaliza ujenzi wa josho la ng'ombe Mjimbini. Huku hamjaanza mumesafisha kiwanja tu, huku munasema munamalizia. Sasa mimi ninataka nijue mnajenga au munamalizia. Maana ninaona hizi kauli zenu humu humu za kiuandishi zinajifunga kidogo. Ningeomba kulielewa hilo. Kwa hivyo, ukisema unajenga na unamaliza na huku unaonesha kitu chengine inakuwa kidogo si vitu vizuri.

Mhe. Spika, kimtazamo inaonesha kwamba tangu zamani, ninarudi tena kwenye sekta ile ile ya uvuvi. Tangu zamani wazee wetu uvuvi ni asili zetu, watu wetu wakivua kwa mitumbwi na vidau. Ndivyo walivyokuwa na kwa

kweli walikuwa wakikidhi shida na mahitaji yao na wakiweza kuendesha maisha yao. Leo tumeendelea na ndivyo inavyokuwa...

Mhe. Spika: Dakika 5 mheshimiwa.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante. Ndivyo ilivyo kwamba jambo hili kwa kweli sasa kumeekwa vikwazo kwamba kuna uvuvi haramu. Sasa mtu ukimwambia hiki haramu basi umpe mbinu za kuona kwamba anafikia kile halali. Sasa haya hayajapatikana ni kuwapa kero wavuvi wetu. Kwa hivyo ni vyema serikali inapoandaa mipango yake basi ielekeze njia na nyenzo za kufikia huko, ili kuepukana wananchi kuwaondoshea hii kudhia inawakabili.

Jengine Mhe. Spika, ni kusema kwamba Mhe. Waziri kuna kudhia kidogo katika eneo la Nyanjale juu ya wavuvi na waanikaji dagaa. Watu hawa kwa sasa kumeingia mradi wa mpira wa gofu ambao unaowafanya wao kuwa katika kizaazaa cha kutojua nini cha kufanya kwa wakati huu. Eneo lao ndilo wanalolitumia kwa kuanika dagaa lakini wavuvi pia, bandari hiyo huitumia.

Mhe. Waziri nikuombe, hapa uwatembelee hawa watu uwaone, mushauriane, wana nafasi nzuri ili na wao waweze kuingia katika hiyo miradi ambayo inawezekana sana ya ufugaji wa samaki na wao wakanufaika na wakaweza kukidhi shida zao na wakaweza kujipatia mahitaji yao.

Pia Mhe. Spika, niende katika mifugo sasa. Niseme kwamba sekta hii nayo kwa kweli ni sekta muhimu sana kabisa. Tatizo ambalo linaikumbuka sekta hii kwanza ni kukosekana kwa wataalamu wa kutosha, lakini pia kuna wataalamu wale ambao walifanya kazi kwa muda mrefu madaktari wetu. Lakini cha kusikitisha kabisa wataalamu hawa kwa kweli wanadharauliwa kimaslahi yao na mishahara yao.

Hata ukimleta mtu wa *PhD* na *degree*, mara nyingi katika utendaji wa kazi huwategemea sana wale wafanyakazi wa mwanzo ambao waliianzisha shughuli ile. Sasa naomba uniambie unawashirikisha vipi watu hawa na kuona kwamba na wao mbali na ile iliyotengenezwa *scheme of service*, lakini wao kutokana na uzoefu wao wa kazi kwa muda mrefu ambao wanaisaidia jamii katika mikoa mbali mbali, madaktari wamo wengine wamepatikana lakini watu huwatumia wale kwa uzoefu wao na ujuzi wao ambao wao hutumia zaidi ule uzoefu, na kwa kweli huweza kunawirisha sana mifugo na kuweza kutabiri mambo mbali mbali ambayo mifugo huikumba katika nchi yetu. Je, munawatumia vipi hawa munapoandaa mipango ya maendeleo katika sekta ya mifugo?

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nisema kwamba na mimi nitaunga mkono hotuba hii baada ya kupata maelezo kidogo juu ya hawa wafanyakazi, lakini pia kadhia iliyowakuta watu wa Nyanjale, ili kuwaona kwamba na wao kwa wakati huu watapata namna, ya kuweza kuboresha maisha yao. Kwa kuwa wizara hii ndio inayohusika na hali hiyo na wao ni miongoni mwa wavuvi waanika madagaa, tena wengi wao ni wanawake.

Nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa uniambie utawatembelea lini na wao ili ukaone eneo hasa husika, ili na wao uwashauri na uwasaidie katika sekta ya ufugaji wa samaki.

Mhe. Spika, kuna kitu kidogo cha kumalizia kwamba wamesema moja ya tatizo ambalo linaikumba sekta ya uvuvi kwa wakati huu ni kuona kwamba yale mazalio ya samaki yameharibiwa sana kutokana na tabianchi. Lakini pia walisema ukataji ovyo wa mikoko. Jambo hili kwa kweli wakati huu limekuwa kweli ni tatizo ambapo anapoingia mwekezaji huruhusiwa kufanya analotaka na sheria kwake huwa haifuatwi.

Mhe. Spika, Nyanjale ni moja kati ya eneo moja zuri ambalo lilikuwa na mikoko ya kutosha. Lakini mikoko hiyo imekatwa na mwekezaji, hana kibali, hana utaratibu na wala hajaulizwa na mtu, hivi ninavyokwambieni! Hivyo basi ni vyema tunapoleta au tunapojenga *idea* ya kuleta miradi mengine mbadala, basi sheria zikafuatwa kwa wageni wetu, si kuwakamata wazawa tu wakakosa eneo lao, lakini mgeni akafanya atakavyo. Ni vyema ukaangalie eneo hilo lililokatwa mikoko ili ulitumie vizuri na wewe katika utaratibu wa kuona kwamba tunaweza tukafugia samaki na kuweza kuleta mabadiliko katika shehia hii. Baada ya kuyasema hayo Mhe. Spika, nakushukuru tena sana kwa kunipatia nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mimi pia nakushukuru. Sasa nimkaribishe Mhe. Mohammed Haji Khalid, afuatiwe na Mhe. Salim Abdalla Hamad, wakati Mhe. Salma Mussa Bilal anajitayarisha.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata wasaa kidogo wa kutoa mchango wangu mdogo sana juu ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha mimi pamoja na sote tulio hapa kuweza kufika katika Baraza hili, kuja kutekeleza majukumu yetu ya kazi zetu za kawaida. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutuandalia kitabu hiki cha wizara yao, ingawaje karatasi zake zinanyofoka ovyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ni moja ya wizara muhimu sana na kwa kawaida kila wizara tunaitaja kuwa ni muhimu, lakini kila moja ina umuhimu wa aina yake; hii ni wizara ambayo ndio tofali la mwili, kwa sababu mwili unajengwa kwa chakula bora na chakula bora kinajengwa na uvuvi. Kuna nyama, maziwa na samaki, vitu hivi kwa pamoja vinafanya chakula bora na ukitumia vizuri unapata *balance diet*. Kama utabahatika kunywa angalau glasi ya maziwa na yai moja la kuku kwa kila siku, basi utakuwa umetimiza mahitaji yote ya mwili, unapata *protean, carbon hydrogen, fat, vitamin* na vyengine vyote. Kwa hivyo, wizara hii ni wizara muhimu sana kwa sababu inahusika na ujenzi wa afya zetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa ina umuhimu huo basi mimi nianze na hii sekta ya mifugo, kwenye mafanikio yao walioyataja kwenye ukurasa wa 3. Nizungumzie kwenye kifungu cha 1, 2 na cha 3 kwa ufupi sana. Kwa sababu kuna ongezeko la maziwa kutoka lita 24,000 hadi 27,000 sawa na ongezeko la asilimia 12, kutoka mwaka 2012 na 2013. Kwa hivyo, wameongeza uzalishaji wa maziwa.

Halikadhalika wameongeza na uzalishaji wa mayai na pia nyama hapa wamesema nyama ya ng'ombe tu, lakini sina hakika kuwa na mbuzi wako, kondoo na wengineo. Kwa kuwa kondoo na mbuzi hawakutajwa, je, hawa hapa Zanzibar hawafugwi na kama wanafungwa wameongezeka kwa kiasi gani au wamepungua kwa kiasi gani, kwa sababu kigezo chao ni nyama ya ng'ombe tu. Wakati nyama inatokana na mbuzi, kondoo na hao ng'ombe, ukiacha kuku ambae anatoka kwenye ndege yeye, tunapata mayai na yeye kuku mwenyewe.

Sasa Mhe. Spika, tulikuwa na miradi mingi ya mifugo ambayo imeanzishwa na taasisi mbali mbali za kimataifa, lakini ugonjwa wetu ni mmoja. Mara tu ule mradi ulipomalizika sehemu nyengi yenye miradi huwa inakufa. Sijui wataalamu wetu wanashindwa kuifuatilia au wafugaji wanashindwa kuiendeleza na vinginevyo.

Mhe. Spika, kulizuka mradi wa ufugaji ng'ombe chotara. Mara tu ule mradi ulipomalizika sehemu nyingi zenye miradi huwa inakufa. Sijui wataalamu wetu wanashindwa kuifuatilia au wafugaji wanashindwa kuiendeleza na vinginevyo.

Mhe. Spika, kulizuka mradi wa ufugaji ng'ombe chotara wa *PADEP*.

(hapa umeme ulizimika kwa muda)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mwangaza huu unatosha Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe endelea.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Niendelee. Sioni. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na kwamba mawasiliano yapo, lakini kutokana na kwamba kumekuwa na kiza kizito, ingawa mimi nawaona huko mliko. Lakini kumbe ilikuwa tuonane. Basi Mhe. Mjumbe anayezungumza pale analalamika zile dondoo zake. Aaah! Huo. *(Makofi)*

(baada ya muda mfupi umeme ulirudi)

Mhe. Spika: Sasa Mhe. Mjumbe uendelee nadhani unaona.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Vizuri sana. Mhe. Spika, nashukuru kuwa mwangaza umerudi na unaangaza vizuri sana. Mhe. Spika, miradi hii ya ufugaji wa mbuzi na ng'ombe tumepata kwa ufadhili. Lakini baada ya mradi kumalizika muda wake basi miradi mingi inakufa.

Je, nimuulize Mhe. Waziri tatizo ni nini? Katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba wamepata ng'ombe wa *PADEP*, lakini katika utafiti wangu kule kwetu Pemba baada ya mradi kumalizika basi ng'ombe wale wamekufa mmoja mmoja na ng'ombe wengi wametoweka hawapo tena, sijui tatizo ni nini. Kwa hivyo, Mhe. Spika, iko haja ya wizara hii pale tunapoanzisha miradi kwanza wafugaji wapatiwe taaluma kabla ule mradi haujaanza, ili kila siku tusianze upya.

Mhe. Spika, wanawake wa ukanda wa bahari wengi wao wanajishughulisha na ulimaji wa mwani, kama wanaume wapo wanaofanyakazi hii ni wachache sana. Lakini kama ilivyoelezwa katika kitabu hiki, biashara hii bei yake ni ndogo sana kazi ni kubwa lakini mapato yake ni madogo sana, ingawaje mashirika binafsi ndio yanayonunua mwani na kwa kuwa kilimo chenyewe kimo ndani ya wizara yetu, kwa hivyo wizara ina haja kubwa tena ya lazima ya kuwatafutia masoko yaliyo bora hawa wanawake, ili watokane na umaskini uliowaganda mgongoni mwao.

Wanawake hawa wanahangaika usiku, mchana wote huko vijijini, akitoka huko akatafute maji apike na afanye shughuli zote. Kwa hivyo, Mhe. Spika, wizara mnayo haki ya kuwaonea huruma kina mama hawa kutokana na mahangaiko makubwa wanayohangaikia maisha.

Mhe. Spika, licha ya mwani, kuna wabebaji na watengenezaji madagaa, sio wavuvi lakini ni wanawake wanaoanika. Wizara iwatafutie mbinu bora za mali hii kwa sababu dagaa siku hizi ni mali, lakini uanikaji wetu bado ni wa kienyeji. Kwa hivyo, tutafute mbinu bora ya kuhifadhi dagaa ili tuweze kusafirisha hata nje ya Tanzania. Kwa sababu ni imani yangu kuwa dagaa na pweza wana bei nzuri.

Mhe. Spika, wizara hii kama nilivyosema ni wizara muhimu na inahitaji wafanyakazi wake waboreshwe, watafutiwe makaazi mazuri, kama wizara hii haina nyumba hata kuwapatia mikopo ya nyumba ni vyema, kama wanapopahala nyumba zao wenyewe basi wafanyiwe vyovyote vile kama zina wapangaji wengine au watu wengine ambao sio wa wizara hii, basi watafute taratibu za kuwatoa, ili nyumba hizi wawakabidhi wafanyakazi wao. Sio vyema kuwa wizara ina nyumba lakini mpangaji wake au mkaazi wake akawa ni mtu mwengine na mfanyakazi wako akawa ana haha na kuhangaika kutafuta akae wapi kumbe nyumba ya wizara ipo. Kufanya hivyo itakuwa wafanyakazi wetu hatuwatendei haki.

Mhe. Spika, uvuvi wa kisasa unahitaji uendelezwe. Siku zote tunazungumza uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Spika, inasemekana Zanzibar kuna samaki wengi sana, lakini nyenzo za kuvulia ni haba sana au hazipo kabisa. Wavuvi wakubwa kwa kule Pemba ni Wakojani ambao wanatumia uvuvi wa nyavu, na utahisi kuwa samaki wapo kwa wingi, lakini utaalamu na vifaa vya kisasa vya uvuvi basi wavuvi wetu hawana. Mara nyengine unamsaidia unampa nyavu, kuna mara moja nimeona wavuvi wanapewa mademe. Dema si msaada mzuri wa kumsaidia mvuvi. Unajikaza unakwenda kumpa mvuvi dema, uvuvi ambao ni wa toka babu yangu hajazaliwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tumtafutie mvuvi wetu zana za kileo za uvuvi aende baharini avuwe ili tupate samaki wa kutosha na ikiwezekana tuweze kusafirisha nchi za nje.

Mhe. Spika, mimi nilisema leo sina mengi ya kusema, lakini nihitimishe maelezo yangu kwa kusema wizara hii kama nilivyosema mwanzo ni muhimu, mazao yake ni yale yenye kujenga mwili. Kwa hivyo, inafaa serikali iiangalie kwa jicho la huruma wizara hii ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, nimetazama idara moja tu ya mipango sera na utafiti. Fedha iliyoombewa mwaka 2013/2014 na zile ambazo walizopata na zile hasa za matumizi mengineyo ni kama milioni 31,300,000 sawa na asilimia 24. Sasa hayo matumizi mengineyo ndio fedha za kuendeshea idara. Idara hii ni ya utafiti, ina maana kila linalofanywa katika wizara hawa ndio wanaotafiti, akini wametiliwa asilimia 24 tu ya pesa za kufanyia kazi. Je, itawezaje kufanyakazi kwa ufanisi na ipate maendeleo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano tu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama serikali kweli imekusudia wizara hii iendelee na iwepo na ilete tija, basi ni vyema ikapewa pesa za kutosha ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nasema ahsante sana na dakika zangu tano kama kuna mwenzangu ana maneno mengi basi namuachia yeye, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Salma Mussa Bilal ameomba dharura, kwa hivyo nafasi yake ichukuliwe na Mhe. Salma Mohammed Ali, wakati Mhe. Subeit Khamis Faki anajitayarisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kitabu hiki cha bajeti cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mhe. Spika, awali ya yote kwanza niende kwenye ukurasa wa 55, ambapo huku kuna kiambatanisho namba 6 chenye orodha ya wafanyakazi wa wizara kiidara na kwa jinsia zao kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hadi mwaka 2014 Aprili.

Mhe. Spika, katika ukurasa huu jumla ya wafanyakazi wote katika idara zote sita ni 752 kati ya hao 526 ni wanaume na 226 ni wanawake, kiasilimia wanaume ni asilimia 70 na wanawake ni asilimia 30, naipongeza wizara kwa kufikia lengo hilo lililokuwa likitarajiwa.

Jengine Mhe. Spika, nianze kwa idara ya mazao ya baharini na katika hili Mhe. Spika, ambalo liko katika ukurasa wa 38 ni kwamba ufugaji wa mazao ya baharini ni pamoja na ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na pia kuna ukulima wa mwani. Mhe. Spika, kwa makusudi wizara imejitahidi sana katika kuona kuwa wanaitumia bahari ya Zanzibar kwa uzalishaji wa mazao ya baharini, na vile vile wanaitumia nchi kavu kwa uzalishaji wa wanyama wa mifugo.

Mhe. Spika, ufugaji wa samaki ni kazi nzito na ni kazi ambayo mpaka ukipata pahala pa kufugia samaki, basi utumie nguvu sana. Kwa bahati nzuri wananchi wetu wa rika zote wameitikia wito wa wizara wa ufugaji wa samaki, na takriban katika majimbo yote ambayo yako karibu na bahari na kwenye mazingira yanayofaa, basi kazi hii imeendelea katika kasi kubwa.

Mhe. Spika, la kusikitisha ni kuwa hii kasi ni ya kitaalamu na ufugaji wa samaki pia ni wa kitaalamu, mazingira ya bahari na humo samaki wanamofugiwa, zinatofautiana kutoka sehemu na sehemu. Kwani hata kwa utaalamu katika kuona ni samaki wa aina gani wawekwe sehemu gani pamoja na hizo sehemu za kufugia.

Mhe. Spika, ili tuendelee pia kunahitaji ufuatiliaji wa nguvu, yaani kila siku kuwe na ufuatiliaji; kuangalia hali ya mazingira yalivyo, kutoa ushauri pamoja na kusaidia pale panapohitaji msaada.

Ninakumbuka Mhe. Spika, wakati tulipokuwa na Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa akijitahidi sana kwa shughuli hizi, tena akijitahidi sana mwisho wa uhodari wake kufika kila sehemu kwa kutumia miguu ama gari na njia nyengine, kwa ajili ya kuona kazi inavyoendelea, lakini kupungua utamaduni ule na hali ya nguvu ya wananchi ya ufugaji samaki imerudi chini, na hivi sasa sehemu nyingi ukienda watu wamekata tamaa.

Kwa hivyo, kwa umuhimu wa suala hilo la ufugaji wa samaki baharini ninaiomba wizara kwa makusudi kabisa, iige ule mtindo ambao Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa akiutekeleza wa kujitahidi mara kwa mara kupita katika sehemu hizi, kwa ajili ya kuziona na wataalamu wake kutoa maelekezo, ili wale wanaoendelea na miradi hii waweze kufaidika na kunufaika. Pia kwa ufugaji wa kaa, chaza na majongoo. *(Makofi)*

Vile vile katika ufugaji wa majongoo ambalo ni jambo lenye thamani sana. Kwa kweli kama wizara ingekuwa inashughulikia na wenzetu wakawa wanaendelea na huu ufugaji na wakapata faida inayokusudiwa. Kwa hivyo, naamini wananchi wangekuliwa wameshajikomboa kiuchumi na pia serikali ingelijipatia fedha za kutosha.

Suala jengine Mhe. Spika, ninashukuru kwa juhudi inayochukuliwa kwa wizara kuhusu uzalishaji wa vifaranga vya samaki kwa upande wa Pemba tu peke yake kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 ni vifaranga 19,750 na kwa Unguja ni 7,796. Kutokana na hali hiyo, ninawaomba wafugaji wenzangu waliopo katika Kisiwa cha Unguja wajitahidi na ufugaji, ili wawe kama wenzao wa Pemba.

Lakini katika kuendeleza mambo haya ya ufugaji wa samaki wizara imetoa mashine tano kwa vikundi vinavyofuga samaki vilioko Pemba, na mashine hizi ni za kuingizia na kutoa maji, ambalo ni jambo muhimu sana, na kwa kuwa kila wanaofuga samaki huwa wanahitaji hizi mashine, kwa sababu kutoa maji ni kazi kubwa na wala hawaiwezi na kuingiza ndio hivyo hivyo.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo, je kwa zile sehemu nyengine ambazo bado mashine hizi hazijapelekwa na kwa umuhimu wake ndio zinahitajika sana, ili mradi uweze kukua, wizara imejipanga vipi kutafuta fedha za kutosha, kwa ajili ya wafugaji wetu wafaidike na mambo haya, ambapo katika sehemu nyengine wameshatuomba lakini uwezo wa kuwasaidia kwa wote ni mdogo.

Kwa kuwa ufugaji uko Pemba na Unguja, ninataka kujua kwa nini mashine hizo zote tano zikapelekwa upande mmoja tu wa Zanzibar na huku kwa wenzetu ikawa hazikupelekwa wakati ufugaji upo.

Nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu ukulima wa mwani. Mhe. Spika, ukulima wa mwani umeshamiri katika visiwa vyote vya Unguja na Pemba na hasa akinamama wanajitahidi katika kufanya kazi hii, lakini kazi ya ukulima wa mwani ni nzito na inapoteza nguvu nyingi, wakati kwenye mazingira mabaya ya chumvi masaa 24, na kwa bahati mbaya bei yake ni ndogo sana. Mhe. Spika, pamoja na juhudi zao wananchi hawafaidiki na kazi ya ukulima wa mwani wanayoifanya.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hiyo simu ingezimwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa sababu hiyo, ninaiomba sana wizara ihangaike kama ilivyoweka azimio la kutafuta soko zuri, ili wakulima wetu wa mwani waweze kufaidika. Hata hivyo, kama upo uwezekano wa kitaalamu kupatikana mbegu nzuri kwa maana ya kuwa zenye bei nzuri na zinazoweza kushamiri, ili waachane na ukulima wa mwani huu wanaoendelea nao, ambao mwani wenyewe hauna faida ya kutosha.

Mhe. Spika, kama upo uwezekano wizara iweke kiwanda maalum, kwa sababu mwani unasarifiwa katika mambo mengi sana, na tukiachia haya madogo madogo tunayofanya hapa hivi sasa, badala ya kupelekwa moja kwa moja nchi za nje kuuza, ili tuweze kuzalisha mambo kadhaa na Zanzibar kupata faida.

Katika ukurasa wa 7 wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, ukurasa huu unaeleza kuhusu changamoto zinazoikabili Sekta ya Uvuvi. Changamoto hizi ni nyingi, na mimi nitaelezea chache tu, naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 8 Changamoto katika Sekta ya Uvuvi kifungu cha pili, kinaeleza hivi:-

"Kuongezeka kwa uvuvi haramu kutokana na kuwepo kwa wavuvi kutoka nje ya Zanzibar na wavuvi vijana, wazawa katika maeneo ya hifadhi na kuvua uvuvi haramu na kusababisha uharibifu wa mazingira ya bahari".

Mhe. Spika, naamini wizara imetenga maeneo kwa ajili ya hifadhi kwa kuona kuwa yatasaidia katika uzalishaji wa samaki, kuenea samaki katika bahari na wananchi waweze kufaidika. Hali hii wamefanya makusudi kutokana na kasi kubwa ya uvuvi haramu kama vile kutumia nyavu zisizofaa na kasi kubwa inayotokana na tabia ya nchi.

Kutokana na hali hiyo ninaiomba wizara isichoke na ishirikiane na vyombo husika na itoe taaluma ya kutosha, ili wenzetu wakubaliane na azma hii nzuri ya wizara, na samaki hawa waweze kuhifadhiwa na kuzaliana kwa faida yetu sote.

Mhe. Spika, kutokana na wakati naona nimalizie hapo kwa habari ya uvuvi na sasa niendelee kabla sijaanza mifugo na uvuvi wa bahari kuu. Kuna uvuvi wa kina kikubwa cha maji kwa ufupi tunauita uvuvi wa Bahari Kuu.

Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba ukanda wetu wa Zanzibar tumeneemeka kuwa na samaki wengi kabisa, na kazi kubwa inayofanywa hivi sasa na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ni kufanya doria na wanatumia fedha nyingi kwa kukodi ndege kwa kufanya kazi hiyo, kuona kuwa samaki wetu hawaibiwi, pia wanafanya doria ili samaki wabakie katika maeneo yao, lakini bado hasa azma ya kuweka Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa ajili ya kupata faida kwa nchi hii haujaanza ipasavyo.

Sasa Mhe. Spika, mimi nafarajika na hii hatua waliyoianza ya kuomba misaada kwa kujenga soko na diko, lakini kwa kuwa tumejiingiza kwenye uvuvi wa bahari kuu, naomba suala hili lifuatiliwe kikamilifu na tuone kuwa sisi tunaingia kikamilifu katika uvuvi wa bahari kuu na kitakachopatikana kisarifiwe katika nchi hii kwa maslahi yetu pamoja na taifa kwa jumla.

Kwa mfano, hivi sasa kama kwa bahati mbaya watakamatwa samaki na kuletwa Zanzibar hawana pa kupelekwa kwa sababu hatuna mahala pa kuhifadhia. Kwa hivyo, ninashukuru kwa huu mpango uliowekwa, lakini uwe ni mpango utakaokamilika, ni vyema wazungumze na wafadhili vilivyo, na serikali ikubali kutoa fedha ilizokusudia, ili mradi huu uendelee vizuri na ninaamini utakuwa ni mkombozi wa Zanzibar.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niingie kwenye Sekta ya Mifugo. Mhe. Spika, katika sekta hii kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 3, kwamba wizara imepiga hatua kubwa sana ya mafanikio. Kwa mfano, kwa maziwa tu, tukiangalia mwaka 2012/2013 ni kuwa yaliongezeka kutoka tani 24,343 mpaka kufikia 27,243, mayai tani 9,663 mpaka kufikia 10,962 na nyama ya ng'ombe tani 4,538 hadi kufikia 4,966.

Katika mafanikio hayo, lakini kuna changamoto. Kwa mfano, katika mifugo wanasema eneo la kupandia majani au malisho halitoshi na tunajua kwamba nchi yetu ni ndogo, sehemu ya kilimo ni ndogo na tunataka kuendeleza ufugaji, watu wanaongezeka.

Kutokana na hali hii sijui wizara ina lengo la kufikia ng'ombe na mbuzi pamoja na wanyama wengine wanaokula majani wangapi, na iwe ni kiwango na kutafuta rai nyengine, ili hawa wanyama wetu isijekuwa tunafuga kwa wingi na halafu tukakosa malisho na matokeo yake ni vifo kwa wanyama wetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa kuku kulikuwa na utafutaji wa machotara katika bajeti iliyopita na wenzetu walikuwa wanatafuta machotara wa kuku kwa kuku wa kigeni na kuku kishingo, na kwa sababu ni kuwa kuku kishingo ni mlezi sana. Leo tunaona kuna kuku wa kigeni pamoja na makuchi. *(Makofi)*

Sasa ninaomba kupata taarifa, Mhe. Spika unapofanya kitu unakifanyia utafiti na kupata matokeo yake na tunaelekezana. Je, ule mpango wa kupata machotara wa kuku kishingo umefikia wapi, umeleta faida au ulikuwa na makisio tu na yale yaliyokusudiwa hayakupatikana mpaka tukaingia katika makuchi. *(Makofi)*

Vile vile tukifungua kwenye ukurasa wa 4 hapa kuna changamoto katika Sekta ya Mifugo. Mhe. Spika, changamoto hizi katika sekta hii ziko nyingi, lakini moja miongoni mwa changamoto ni kutowafikia baadhi ya wananchi wanaohitaji huduma ya ugani, kutokana na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi ikiwemo vyombo vya usafiri kwa watoa huduma za ugani.

Mhe. Spika, huduma za ugani ni za lazima kabisa, kwa sababu huu ni ufugaji na tuna-*deal* na viumbe, wanapatwa na matatizo mengi, kwa hiyo elimu hii kwa wanyama ni muhimu. Kwa hivyo, ikiwa wizara yenyewe ina matatizo haya ya kutokuwa na usafiri na wenzetu kuweza kufika huko kwenye ufugaji, sijui ufugaji huu utaendelea vipi, wakati inaweza kutokea athari ndogo tu na ikasababisha viumbe vingi kupata athari.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze baada ya kujua kwamba kuna changamoto hii, amejitahidi vipi kuona kuwa changamoto hii itaondoka, ili wenzetu wanaojitahidi na ufugaji wasije wakatokewa na matatizo ya kuvunjika moyo ambayo hawakuyatarajia.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, sawa. Suala jengine ni kuhusu uhaba wa malisho ambalo tayari nimeshalieleza.

Sasa kama zimebakia dakika tatu naomba niende ukurasa wa 66 na hapa naomba nipate maelezo. Mhe. Spika, katika ukurasa huu kuna kiambatanisho 14 kuhusu Mradi wa kuimarisha ufugaji wa mazao baharini. Ni mradi wa mwaka 2012/2013 na 2013/2014, gharama zinazohitajika za mradi huu hupangwa kila mwaka na kuidhinishwa na mfadhili na serikali, lengo kuu ni kuimarisha ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Mhe. Spika, mradi huu ulitengewa shilingi milioni 100 kutoka serikalini na jumla ya shilingi milioni 564 kutoka kwa washirika wa maendeleo, lakini kwa bahati mbaya mradi huu, ambao ulikuwa na malengo makubwa tu haukutekelezwa kutokana na kuwa hakuna fedha iliyopatikana. Kwa hivyo, ninaomba kujua ni hasara ya kiasi gani ambayo imetokea ya kukusanya fedha hizi na kwa nini hazikupatikana hata hizo fedha za serikali zilizoahidiwa.

Mwisho Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati kuna mradi huu wa kuimarisha uvuvi wa kina kirefu cha maji, na mradi huu jina lake ni Mradi wa Bahari Kuu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umemalizika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, sawa namaliza hii *table* tu. Muda wa miaka minne na huu pia kazi haikufanyika hata moja naomba nijue kwa sababu gani.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mhe. Salma Mohammed Ali, baadaye Mhe. Subeit Khamis Faki na anajitayarisha Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake, pia nimpongeze kwa mashirikiano makubwa waliyonayo na Mhe. Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa jitihada yake kubwa aliyonayo ya kuwatembelea wafugaji wakiwemo vikundi vya wafugaji vilivyomo kwenye wilaya yangu. Kwa kweli ninamuomba aendelee nayo jitihada hiyo, kwa sababu vikundi ni vingi, na wote wanaona Mawaziri wakiwatembelea hufarajika na hupata angalau kupewa mawaidha kidogo katika zile kazi zao. *(Makofi)*

Nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 22 kuhusu Idara ya Uzalishaji wa Mifugo na mchango wangu utakuwa ni mdogo sana. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri ametueleza kama ng'ombe waliopandishwa ni 2013/2014 ni ng'ombe 2,385, lakini ng'ombe walioshika mimba ni 1,623 sawa na asilimia 68 na hii si asilimia ndogo. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, anieleze kuhusu hawa ng'ombe 762 kuna sababu gani iliyosababisha wasishike mimba, hivi mbegu ni mbovu au ni matatizo ya ng'ombe wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, najua Waheshimiwa Wajumbe wanashangaa kuuliza hivi, lakini nauliza hivyo kwa sababu na mimi ni miongoni mwa wafugaji. Vile vile ninasema haya kwa sababu ninajua wafugaji wanazinunua mbegu, gharama ya kununua mbegu mpaka ukamaliza ile huduma ya kupandisha si chini ya shilingi 9,000/= au 10,000/=. *(Makofi)*

Kwa kweli tumuangalie mfugaji mnyonge anunue mbegu mara ya kwanza asifanikiwe, mara ya pili asifanikiwe na mara ya tatu nadhani atakata tamaa. Mhe. Spika, hii itarudi kule nyuma ambako Mhe. Waziri ametueleza kwamba kuna mpango wa kuondoka huko tulikokuweko huko nyuma kuwa na kundi kubwa la ng'ombe lakini uzalishaji wa maziwa ni mdogo.

Mhe. Spika, mfugaji atakapotoa fedha mara mbili au tatu kwa kupata huduma hii na asifanikiwe, lazima atarudi kule kule na wala atakuwa hana uwezo wa kuendelea kila mara kununua mbegu.

Kwa hiyo, ninamuomba hapa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atufahamishe ni tatizo gani, lakini ikiwa ni tatizo la kiafya au matatizo mengine ya mifugo, awaelimishe wafugaji, ili waepukane na hizi hasara zinazotokea.

Katika maelezo ya Mhe. Waziri amesema kwamba ndama 409 wameekewa kumbukumbu za wazazi wao pamoja na uzalishaji wa maziwa.

Mhe. Spika, najua pengine hawa 400 ndio waliozaliwa katika hao waliotajwa wameshika mimba pengine kuna wengine hawajazaliwa, lakini naomba niulize hawa ndio walioulizwa? Na ikiwa ni zaidi ya hawa kwa nini hawa wengine wasiwekewe kumbukumbu kwa sababu Mhe. Spika, hapo mimi nilipokuwa nikifuga na nilikuwa nipo makini hasa maana yake ilikuwa sasa hivi sina utulivu katika mifugo, yule ng'ombe akija kupandishiwa na daktari kuna gamba ananijazia kama unavyokwenda kliniki mja mzito au mtoto, sasa ile peke yake ni kumbukumbu, na ile inasaidia yule mfugaji anajua kama ng'ombe kutokana na asili yake uzalishaji wake utakuwa vipi.

Kwa hivyo atakuwa imara katika kumkuza yule ndama kuliko ikiwa hana chochote, ana kundi la ndama hajui yule aliyekuwa na kiwango kizuri ni yupi, wote atawalea katika mazingira yaliyokuwa ni sawa sawa, lakini yule akijua kwamba yupi uzalishaji wake ni mzuri atamlea vizuri kwa sababu atakuwa na matumaini.

Mhe. Spika, hili jambo la kuweka ni zuri na naomba wizara iwe makini, kila mfugaji ambaye watampa huduma hiyo ya upandishaji basi wamuwekee kumbukumbu ya ng'ombe wake na ule uasilia wake, ili wakimfahamisha ile thamani yake pengine ataweza kumuendeleza vizuri yule ndama kuliko kuachia tu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo napenda nilizungumzie ni ukurasa wa 28 hii ni Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo. Mhe. Spika, katika malengo yao ya mwaka 2013/2014 mbili pale kuna kuendeleza huduma za ugani kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama na maradhi ya kuambukiza, kupe na kuhamasisha wananchi juu ya kuzuia ukatili wa wanyama.

Hapa mimi sitaki niseme mengi lakini nawapongeza sana ingawa sijui mafanikio kwa huku kuhamasisha wananchi juu ya kuzuia ukatili wa wanyama. Mhe. Spika, mwaka jana nilichangia sana kuhusu ukatili wa wanyama, lakini japo wizara imefanya jitihada lakini ukatili bado upo, tukitembea tembea leo Mhe. Mussa kasema hapa kwamba ng'ombe hupewa mizigo ambayo alokuwa haiwezi, hili ni kweli. Utamkuta ng'ombe kapakiwa kwenye gari hata kunyanyua ule mguu hawezi, na yule mwenye ng'ombe ukimwambia kama huyu ng'ombe bora hii mizigo ungeliigawa aende akarudi akaja akachukua tena kuliko hivi ulivyompakilisha, hukwambia huyu ng'ombe wangu akifa usije ukaninunulia mwengine.

Mhe. Spika, huyu anakujibu kwa sababu anaona ile mali ni yake, kwa hivyo wewe huna uwezo wa kumuingilia, kwa hivyo naomba wizara bado itoe elimu kwa wafugaji. Halafu vile vile na hatua zichukuliwe kwa wale wanaofanya ukatili, kile ni kiumbe hata kama ni chako lakini ni kiumbe, huwezi kukiumba wewe na ana hisia na maumivu, kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Wizara iwe makini juu ya suala hili.

Kwa kweli katika Wilaya ya Chake jimbo lililokuwa likiongoza kwa ukatili wa wanyama ni jimbo la Wawi, ukiweka ng'ombe wako ukienda asubuhi ameshakatwa paja, keshachinjwa, hawachukui watu waue tu, kwa kweli huu ni ukatili mkubwa, lakini hivi sasa tunashukuru umepungua kidogo. Ingawa kwa masikitiko makubwa Mhe. Spika, ukatili ule jimbo la Wawi umetoka kwenye ng'ombe sasa umekuja kwenye binaadamu. Juzi tu tulimsikia hapa Maalim Saleh akizungumzia kuhusu mtoto aliyenyongwa na kutiwa kwenye jengo kwa kweli haya ni mambo ya kusikitisha.

Lakini katika lengo hili pia Mhe. Spika, wametaja hawa kuhusu adui mkubwa wa mifugo ambaye ni kupe, na katika ukurasa wa 29 wameeleza kama wanyama waliokogeshwa ni 51,370, kwa kweli Wizara imejitahidi lakini katika kupambana na suala la kupe ni lazima kuimarishwe majosho, majosho ni muhimu; wafugaji wote si kweli kama wataweza kupata bomba na kupata kulitumia na hapa pia ni tatizo kwa sababu mimi ninavyohisi inaweza kuwaletea athari ya afya yao.

Mhe. Spika, mimi ni mfugaji wa miaka mingi na utaratibu ambao wafugaji wengi wanautumia wa kukosha ng'ombe wao ni kuingiza maji kwenye ndoo wakaingiza na dawa, halafu wakapaka kwa kumbi ile Mhe. Spika ni sumu, sasa ikiwa mtu kila akitaka kukosha ng'ombe wake pengine ana ng'ombe watano au sita kazi ni ile pale pana athari.

Naiomba Wizara ijipange kutayarisha majosho, na tena hapa namuomba hasa Mhe. Waziri atakaposimama anambie katika kisiwa cha Unguja kuna majosho mangapi na Pemba kuna majosho mangapi, na yanayofanya kazi ni mangapi, kwa sababu pengine yapo mengi lakini hayafanyi kazi. Halafu anieleze hawa wafugaji wamewahamasisha vipi juu ya kutumia hayo majosho.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo Mheshimiwa ni changamoto kwa kweli hii ni changamoto kubwa ni ukosefu wa malisho hasa wakati wa kiangazi, na katika ukurasa wa 21 Mhe. Spika, usishangae kuona natafuta sana kwa sababu hichi kitabu kila karatasi ni pake, hakuna karatasi zilizoshikana, unaweza kukuta namba 21 unaitafuta lakini iko kwenye 55, kwa hivyo tunakuomba utuvumilie.

Katika ukurasa huu wa 21 Mhe. Waziri kasema kama wafugaji 20 walipatiwa mafunzo ya kuhifadhi malisho, na umuhimu wake kuwapa mafunzo wafugaji kwa kuhifadhi malisho ni jambo zuri, kwa sababu tunaiona hali ya

malisho ilivyo na ikifika msimu huu ng'ombe kwa kweli hudhoofika, uzalishaji hupungua, lakini kinachonishangaza waliopewa mafunzo ni wafugaji 20. Namuomba Mhe. Waziri atakaposimama anambie Zanzibar tuna wafugaji wangapi na hawa 20 ambao wamewapa mafunzo ni asilimia ngapi, hili tupime hawa waliopewa mafunzo watatusaidia vipi. Kwa sababu sifikirii kama pengine kwenye watu 5000 uchukue mtu mmoja umpe mafunzo halafu useme tayari nishafundisha.

Mhe. Spika, changamoto nyengine ambayo imewakabili sana wafugaji wa kuku ni ugonjwa. Na hapa pia naomba niipongeze sana Wizara naiona jitihada yao lakini bado ugonjwa wa kuku na mabata ni matatizo, utamuona mfugaji tayari ameshaimarika ana kuku wengi siku moja tu mahepe yakiingia washamaliza. Sasa naomba Wizara bado iendelee na jitihada zao tunaziona, lakini waendelee kwa sababu wananchi wengi walio wanyonge wanategemea hii mifugo, sasa ikiwa kila siku umeshajenga imani tayari imeshaondoka yote, tunaomba waendelee halafu pia watoe elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora.

Mhe. Spika, changamoto nyengine ambayo nayo ni nzito kwa wafugaji ni ughali wa dawa. Kwa kweli hili ni tatizo na naomba Wizara iwahurumie wafugaji, kwa sababu nina mfano mimi Wizara ya kilimo siku hizo nina muda wa kufuga lakini nikilima, ukitaka mbegu mabilingani na nyengine unakwenda zako duka la kilimo, kwa nini Wizara na wao hawaweki duka la kuuza hizi dawa, kwa sababu ile Wizara itakuwa na wao pia ni wadau hawatowafanyia kama wafanyabiashara ambao wanatia faida mara tatu zaidi, lakini ikiwa kuna duka la kilimo ingelikuwa wale wanatia faida ya kupata wao lakini wakajua na wale wafugaji watapata faida. Mhe. Spika, naomba Wizara ilizingatie hili.

La mwisho ambalo sitaki nichangie lakini ni malalamiko kidogo Mhe. Spika, ni kuhusu chumvi. Mwaka jana nilichangia kuhusu chumvi tena niliichangia Wizara ya Kilimo, *hansard* ninayo na nitasoma pale ambapo ulinambia wewe niachie, ulisema Mhe. Mwenyekiti wakati huo wewe ni Mwenyekiti mimi nafikiri Mhe. Salma kwanza tukupongeze kama walivyokupongeza Waheshimiwa Mawaziri juu ya suala hili, na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi tayari ametoa ahadi namalizia hapo.

Mhe. Spika, hichi ni kitabu cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi sijaona hata kifungu kimoja kilichozungumzia chumvi, isitoshe malalamiko yangu mengine kwako nilileta swali baada ya bajeti tu ile nikasema nitapeleka swali la chunvi bila ya shaka tutapata ufumbuzi.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa nasikia swali lile limekuwa kama mpira kati kati ya uwanja; likipelekwa kilimo wanasema halituhusu, likipelekwa mifugo nao wanasema si letu, likipelekwa biashara mimi mpaka pazalishwe. Sasa naomba swali langu nililolileta Serikali hii ina Wizara 16, na najua hakuna hata jambo moja lililokuwa halina Wizara, kwa hivyo ikiwa swali lile halikupata Wizara; swali langu lipelekwe kwa Makamu wa Pili wa Rais aje anijibu. Nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mnadhimu wa Serikali amesikia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana jioni hii ya leo kunipa na mimi fursa kuchangia machache niliyonayo Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianzie na Idara ya Mifugo Mhe. Waziri ametueleza katika kitabu chake cha hotuba yake ya bajeti kama wameongeza mazao haya ambayo wamezalisha nyama nyingi, asilimia ukurasa huu wa nne ambao kuwa wanasema wamezalisha nyama.

Kwa mwaka wa fedha uliopita 2012 ilikuwa ni tani 4,338 lakini kwa mwaka huu 2013 mwaka uliopita wamezalisha tani 4,966 hiyo wameongeza kuzalisha mayai ambayo kwa mwaka uliopita 2012 ilikuwa ni tani 9,663 na kwa mwaka 2013 wamezalisha tani 10,992.

Pia wakati huo huo wamezalisha mayai wameongeza ikiwa mwaka 2012 walizalisha tani 24,343 na mwaka 2013/14 wamezalisha tani 27,245. Mhe. Spika, ni ongezeko kubwa hili, lakini sasa tujiulize kutokana na hali ya nchi yetu na jinsi Mwenyezi Mungu anavyotujaalia soko ambalo vitu vyote hivi vinavyotajwa kwa hapa kwetu vina soko, kwa sababu vitu vyote hivi vinatumika katika utalii na *alhamdulillahi* katika nchi yetu utalii upo na hivi vitu vinatakiwa.

Sasa Mheshimiwa pamoja na jitihada hii wanayofanya ya kuzalisha na kuongeza mazalisho hayo mimi nawaomba sana waongeze bidii, kwa sababu soko lipo na bado tunaagizia vitu hivi kutoka nje ya nchi.

Kama tunaagizia vitu hivi kutoka nje ya nchi sisi tunapiga kelele kwa ajira, kwa hivyo kama tunapiga kelele kwa ajira ina maana watu wa mahoteli hawa wakiagizia mayai kutoka kwao kuna watu huku ambao walikuwa wanazalisha mayai wangepata fedha zikabakia katika nchi yetu zinakwenda kwao. Wangeongeza hizi nyama basi fedha zile zingebakia kwa ajili ya kuzunguka katika nchi yetu, na ikiwa ni kuku kadhalika.

Mheshimiwa naomba sana Mhe. Waziri kwanza hata tukimlaumu lakini pia tumuonee imani, kwa sababu bajeti anayopewa ni ndogo kweli kweli, sasa tunaiomba Serikali bajeti hii ya uvuvi iongezwe, kwa sababu kuna mambo mengi muhimu ambayo kuwa yanaweza kuwasaidia wananchi wetu kupata ajira zaidi.

Sasa ikiwa kuku wanaagiziwa kutoka nje wale tuliopiga kelele kipindi kilichopita wale ingekuwa wanazalishwa kuku kwa wingi zaidi hapa kwetu wasingeletwa kuku wale kutoka Brazil, wangekuwa kuku wote wanatoka hapa hapa kwetu, lakini inabidi kutoka kuku kule.

Kwa hivyo nawaomba sana Mheshimiwa waongeze bidii wawezeshe wafugaji wawasaidie mitaji, na wakati huo huo Mheshimiwa awasaidie wajiimarishe kuwasaidia dawa za ugonjwa wa kuku, kwa sababu kuku wanafuga halafu wanapata matatizo wanakufa. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kwa kupitia Wizara yake waongeze juhudi zaidi ili mifugo hii iongezeke hapa kwetu, kwa sababu Mheshimiwa ukiangalia hizo tani za nyama zinazotajwa hapa usidhanie kwamba ng'ombe hao wote wanatoka hapa Zanzibar, hapana, ni ng'ombe kutoka nje ya Zanzibar.

Sasa sisi tumeongeza hizo nyama tani kwa kupima kwenye mabucha lakini ni ng'ombe wanaotoka nje ya Zanzibar, kwa hivyo tuongeze bidii ili haya mazao yawe yanaenea hapa hapa Zanzibar, suala hili naliachia hapa.

Mimi nakwenda suala la Uvuvi. Mheshimiwa kwanza tutawaua wananchi wetu kwa tamaa, kwa sababu wananchi tunawatia tamaa kubwa lakini tukishawatia tamaa ule utekelezaji wake haupo, kila saa tunakuja kupiga kelele hapa uvuvi haramu uvuvi haramu,lakini sasa kama uvuvi haramu tunapiga kelele lazima watu wapate uvuvi mbadala.

Kila siku tunazungumza tu uvuvi wa Bahari Kuu uvuvi wa bahari kuu, hivi Mheshimiwa hatuoni kwamba kila mmoja anakula kutokana na hali ilivyo pale nchini. Wenzetu Tanzania Bara wana eneo kubwa la ardhi; wanazalisha almasi, dhahabu, kutokana na ardhi yao waliyokuwa nayo na ukubwa wa ardhi yao. Mwenyezi Mungu sisi Wazanzibari katukuzia bahari kwa sababu sisi tupo baharini, kwa hivyo tunatakiwa na sisi tule kutokana na bahari, ndiyo Mwenyezi Mungu aliyotujaalia, tunayo kubwa.

Lakini leo bahari tunayo; vya kutunza tukaizalisha tunaichezea tu hivi mpaka lini tutazalisha, yaani sisi tunashindwa kuzalisha samaki na Mwanza ambao wana Ziwa, wanauza minofu ya samaki wanapata faida katika nchi yao leo sisi tuna bahari tunashindwa kuuza samaki, tunavua samaki wa kitoweo tu hapa nchini kwetu, Mwanza wanauza samaki wakipeleka nje na tena ni ziwa tu, wanavua kwenye ziwa tu.

Mwenyezi Mungu katujaalia Bahari ya Hindi tunayo, sisi hapa Zanzibar muna makanadi hawajaonapo wavuvi, tizama wakati wa kaskazi tu hapa tuangalie wakati wa kaskazi tu wavuvi wetu hawa wadogo wadogo ambao hawana zana za ukamilifu, lakini tizama wanavyowaleta nduaro hapa, wanaleta mbasi wale tunaowaita nduaro hapa kaskazi mpaka unashangaa.

Kwa hiyo Mheshimiwa tunaomba sana muiwezeshe hii Wizara ili iweze kuongeza mazao na iweze kuongeza mapato ya nchi yetu, kwa sababu kama kweli bahari tunaweza kuishika kweli na Serikali ikafumbua macho ikaleta zana za wavuvi, kama hatuna uwezo tukaleta wafadhili; wahisani, wakawekeza lakini wananchi wetu wanaweza kupata ajira wengi na tunaweza kuongeza, maana sasa hivi tunategemea utalii na zao letu la karafuu, lakini Mwenyezi Mungu katujaalia mazao yapo ya baharini kwa nini hatuyavui au hatuyazalishi mpaka lini tunapanga karatasini tu.

Mhe. Spika, sisi tunapanga vitabu vyetu watu wanavitumia, maana sisi tunapanga kwenye vitabu tunayaacha kwenye maboksi watu wanatumia, wenzetu wameshaendelea kwa bahari kuna nchi wanataka masamaki yale ambayo kuwa ni majodari, yale ambayo Wachina wanakula mpaka mabichi, lakini kwa nini sisi tunapanga karatasini tu mpaka lini hivi,

Mhe. Spika, namuomba sana Waziri wa Fedha hayupo, leo aone kama huyu Waziri ampe bajeti kubwa aweze kuajiri watu, kwa sababu ajira zipo hapa kwenye uvuvi katika nchi yetu. Jamani sisi tumepewa bahari na Mwenyezi Mungu, kwa nini hatuvuni kwenye bahari mpaka lini jamani tutapiga kelele mpaka lini? Kila siku uvuvi wa bahari kuu unapangiwa uvuvi wa bahari, hivi tutakuja vuna lini au sisi kwetu ni kupanda hatuvuni? Mhe. Spika, suala hilo napenda niliache hapo.

Suala jengine ambalo nataka nizungumze wenzangu wamezungumza hapa kuhusu kilimo cha mwani. Kilimo cha mwani wakulima wetu wa mwani bado bei iliyopo ni ndogo, ni ndogo hawa walimaji wa mwani Mheshimiwa wanakuwa na matatizo sana, kwa sababu matatizo yao wanaolima, mule wanamolima mwani mnakuwa na hasara kubwa sana. Sasa inatakiwa watu wakienda kule kwenye zile hasara, wakirudi wapate matunda mtu anaweza kuulima mwani, zao la mwezi mzima akatumia wiki mbili tu, hapati akiba.

Naomba sana Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na serikali wafanye jitihada kwa hawa wanunuaji wa mwani, ili waweze kuwaongezea bei wananchi wetu wafaidike na zao lao hili la mwani hasa ukizingatia kwamba wananchi wetu wameitikia sana kilimo cha mwani. Na ukizingatia kilimo cha mwani kinakubalika.

Kwa hivyo ninamuomba sana, kwa sababu wananchi wangu wa Micheweni wameitikia na mwani unapatikana kwa wingi, kwa hivyo naomba sana waone kwamba wakulima wa mwani na wao wanahitaji kuongezewa bei ili wafaidike na kilimo chao.

Mhe. Spika, katika wakulima wa mwani mule wanamolima muna samaki wale wanaoitwa makarwe, kuna samaki wanaoitwa bocho, wote hao ni samaki ambao wanaweza kulima na kilimo hiki kinalimwa sana wanawake.

Anakwenda mtu kuvuna mwani anachomwa na bocho anakaa miezi miwili kitandani, anakwenda kulima mwani anachomwa na karwe miezi miwili yuko kitandani. Leo miezi miwili yuko kitandani na kile kilimo anachokweda kinampa hatari hawezi kupata hata kula ya siku mbili. Mhe. Spika, namuomba sana hili suala alione.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka nizungumzie ni kwamba wavuvi tunawadharau, na kwa nini niseme wavuvi tunawadharau. Kipindi kilichopita sisi sote tulikwenda Bunge la Katiba na ilikuwa zimetengwa nafasi kutoka taasisi mbali mbali Wajumbe ambao watashiriki kwenye Bunge la Katiba, na katika hao Wajumbe waliopangwa kushiriki kwenye Bunge la Katiba walikuwemo na wavuvi walitajwa kwamba na wavuvi wawemo.

Sasa kama ilikuwa na wavuvi walikuwa watajwe mteuaji wa Wajumbe hawa ni Rais, lakini ninavyoamini mimi kama Rais anashirikiana na ile taasisi inayotakiwa kwa wale wajumbe. Kwa mfano kilimo wakulima wanatakiwa ashirikiane na Waziri wa Kilimo.Wavuvi wanatakiwa washirikiane na Waziri wa Uvuvi, lakini Waheshimiwa wavuvi walioko kwenye Bunge la Katiba hakukuwa na mvuvi hata mmoja, wale ni watu waliochukuliwa maofisini wakapelekwa kwa jina la uvuvi, na wakati huo huo hakukuwa na hata mfanyakazi mmoja wa Idara ya Uvuvi au Wizara ya Uvuvi.

Kuna makarani wale wanaokaa na wavuvi, wangepelekwa angalau wale tukawaona, lakini wamechukuliwa watu maofisini wamepelekwa kwa jina la kuwa ni wavuvi, ninamuomba Mhe. Waziri akija anambie je hawa wavuvi waliopelekwa walichukuliwa katika kijiji gani, na walitoka katika taasisi ipi? Kwa sababu wavuvi hakuna kwa Unguja na Pemba kama Wakojani hakwenda hata mmoja, kama Matemwe hakwenda hata mmoja. Kama Tumbatu hakwenda hata mmoja, Micheweni hawakwenda, walichukuliwa wapi wavuvi wale?

Mhe. Waziri nakuomba sana uje unisaidie kunijibu swali hili, kama wale wavuvi wanaochukuliwa kule ni wavuvi kutoka wapi, maana mimi naona watu waliotoka maofisini watupu au umeshauriwa wewe, naamini Rais alikutaka ushauri wewe, kwa hivyo ukija utujibu hapa, utueleze wale wavuvi walitoka wapi?

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze, nyuma huku kulikuwa na utaratibu watu wakipewa kuku wa mifugo kusaidiwa kwenye vikundi. Wakisaidiwa mbuzi na kipindi kilichopita nilipiga makelele sana kwa ajili ya kuongeza na kuwapunguzia wananchi umaskini. Lakini ghafla suala lile naona limefifia na limekufa, kwa hivyo Mhe. Waziri naomba ukija pia unieleze hili suala lilikufa, kwa sababu msingi ule haupo au mfadhili aliyetufadhili hatufadhili tena, au kama ni serikali haitoi tena fedha. Kwa hivyo ninakuomba na hilo utakapokuja uje unisaidie.

Mhe. Spika, baada ya machache hayo kwa sababu nimekwambia nitazungumza machache, ninamuomba Mhe. Waziri akija anipe majibu ya hayo ninayoyazungumza na mimi nitamuunga mkono baada ya kupata maelezo mazuri.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi nikaweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii. Nianze kwa kukushukuru wewe binafsi uliyenipa nafasi hii lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa jumla wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara husika.

Mhe. Spika, mimi nikianza kuchangia mchango wangu naanza na eneo la mapato. Nimejaribu kuangalia mapato ambayo yanatarajiwa kukusanywa na Wizara hii, kusema kweli mimi hayajaniridhisha, kwa sababu sikuona tofauti baina ya mapato ambayo yamekusanywa mwaka ambao unamalizika na mwaka ambao unafuata.

Hii itakuwa inaashiria kwamba Wizara imeridhika na kile ambacho kinapatikana kwa sasa wala sekta kuu ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaonekana kwamba inajipangia kutofanya kazi ya ziada. Kwa msingi huo ningeliomba nipate maelezo ni kwa nini taasisi kama hii kubwa ambayo ilijiwekea malengo mwaka uliopita mwaka 2013/2014 ya kukusanya 613,000,000 na ikafanikiwa kufanya hivyo, na mwaka huu ikaweza kuweka malengo yale yale kwa mwaka unaofuata. Naomba maelezo ni kwa sababu gani hata ikabidi malengo ya mwaka jana yameridhisha kwa taasisi hii na badala yake wakaona waweke malengo yale yale?

Nikimaliza hapo ningependa nipate ufafanuzi katika maeneo ya vifungu. Katika ukurasa wa 104 ningeliomba nipewe ufafanuzi katika fungu namba 211100. Hapa kuna eneo la mishahara, malipo ya likizo, malipo baada ya saa za kazi na malipo ya kujikimu.

Mhe. Spika, mwaka jana Wizara hii ilikuwa na makisio shilingi 880,000 lakini mwaka huu wa fedha imeomba 3,040,000 ni kitu gani kimesababisha ongezeko hilo kubwa. Ukiondoka hapo ukija katika eneo la huduma za simu pamoja na mambo yote ambayo yameongezeka, lakini nimeona kwamba katika kifungu kidogo 220100, 220101 mwaka jana waliomba kuidhinishiwa shilingi 480,000 lakini mwaka huu wameomba 1,440,000, ningeliomba kupata ufafanuzi fedha hizi kwa nini zimeongezeka kiasi kama hiki.

Nikiondoka hapo nakuja kwenye ukurasa namba 112 kifungu kidogo 220200 viburudishaji. Pale katika kifungu namba 220201 chakula na vinywaji mwaka jana ziliombwa shilingi 600,000 lakini mwaka huu wa fedha zimeombwa shilingi 3,210,000 lakini ukilinganisha na gharama za mambo mengine utakuta kwamba kuna mambo ya msingi hasa hayakuombewa fedha kama ambavyo ilikuwa inapaswa, lakini fedha nyingi zimekuja hapa, ningeomba vile vile nipate maelezo katika eneo hili.

Eneo jengine ambalo pia nilikuwa naomba maelezo ni ukurasa wa 117 katika kifungu namba 220100; gharama za vifaa na huduma za mawasiliano. Hapa vile vile huduma za simu kutoka shilingi 360,000 zimekwenda kwenye 1,200,000 ningeliomba nipate maelezo katika eneo hilo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa ninakuja katika kijitabu chetu hiki katika utekelezaji wa mwaka ambao unamalizika 2013/2014. Katika muhtasari wa mapato na matumizi Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki naomba kunukuu maneno ambayo yameandikwa hapa.

"Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,678,600,000 tunaendelea huko lakini *point* yangu hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara ni shilingi 2,045,774,050".

Lakini ukiangalia fedha za *OC* zilizopatikana ni shilingi 463,918 hii ni katika hotuba yako Mhe. Waziri, lakini ukija katika jadweli katika ukurasa wa 49 fedha za mishahara zilizopatikana ni shilingi 2,326,000 ina-*differ* na kule ambapo ilikuwa umezungumzia katika bajeti yako. Sasa ningelipenda kupata ufafanuzi. Lakini ukija katika *OC* iko 426,700,000 ukiangalia na kile kitabu cha kule utakuta vile vile kuna-*differ,* ningeliomba kupata ufafanuzi katika eneo hilo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nilikuwa nataka kupata ufafanuzi vile vile Wizara hii katika mwaka wa fedha unaomalizia utekelezaji wake ni pamoja na matayarisho ya awali ya ujenzi wa josho la Mjimbini, yamefanyika ikiwemo shughuli ya kusafisha eneo la ujenzi, kuchora ramani na uwekaji alama za mipaka.

Aidha makisio ya ujenzi yameshatengenezwa na mkandarasi wa ujenzi amepatikana. Mkataba wa ujenzi wa josho umesainiwa na kazi inayotarajiwa kuanza hivi karibuni. Ufuatiliaji wa shughuli za mradi umefanyika pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

Swali langu Mhe. Spika, ukiangalia malengo waliyoyaweka kwa mwaka 2014/2015 malengo yao ni kumalizia ujenzi wa Kituo cha Utibabu Unguja Ukuu, lakini pia wanakumalizia ujenzi wa josho la ng'ombe Mjimbini. Nikiangalia sasa pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya shughuli za mradi hayo ndio malengo yao.

Nikija katika kitabu hiki ambacho kuna fedha ambazo zinapatikana kwa wahisani wa maendeleo humu sikuona eneo ambalo linaweza kutuelekeza kwamba wana mpango wa kupata fedha hizo kutoka eneo gani. Sasa ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutufafanulia na kutuelekeza ni wapi fedha hizi kwa ajili ya mradi huu zitakuwa zinapatikana.

Nikiondoka kwenye eneo hilo Mhe. Spika, sasa ninakuja katika mchango mwengine wa jumla. Ukiangalia bajeti halisi ya Wizara hii mwaka jana waliomba shilingi 4,600,000,000 lakini mwaka huu wameomba 4,200,000,000 ukiangalia katika fedha hizi ambazo walikuwa wameomba ukitoa kasma ya mshahara tu 2.7 kama sikosei katika Wizara hii panabakiwa na 1.4 bilioni. Fedha hizi ukiangalia ni fedha kidogo sana kwa Wizara kama hii ambayo kwa mtazamo wetu Mhe. Spika, baada ya sekta ya uvuvi baada ya zao letu karafuu kupoteza muelekeo tukiondoka katika sekta ya utalii kwa sasa, sekta ya uvuvi ni sekta ambayo inatizamwa kwa mtizamo ambao unaweza kusaidia kunyanyua uchumi wa nchi yetu, lakini ukiangalia uhalisia wa bajeti Mhe. Spika, bajeti ambayo wameidhinishiwa ni fedha ndogo sana. Ningeliomba kwa mwaka wa fedha ambao unaofuata Wizara hii ipewe kipaumbele na iangaliwe kwa umuhimu wake na wapatiwe fedha zitakazoweza kusaidia, na kuonesha kwamba ni kweli eneo hili ni muhimili na ni eneo ambalo linaweza kusaidia uchumi wa nchi yetu.

Mwisho kabisa kwa kumalizia ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie kile kile kilio changu cha kawaida ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaanzisha Chuo cha Uvuvi Zanzibar?

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja kwa asilimia 85 nabakisha 15 mpaka nitakapoweza kujibiwa vizuri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu sote tukiwa katika hali ya uzima na afya njema jioni hii, pia ninakushukuru wewe Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa pia niwapongeze watendaji wako wote wa Wizara hii kwa kazi yao kubwa ambayo sekta hii inawagusa jamii moja kwa moja hasa katika sekta ya ajira. Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake wote kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye ukurasa wa 37 sekta ya uvuvi. Kama tunavyojua uvuvi ni kitu muhimu sana, na katika jamii ni sehemu kubwa imegusa kwa vijana wetu kuhusu ajira, hasa uvuvi huu wa kina kirefu cha maji ambao unajumuisha pia mradi wa kujenga diko na soko la samaki Malindi, unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo Japan *JICA*, mradi huu hawa wafadhili watasaidia bilioni 6 na kidogo na serikali yetu inatoa karibu bilioni 2 kuchangia mradi wa diko na soko la samaki lilioko Malindi.

Mhe. Spika, lakini mimi niseme Mhe. Spika, nisikitike kidogo mradi huu unagharimu karibu bilioni 6 lakini ukitizama serikali yetu inatoa bilioni 2. Kwa hivyo ninaomba sana wafadhili kama hawa wanapokuja na sisi tujitahidi sana kuweka fedha nyingi, ili na wao waone kama sisi tuna matumaini na maendeleo makubwa katika miradi hii au wafadhili hao wanaweza wakaondoka na wakaacha miradi ikawa haiendelei wakatuacha mkono. Kwa hivyo ninaomba serikali iangalie sana suala hili itenge fedha nyingi ili ziweze kusaidia miradi hiyo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 36 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imetekeleza mradi mmoja wa kuimarisha uvuvi wa kina kirefu lakini kwa masikitiko makubwa Idara iliomba milioni 100 lakini serikali iliwapa kama 1,600,000 kwa kweli Mhe. Spika, ni kidogo sana na hawa wenzetu wana nia njema ya kuleta uvuvi huu wa kina kirefu, lakini Mhe. Spika, sekta hii ya uvuvi bado haijatumika ipasavyo hapa Zanzibar.

Kwa hivyo nasema hivi kwa mfano Mauritius, Seychelles mbali ya kuingiza pato la taifa lakini ni sehemu kubwa ya ajira kwa vijana wetu. Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, suala hili ni zuri na uwe na mfano kama hivyo ulivyoombea pesa kwa ajili ya kuendeleza huu uvuvi wa kina kirefu kama wenzetu hawa Mauritius, Seychelles, wanaingiza fedha nyingi kwa upande wa taifa, lakini bado vijana wetu wanapata ajira kupitia sekta hii. Kwa hivyo naomba sana wazo lako na nia njema hii uliyokuwa nayo iendelee ili tuweze kuwakomboa vijana wetu kwenye sekta hii ya uvuvi wa bahari ya kina kirefu.

Mhe. Spika, uvuvi wa bahari kuu zikiwemo sheria za kimataifa yanataka mawasiliano ya uhakika, kwani sisi tunashindwa kuvua katika bahari kuu, zana zetu kwanza hazina ule ubora wa mawasiliano kwa sheria ya kimataifa hatuwezi kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri hili suala lifanikiwe haraka na serikali iweze kutia mkono wake hapa. Kama nilivyosema sheria za kimataifa hatuwezi kuzitimiza wananchi bila ya serikali kushirikiana na wananchi kwa kuleta zana za kisasa.

Mhe. Spika, niipongeze sana serikali kwa juhudi zake kubwa kabisa kwani ilitenga shilingi milioni mia tano (500,000,000) kwa ajili ya kununua boti lakini gharama za boti hiyo ilikuwa kubwa sana. Kwa hiyo, mimi naishukuru sana serikali kwanza kwa nia yake njema japo fedha zetu kidogo lakini ilionesha nia nzuri ya kutafuta boti hii, lakini kwa kweli gharama yake ni kubwa, lakini naomba iongeze juhudi ya kutafuta pesa kununua boti ya kisasa.

Mimi siku moja nilikuwa Canada nilipata bahati kutembea katika sehemu ya wavuvi, hivyo nilipata kutembelea boti moja niliiona pale nikaingia ndani nikaambiwa boti hii haina haja ya kuvua ukii-*park* pahali samaki wanaingia wenyewe humu ndani na unaowataka unawachukua na usiowataka unawaacha.

Kweli ni jambo la kileo na la utaalamu mkubwa lakini hatuwezi kununua kwa sasa hivi ila nafikiri tukijitahidi na kwa nia njema ndani ya nchi yetu tunaweza tukanunua vifaa ambapo boti kama hii ambayo unaenda kuitega tu pahali samaki wanaingia wenyewe bila hata kuvuliwa.

Mhe. Spika, niingie kwenye hili suala la ukulima wa mwani hasa kinamama tunaona wanalima mwani sana ukitizama kule Pemba na Unguja sehemu ya pwani pwani wanalima sana ukienda utaona, lakini wanapata tabu sana kinamama, kwani hawana viatu siku nyengine wanachomwa na nyenga au wadudu wabaya wa kwenye bahari, wanapata tabu sana na ukitizama gunia zima wanalolitafuta na wakilipata faida yake ni ndogo sana. Kwa hiyo, naiomba serikali iwaangalie sana kinamama.

Naamini kabisa Mhe. Spika, wanawake wakiwezeshwa wanaweza kabisa, kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri uwaangalie sana wanawake kwani kazi zao zinakuwa ngumu na hawawezi kufanya kazi nyengine, hivyo tuwawezeshe na tukiwawezesha basi watafanya kazi hii kwa uzuri kabisa, hasa hawa wakulima wa mwani mazingira yao ni magumu kabisa.

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalotukabili sisi vijana ni tatizo la uvuvi kwa kukosa mitaji. Mheshimiwa mitaji ni midogo lakini vijana wana uamko na wana shauku ya kufanya kazi ya uvuvi kwani wanaiweza. Vijana wengi waliokaa mwambao wa pwani wanaelewa jinsi ya kuvua na wana taaluma nzuri kabisa kwa sababu wamezaliwa ndani ya visiwa hivi.
Vijana wengi wamemaliza skuli Mhe. Spika, hawana ajira, ukitizama vijana wetu wamemaliza elimu ya juu ajira hamna, lakini sekta hii ya uvuvi ikiwa ina mitaji mizuri ya kukopeshwa zana nzuri mimi naamini vijana wetu watavutiwa sana na sekta hii ya uvuvi, kwani ina tija kubwa na ina ajira kubwa katika dunia nzima kama ilivyosemwa mwanzo Mauritius, Seychelles wanajishughulisha sana na uvuvi huu wa baharini hasa bahari kuu. Kwa hiyo, vijana wetu hawa tukiwapatia nyenzo mimi naamini wataweza kufanya kazi vizuri na wanaweza kujitahidi.

Mhe. Spika, suala hili la uvuvi ukitizama zamani mimi nakwenda kununua mishipi na ndoana pale Malindi. Vitu vingi vinauzwa nyavu nilikuwa nakwenda kuvua kule Malindi na bei ilikuwa rahisi, lile duka lilikuwa la serikali ama sijui la wizara. Kwa hiyo, naiomba serikali ifungue duka kama hili moja kwa ajili ya kusaidia hawa wavuvi wadogo wadogo waweze kuuziwa hata nusu ya bei, serikali iwasaidie vitu kama hivi kama ndoana, nyavu, na mashine za boti; ni tatizo kubwa sana kwa wavuvi wetu, wanashindwa kumiliki hata ndoana.

Kwa hiyo, naiomba sana wizara iangalie suala la kufungua duka liwe la serikali angalau liwe linaingiza pesa nusu, lakini itakuwa limeshasaidia vijana na ajira kwa wananchi wetu kuwasaidia katika kazi hii ya uvuvi.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye soko hili mbali na soko hili la ufadhili wa *JICA* lilosemwa mwanzo la Malindi.Mimi nawapongeza sana wafadhili hawa kwa moyo wao na wajitahidi wazidi kutusaidia na nawashukuru sana kwa imani yao waliotuonesha, lakini nasema Mhe. Spika, mbali katika soko hili hapa Kizingo kuna bandari nzuri sana Jimbo la Kikwajuni, bandari ile ya Kizingo iko miaka mingi iko vile vile Mhe. Waziri naomba kama kuna uwezekano wa kuisaidia bandari ile iwe nzuri na ya kisasa kwani nashukuru sasa hivi kuna Msikiti unajengwa katika eneo lile, lakini serikali pia iimarishe ile bandari pale, kwani ni wavuvi wengi wanavua pale na wao waweze kufanya kazi kwa urahisi.

Pia ukitizama katika Jimbo langu la Bububu kuna bandari tatu pale Kibweni, Sharifumsa na Bububu lakini hata banda la wale wavuvi la kuezekwa kwa kujificha jua au mvua hamna. Kwa hiyo, naomba wizara yako Mhe. Waziri ukipata nafasi angalau Kizingo kuna banda lakini ukija katika jimbo langu kuna sehemu tatu hakuna hata banda na wafanyabiashara wanaumia sana kwa kazi zao, kwani wakitoka baharini hawana pa kujificha.

Mhe. Spika, vijana wetu wanajitahidi sana na kazi hii ya kuvua kwa ajili ya kufanikiwa katika maisha yao. Lengo la Mapinduzi yetu ya 1964 ili tufaidike na haya Mapinduzi na tule matunda yake kwa kuwajengea hawa vijana wetu mazingira mazuri, hivyo ndio faida ya Mapinduzi Mhe. Spika. Kwa hivyo, naomba sana tuwaangalie hawa wenzetu.

Mhe. Spika, nikija upande wa soko la samaki ukitizama sasa hivi hawa samaki hata soko lake halifahamiki, ukienda jioni bei inapungua, ukienda asubuhi bei inakuwa kubwa kwa sababu wanatoka baharini, samaki wakiwa kidogo bei inakuwa inazidi na samaki wakiwa wengi bei inapungua.

Kwa hivyo, hawa wavuvi wetu bei zao haziko *stable*, mimi naomba tuwajengee mazingira mazuri hata ukienda asubuhi bei ile ile, ukienda mchana bei ile ile inakuwa wale wavuvi hawapati kujua kwamba mimi nitauza samaki hawa kwa bei gani na soko langu litakuwa vipi, unakuta bei zinabadilika tu kila wakati.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri hilo uliangalie sana kupitia wavuvi wetu wadogo wadogo, kwani wanahangaika sana kupata soko lao hasa katika marikiti zetu. Na kule Malindi utakuta wanauza nje hata ndani hawauzi sijui kwa nini au ndani kumejaa au vipi, kwa kweli mazingira yao ni magumu, naomba uwasaidie sana Mhe. Waziri ili wapate kuwa makini katika soko lao.

Mhe. Spika, mimi niipongeze sana wizara kwa kujitahidi kukusanya mapato zaidi ya milioni mia nne (400,000,000). Kwa kweli nawapongeza sana na inaonesha kama kweli nia ipo na tamaa ipo ya serikali kupata pato jingi zaidi kupitia kwa wavuvi wetu hawa kwa kuingiza tija, lakini ukitizama sasa hivi kweli wavuvi wako wengi na takwimu nilizoziangalia haraka haraka sasa hivi Zanzibar tuna wavuvi karibu 80,000 ambao hawa tayari wana ajira katika sekta hii ya uvuvi, hili ni jambo la kujivunia na naamini itaongezeka zaidi.

Mhe. Spika, kwa uchunguzi nilioufanya nina imani na nia njema na nchi yetu pamoja na serikali yetu tunaweza tukafika mbali katika sekta hii ya uvuvi kwa hivi ninavyoona. Ukitizama sekta hii inaongezeka siku baada ya siku na matunda yake tunayaona.

Mhe. Spika, pia ukitazama hata katika hoteli za kitalii zinategemea sana uvuvi hasa chakula cha *sea food*. Watalii wanaokuja hapa Zanzibar wanapenda kununua, hivyo wavuvi wanafaidika na hawa wageni wetu wa kitalii. Kwa hiyo, mimi naomba tuangalie sana sekta hii kwani ina manufaa makubwa na inaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Spika, katika ukurasa Nam. 5 sekta ya uvuvi imepata mafanikio makubwa sana. Mimi nawapongeza sana wizara kwa juhudi zao kubwa kabisa kwani nikitizama ukurasa wa 5 kitabu cha Mhe. Waziri kifungu Nam. 2 kumevuliwa tani 41,952 za samaki.
Kwa kweli hii sio kazi ndogo, mimi nawapongeza sana wavuvi kupitia wizara hii kwa juhudi zao kubwa kabisa za kutusaidia kupata kitoweo pamoja na watalii wetu na wawekezaji mbali mbali wanaweza kufaidika kupitia wavuvi wetu hawa, japo hali zao ni ngumu sana lakini wanajitahidi na mimi nawapongeza sana na wazidi kujitahidi na serikali izidi kutafuta njia za kuwakwamulia matatizo yao Mhe. Spika.

Mhe. Spika, pia niseme kwamba wavuvi wetu hawa zimewaingizia fedha ambazo wameweza kujipatia katika uvuvi wao huu miezi 9 iliyopita karibu bilioni 153; kwa kweli hili sio pato dogo kwa wavuvi kama hawa na ajira kubwa kwa fedha kama hizi kuingiza. Mhe. Spika, hili ni jambo la kupigiwa mfano na kuwapongeza sana hawa wenzetu.

Mhe. Spika, sasa hivi nije kwenye sekta ya mifugo…

Mhe. Spika: Dakika tano bado.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Spika, namalizia katika sekta ya mifugo mwaka 2013/2014 imeweza kupata mafanikio makubwa, lakini mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa kwa kuweza kukisoma kitabu chake ametwambia hapa uzalishaji wa mayai karibu tani 10,362 kwa mwaka huu wa 2013 kwa kweli hili ni la kupigiwa mfano.
Pia uzalishaji wa nyama ya ng'ombe tani 4966 kwa kweli jambo la kupigiwa mfano Mhe. Waziri hii ni jitihada kubwa na bado bidii ipo ya kuongeza ili hili soko letu liweze kukua zaidi.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba soko bado linahitajika Zanzibar japo wazalishaji wetu wanajitahidi kwa kazi yao kubwa, lakini bado soko tunaagiza nyama kutoka nje, kuku kutoka nje, mayai kutoka nje. Kwa hiyo, naamini bado uwezo upo wa kuingiza kipato kikubwa kwa serikali katika sekta hii ya kilimo.

Mhe. Spika, nimalizie sekta hii ya kilimo tatizo kubwa ni zana. Naiomba sana serikali kwa kupitia wizara yako Mhe. Waziri iangalie vijana, sasa hivi ukitaka washajihike basi tuwapatie zana za kisasa hasa haya matrekta na mambo mengine ya pembejeo mazuri mazuri watashawishika na watavutiwa sana kuja kwenye sekta hii ya kilimo.

Tukiwapatia zana hizo basi naamini wataacha ajira nyengine basi watakuja kwenye sekta hii kwa sababu ya zana na mafanikio yatakuwa mazuri kabisa. Kwa hiyo, naomba uwasaidie sana kupitia Serikali yetu ya Mapinduzi iliangalie hilo.

Mhe. Spika, nimalizie kidogo kuhusu miradi ya wafadhili wanapoondoka miradi hii inakufa, inaweza kuwa wafadhili wamechukua mradi huu wanauendesha wao lakini wakituachia sisi ule mradi unakufa. Nitoe mfano mzuri tu hili shamba la wafugaji wa ng'ombe Chamanang'we hili shamba limekufa kwani wafadhili walipoondoka hawa ng'ombe wamepotea, shamba limepoteza hadhi yake. Kwa kweli mimi nasema mambo haya yasijirudie, kwa hiyo wafadhili tunapokuwa nao na sisi wazalendo washirikishwe ili wafadhili wanapoondoka tuweze kujiendesha wenyewe na lile lengo na madhumuni ya mradi ule usije ukafa.

Mhe. Spika, baada ya hayo na mimi naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kutupa uwezo wa kutoka katika maeneo yetu hadi hapa, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Nadhani Mhe. Spika, nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri alivyoiwasilisha na tumeifahamu. Aidha, nachukua fursa hii kutoa pongezi maalum kwa Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kuchukua hatua ya kufika katika Jimbo langu la Wawi na kukagua vikundi mbali mbali vya ufugaji samaki. Sasa kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Wawi namshukuru Naibu Waziri wa mambo haya ya uvuvi na mifugo kwa kuweza kututembelea kule.

Mhe. Spika, leo hii mbele yetu kuna hii hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi mimi nataka nianze na uvuvi.

Mhe. Spika, kama kuna sekta muhimu sana inayohitaji umakini katika kuisimamia na umahiri katika kuiendesha kwa nchi za visiwa kama sisi hapa Zanzibar basi ni hii sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa wakati wenzetu wanapanua bajeti zao katika masuala ya uchimbaji wa mafuta, wanapanua bajeti zao katika kuimarisha viwanda, sisi nilidhani kama serikali ingekuwa na bajeti kubwa katika suala zima la uvuvi, kwa sababu eneo letu kubwa sisi limezungukwa na bahari. Kwa mnasaba huo nilidhani kwamba serikali ingekuwa makini mno katika kuimarisha hii sekta ya uvuvi. Nilitegemea kwamba bajeti ya serikali angalau asilimia 35 ingeekezwa huku. La kusikitisha Mheshimiwa sidhani hii bilioni 11 kwamba inafika hata asilimia 11 *total budget* ya nchi. Hii ni dharau kubwa kwa taasisi nyeti kama hii.

Mhe. Spika, nimelazimika kusema hivyo kutokana na kwamba asilimia kubwa ya Wazanzibari wamewekeza katika mambo ya uvuvi pamoja na mazao ya baharini, la kusikitisha ni kwamba serikali haikutoa kipaumbele.

Mhe. Spika, hivi tunavyozungumza ni kwamba vikundi mbali mbali vya kinamama katika jimbo langu na majimbo mengine ya visiwa hivi wamewekeza katika suala zima la kushughulikia mazao haya ya baharini ikiwemo mwani, chaza, kaa pamoja na samaki. Tena hawa wanafanya kazi, kwa sababu tunaweza tukasema sisi walimu wameamua kuwekeza katika kilimo cha chaza kwa mfano akinamama walioko pale katika jimbo la Mhe. Abdalla pale Makombeni, akinamama wa Makombeni wamewekeza katika kilimo cha chaza *just for their curiosity*. Hakuna mtu aliyekwenda akatoa ubunifu, wameibuka wenyewe wakaamua kuwekeza kilimo cha chaza, na serikali imewaona wale kinamama kwa sababu wale kinamama kwa kweli mimi nachukua fursa hii kuwapongeza sana.

Mhe. Spika, kinamama wale wanafanya kazi katika mazingira magumu, yaani vifaa vya kufanyia kazi hawana lakini hivyo hivyo wanakwenda. Sasa nilidhani kama serikali katika suala zima la kuongeza kipato na kupunguza umasikini lingewafungulia jicho wale akinamama wa pale kwa kuweza kuwapa ushauri, kwa kuweza kuwa nao pamoja ili kutekeleza ule mpango wa kupunguza umasikini na kujiongezea kipato wa MKUZA II, lakini sidhani kama Mhe. Waziri hata hao kinamama anawajua, hata hicho kikundi sidhani kama anakifahamu.

Mhe. Spika, mimi nilibahatika kwenda na kamati yangu siku zile niko katika Kamati ya Wanawake na Watoto ya Baraza hili. Tulibahatika kutembelea kile kikundi, tulipokwenda kule Mheshimiwa wanafanya kazi sana walikuwa wanapanda chaza halafu wanavuna na kupata lulu ile, lakini unakuta siku nyengine maji yanakuwa mbali yanakuja juu sana yanakuwa yana kina kirefu mpaka kufika zile kamba zao zenye wale chaza inakuwa maji ni makubwa, hata *life jacket* moja hawana wale. Nilidhani kama serikali ingeweka *life jacket*, na la kufurahisha zaidi kile kikundi asili yake ni Chama cha Mapinduzi, namuomba Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi au Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi kama yumo humu yeyote aende pale Makombeni akawaangalie wale wanachama wake jinsi wanavyopata shida katika kuzalisha mazao yale pale.

Sisi tulikwenda pale kama Kamati; yaani wanakwenda pale maji makubwa hawana *life jacket* hata moja. Mimi nawanasihi wale wafanyabiashara waliomo humu ndani Dk. Mohammedraza Hassanali hayumo sasa hivi lakini wamo wenzake hebu wawatembelee wakawasaidie kidogo wale kinamama angalau *life jackets* hizi. Sisi tunakwenda kuwasukuma hivyo kidogo kidogo lakini na nyinyi haitakuwa vibaya kwamba *Hassan & Sons* akaingia pale au *Bhaa Enterprises* akaingia pale na yeye akasaidia.

Mhe. Spika, niende kwengine katika suala zima la wakulima wa mwani. Nilitembelea Kuukuu Kangani kule akinamama wako makini sana katika hiki kilimo lakini napata tatizo kwamba Waziri sidhani kama amekwenda ukanda ule akawaona wale akinamama, pamoja na kwamba bei ya mwani inayumba yumba lakini ushauri pia ungewasaidia, na sasa katika kilimo cha mwani *in general* sasa hivi ni tatizo. Tukiangalia upande mmoja unapata maslahi lakini kwa upande mwengine ukiangalia kilimo cha mwani wanakata miti katika kutia zile kamba zao.

Hii inaitwa *environmental destruction,* sasa mimi nadhani wataalamu hawa wangetusaidia tufanye nini ili hawa wakulima wa mwani badala ya kutumia miti tuweze kutumia jambo jengine ambalo halitaathiri mazingira. Inasikitisha kwamba wakati tunazungumzia mabadiliko ya tabia nchi, wakati tunazungumzia ongezeko la hewa ukaa katika nchi, wakati huo huo tunafanya kilimo kwa kukata miti, tukate miti ndio tukapate pegi pale, hakuna *another alternative*? Hebu wataalamu twambieni hakuna *another alternative* tunayoweza kuitumia ili wale wakulima wa mwani wasikate ile miti kufanya zile pegi zao pale ili wasituharibie mazingira. Mimi nadhani waende Kuukuu Kangani wakawashauri wale ili waweze kufanya shughuli zao vizuri na kadhalika.

Mhe. Spika, niende katika wavuvi wa kaa. Juzi katika swali langu la msingi niliuliza hapa mambo ya uvuvi wa kaa. Kaa kwa kweli sasa hivi ni *first class marine food*, lakini tatizo liliopo watu wanalima kaa, kinamama wanajiwekeza katika sehemu za Kidundo Mtambwe kule, sehemu za Vitongoji kule Kibokoni, Umangani, wamewekeza katika kilimo cha kaa lakini soko ni tatizo. Haya hayana ile *scientific advise* ya kuweza kuwapa ushauri, hivyo vifaranga vinaua vifaranga vya samaki. Je, hivi vifaranga vya kaa viko, kama viko mnawapelekea hawa kinamama? Wana bidii sana tena wanakuwa wakubwa kaa wao. Sasa mimi nilikuwa namuomba Waziri na wataalamu wake waende sehemu za Kiuyu wanafuga sana kaa, sehemu za Kidundo, Mtambwe wakawashauri hawa kinamama.

Mimi kipindi fulani nilikuwa safarini China, wenzetu wameendelea wale kaa wanawafuga mpaka kwenye maduka hivi unawakuta kaa wamo kwenye makontena fulani vifaranga vinakua pale pale mtu anakuja dukani kununua. Sasa

kama wenzetu wamemudu vile, sisi vipi tunaweza tukafika kule? Waje watushauri wataalamu hapa, badala ya kuchezea matope kwenda baharini huku wanachomwa na miba na matope tunaweza na sisi tukafuga kaa kama wanavyofuga wenzetu China kuchukua maboksi ukaweka barazani wakaja wakatushauri?

Mhe. Spika, sasa nizungumzie sekta ya mifugo. Hapa tumeambiwa kwamba mifugo imeongeza idadi ya maziwa, nyama, na mayai; lakini mifugo ina matatizo sana hasa sisi tulioko kule katika pembezoni mwa miji.

Mimi mwenyewe ni mfugaji wa kienyeji nafuga ng'ombe wa kienyeji, nafuga kuku wa kienyeji, lakini tatizo tunalokumbana nalo sisi wafugaji wadogo wadogo kule ni ushauri wa maafisa hawa mnaowaita maafisa ugani, maafisa hawa kule kwetu ni tatizo sijui wako au hawako hawa, hatuwaoni.

Hivi karibuni kuliingia tatizo la magwa sijui kitaalamu maradhi ya kuku yanaitwaje sisi tunaita magwa, wanapukutikwa na miguu halafu wanakufa, yaani yakiingia hayo ndio unamaliza mifugo yote.

Sasa nataka wataalamu hawa Mhe. Waziri hivi hawa maafisa ugani siku hizi jamaa wa Utumishi Serikalini maana huna uwezo wa kuajiri wewe, hawataki kuwaajiri? Hii ndio njia pekee katika masuala mazima ya *income generating* na *poverty reduction.*

Sisi tumeamua kuwekeza kwenye mifugo leo bila ya kutuletea maafisa ugani katika vijiji vyetu ni tatizo kubwa. Sasa nilikuwa namuomba Waziri ni sababu gani za msingi ambapo sisi wafugaji wa kuku na mbuzi kule Vitongoji, wafugaji wa ng'ombe kule Furaha Uwandani kwa nini hatupati ushauri wa kitaalamu?

Juzi mimi chotara wangu yaani hivi hivi tu kanitoka niko kwenye Bunge la Katiba pale nikaambiwa ng'ombe anataka kujifungua sijui ana tatizo la nini na nini ikawa wanangu wanamtizama tizama tu pale, matokeo yake alifariki yeye na mtoto. Nikawaambia nendeni mkaangalie huko hao maafisa wakahangaika sana wakashindwa kupata madaktari. Sasa mimi nilikuwa naomba sana kwamba Mheshimiwa kuwa na tatizo hili basi hebu ajiri, chuo si kipo kile kinasomesha mambo hayo pale Kizimbani tupate wataalamu waweze kutuzalishia ng'ombe wetu.

Mhe. Spika, tatizo jengine ni wizi katika eneo la Vitongoji pale Ole Furaha, nilileta swali hapa kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu suala zima la Jeshi la Polisi watatusaidiaje, kwamba mtu anaiba ng'ombe leo, kesho anadunda mtaani hazuiwi wala hafunguliwi kesi Mahakamani.

Waziri yeye alinijibu hivi, akatwambia masheha sijui nini, lakini sasa Mhe. Waziri nilikuwa nataka unieleze kwamba mnaweza mkatusaidia vipi sisi wafugaji wa maeneo haya kunusurika na wizi wa ng'ombe. Kwa sababu Ole na Vitongoji wamekithiri ng'ombe wetu kuibiwa, na sisi ndio mitaji yetu na ndio maisha yetu haya. Sasa sijui wewe Mhe. Waziri ukiwa *mas-uli* katika masuala haya ya mifugo utashirikianaje na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mratibu hapa katika masuala ya Muungano ambaye anamiliki mambo ya majeshi ya polisi, ili wale wanaoiba ng'ombe wetu angalau zile kesi Mahakamani ziwe zinakwenda na ikiwezekana wahukumiwe, sio leo anaiba ng'ombe kesho anaonekana huyo hapo.

Jengine katika suala zima la mifugo ya mbuzi na kuku tunakumbana na tatizo la mbwa. Mbwa nao ni sehemu ya mifugo, hapa Mhe. Salma Mohammed Ali tukija tukiwaua mbwa watakuja kuwa wakali watasema tunawaadhibu wanyama, lakini hawa mbwa wanatuhusudi, ndama anazaliwa sasa hivi hapo hapo ukienda ng'ombe keshazaa ndama analiwa na mbwa,mbuzi wanaliwa na mbwa. Sasa naomba mutusaidie Mhe. Waziri kwa kushirikiana na hawa polisi au Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa, mnaweza mkasambaza vipi magobore sio kuadhibu mifugo, hivyo ni kuinusuru mifugo mkawaulia mbali wale mbwa mwitu pale ili mifugo yetu ikapata nusura.

Mhe. Spika, jambo jengine nimalizie kwenye haya mambo ya uvuvi, vile vile kwamba sisi wavuvi tuna tatizo Mhe. Waziri, kwanza sisi wavuvi tuna tatizo kwamba mazao haya yaani samaki hatuwezi kuwa-*store* na *seasonal*. Tunalazimika kwenda kwenye bamvua lile samaki wanavuliwa wengi tunauza kwa bei ya kutupa. Mhe Waziri anaweza akatusaidia vipi ku-*stabilize* ile *marking food price* ili ikawa *stable* tukapunguza angalau huo umasikini.

Leo katika kipindi cha mwezi wa giza dagaa unakuta sufuria zima ni shilingi 1,000; wakati ingelikuwa tunaweza kuli-*store* dagaa lile likakaa mpaka kipindi cha mwezi mdande basi tukaliuza kwa bei nzuri, lakini sasa hatuna uwezo huo. Je, wizara yako sisi wavuvi wadogo wadogo mtatusaidia nini?

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuiomba serikali yetu kwamba iwe makini katika sekta ya uvuvi. Hivi sasa kama kuna nchi ambayo ina utajiri mkubwa wa samaki ni sisi lakini hawa wanapewa shilingi 11 bilioni na *point*, kuna samaki katika bahari kubwa kule hawawezi kufanya doria kwa pesa hii.

Mimi nashauri Mheshimiwa kwamba kuna haja sasa serikali kuwa *serious* ili wampe nguvu Mkurugenzi katika masuala haya aweze kutulindia samaki wetu na sio kupita mameli ya nje yakiopoa majodari na samaki wengine.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa naomba niunge mkono kwa kiasi fulani hii hotuba na nimalizie kuja kuunga mkono pale Waziri atakaponieleza juu ya kwamba atasaidiana na Waziri wa mratibu wa mambo ya Jeshi la Polisi na ofisi ya *DPP* kuona kwamba wale wezi wa ng'ombe pale Vitongoji, Furaha, Wawi zile kesi za ng'ombe zinafunguliwa na zinakwenda, na sio mtu kama anaiba ng'ombe kesho anarudi keshokutwa anakwenda kuiba ng'ombe mwengine. Naomba maelezo hayo ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kupata fursa hii jioni ya leo kuchangia machache tu kama kawaida yangu katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza niseme wizara hii ni muhimu kiafya, kiuchumi na hata kibiashara. Sekta ya Mifugo ina mchango mkubwa katika kujenga afya zetu za kila siku, pia ili tupate watu wenye afya ni lazima tupate chakula bora ikiwemo mboga mboga, samaki, maziwa na mayai na hivi vyote havipatikani bila ya kuwa na wafugaji ambao watafuga kisasa zaidi. Wizara hii itakuwa na jukumu hilo la kutoa taaluma ili wafugaji hawa wapate mifugo yenye ubora zaidi.

Mhe. Spika, vile vile sekta hizi zinachangia pato la taifa, ni lazima serikali isaidie makundi ya wafugaji ili ule ufanisi uweze kupatikana. Kwenye kitabu hiki Mhe. Waziri katika ukurasa wa 3 amesema kwamba sekta ya mifugo na uvuvi imefanikiwa kwa kiasi fulani, mafanikio katika sekta hiyo ni kwamba kuongezeka uzalishaji wa maziwa kutoka tani 24,343 mwaka 2012 hadi kufikia tani 27,243 kwa mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka huu.

Mhe. Spika, kwa kweli na mimi najenga hofu kidogo kwani sijui takwimu hizi wamezikusanya kutoka sehemu gani, kwani ni imani yangu kwamba wizara labda ingekuwa na sehemu au *ranch* wanaweka mifugo na hii ikawa ni hesabu ambayo imetokana na ule uzalishaji wao wenyewe, lakini hapa naona siamini kwamba uzalishaji wa maziwa huu ni kwa Zanzibar nzima; yaani pamoja na Pemba au ni vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija atanifahamisha zaidi ili niweze kumuunga mkono katika bajeti yake hii, na mimi sina tatizo ya kuiunga mkono bajeti hii kwa niaba ya wale walionichagua.

Vile vile kuna mafanikio mengine kuongezeka uzalishaji wa mayai kutoka tani 9,663 mwaka 2012 hadi kufikia tani 10,992 kwa mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 14 kwa mwaka huu. Hii vile vile inanitia mashaka kama ile ya mwanzo kwamba naona hizi hesabu sijui zimepatikana kwa vigezo gani. Niiambie tu wizara kwamba ijitahidi kuwawezesha hawa wafugaji ili wafuge kuku wa kisasa na wale ambao hawatatumia makemikali mengi. Kwa sababu tunaona kwamba kuna mayai haya yanaingia kwa kweli yanatushangaza, unakuta mayai yako *size* moja meupe sijui haya ni mayai ya aina gani na yanaathiri kiasi gani.

Kwa hivyo, ni lazima tuwe na uchunguzi wa mayai haya, ni vizuri zaidi tukawawezesha wakulima wetu hawa wa humu ndani wakazalisha zaidi hawa kuku. Kwa sababu mifugo nayo pia inaingia katika kilimo kuona kwamba mtu akiwa mkulima bora basi awe na mifugo, na hapa unapata ule mjumuisho kwamba unafuga na unalima. Kwa hivyo, hata kwenye kilimo chako baada ya kutumia mbolea za kemikali basi unatumia hata zile mbolea za vinyesi vya wanyama.

Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Said Salim Bakhressa kwa kuanzisha Kiwanda cha Maziwa; huu ni uzalendo na Mungu amzidishie kwani kupata kwake ndio kupata kwetu. Serikali inapata mapato kutokana na uwekezaji huu na pia watoto wetu wanapata ajira, ambapo atalipunguzia taifa mzigo kwa vijana kukosa ajira. Kukosa ajira kwa vijana ni kujitumbukiza kwenye mambo mengi maovu.

Mhe. Spika, ni nafasi ya serikali sasa kuwawezesha wafugaji wa ng'ombe na mbuzi ili waweze kupata maziwa mengi zaidi, wakipata maziwa mengi nina hakika kwamba tutatokana na umasikini kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kuna msemo unaosema kwamba: "*Ng'ombe wa masikini hazai*". Tuna rasilimali nyingi bado hatujaweza kuzitumia, mfano uvuvi wa bahari kuu hata hatujagusa na sijui lini tutafikia uvuvi huu. Kwa kweli hili ni tatizo na nilisema juzi kwenye mchango wangu wa bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano niliposema kwamba, ni lazima kama Shirika la Meli ni shirika la kibiashara basi ilikuwa lisiwe na meli mbili zilioko sasa; ambazo huko nyuma nakumbuka kulikuwa na meli zinafika nne, lakini badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma.

Kwa kweli kulikuwa na haja sasa ya kutafutwa na meli ya uvuvi ili ikienda huko bahari kuu. Tunaona kwamba ni kazi kubwa na tutatumia pesa nyingi, lakini siku zote ukitaka kutengeneza pesa basi kwanza utumie pesa. Kwa hivyo, ni jambo zuri hili tukawa na meli yetu ya uvuvi na tukaanza kuvua huo uvuvi wa bahari kuu tungepata mapato mengi.

Sekta hii kwa kweli ni sekta kubwa, tungekuwa tuko *serious* na hili jambo basi naamini kwamba serikali yetu ingekuwa ni tajiri sana, na tunao utajiri lakini kama alivyosema mwenzangu asubuhi hapa kwamba utajiri tunao lakini tunaukalia.

Vile vile kuna mambo haya ambayo na mimi yananiumiza kweli, tunakuwa tunatumia pesa nyingi lakini baadae tunaacha rasilimali zile zinapotea. Kwa mfano lile soko la Tumbe hata sisi tulikwenda kama *PAC*, sasa hivi limeshakwisha wala halionekani kufanya kazi, kwa kweli hili pia ni tatizo kwani ile *value for money* haionekani. Kwa hivyo, ni lazima soko hili lifanye kazi ili vile lilivyotarajiwa basi yapatikane yale malengo, lakini kwa kweli inavunja moyo sana kwamba pesa nyingi zinatumika lakini baadae yale malengo hayafikiwi.

Mhe. Spika, soko hili kama ni wizara kulimaliza huyu mkandarasi ambaye amepewa, na sijui ilikuwaje kwa kweli hili ni tatizo. Mhe. Spika, niseme kwamba haya ni matatizo ambayo tunayo.

Mhe. Spika, jengine kulikuwa na mradi ule wa *Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe* sijui umefikia wapi. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja pia aniambie mradi huu umefikia wapi.

Mhe. Spika, baada ya hayo kama kawaida nimekwambia sina mengi, na kwa sababu si mvuvi wala sifugi, kwa hivyo nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi kabla ya kutoa mchango wangu sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia jioni hii kuwa mzima wa afya na kuweza kutoa machache katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie mambo mawili. Moja, ni hili alilomalizia Mhe. Fatma Mbarouk Said kuhusu Soko la Tumbe. Mhe. Spika, Mhe. Bikame Yussuf Hamad amelizungumzia suala hili asubuhi.

Mhe. Spika, toka kujengwa soko hili kwa kweli ni muda mrefu. Na muda wote huu sio kwamba kuna majengo hapo mengi yanayosababisha kutomalizika kwa kazi hii, ni jengo moja tu kubwa, lakini hii kampuni iliyopewa jukumu hili ama Serikali ina matatizo yake, lakini pia na hii kampuni haikosi kuwa na matatizo ya kutolifanikisha jengo hili kukosa kufunguliwa hadi leo hii.

Mhe. Spika, hili soko toka kujengwa ile kampuni kumaliza maliza, mimi nilikuja nikachangia hapa kueleza jinsi ya lile soko vile lilivyo na yale matatizo ambayo yamo katika jengo lile.

Nashukuru Mhe. Naibu Waziri alikisikia kilio kile na mara moja akafanya ziara kwenda kulitembelea lile soko na akanialika tuwe pamoja kule na tukaenda. Kwa kweli aliitaka idara inayoshughulika na mambo haya ya uvuvi ifanye matengenezo kwa mule mote ambamo mnaonekana kwamba ni kero. Idara hii ikachukua jukumu hilo, lakini Mhe. Spika, mpaka hapa ninaposimama Naibu Waziri alikwenda tena kwa mara ya pili na tayari hivi sasa wapo kulisimamia na kukarabati yale maeneo ambayo bado yana matatizo.

Mhe. Spika, najiuliza tatizo ni wizara, tatizo ni Serikali, tatizo ni mafundi. Mhe. Spika, jengo hili tunalolipigia kelele limekosa miundombinu ya ujenzi, linavuja maji yanaingia ndani, halina nafasi ya kima cha juu, mchana ni usiku.

Kwa hivyo, pamoja na matatizo mbali mbali yanayojitokeza namshukuru sana Naibu Waziri katika kulisimamia jambo hili liweze kumalizika.
Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kwamba kuna mafundi, toka kuja mafundi hawa wana mwezi mmoja na nusu, lakini zana za kufanyia kazi hakuna. Wapo hapo wanaongeza siku tu. Kuna maeneo kama sehemu ile ya mnada imechimbwa, kwa hivyo wanahitaji kupata saruji, Serikali imeshindwa kupeleka saruji.

Kuna eneo la chini lililotiwa *tiles*, katika zile *tiles* za mwanzo zilizoingizwa ilikuwa ukitembea tu basi nyengine zinakufuata zinabanduka. Ikalazimika kwamba zile zibanduliwe ziwekwe *tiles* nyengine, lakini katika kubandua kuna nyengine lazima zitapata dosari mbali mbali zitavunjika. Kwa hivyo, zile ambazo zilikuwa ni nzima tayari zimewekwa, lakini kuna *tiles* nyengine zinasubiriwa. Mhe. Spika, hili ni tatizo. Kwa hivyo, kuna matatizo mbali mbali madogo madogo ili kuweza hili jengo likamalizika na Serikali wakalikabidhi kwa wavuvi wale wa Tumbe, lakini kazi yenyewe inakwenda kama kwamba haina msimamiaji.

Mhe. Spika, katika jengo hili kuna matatizo ya mashimo ya vyoo. Mwaka jana nilisema kwamba yale mashimo yalichimbwa madogo mno. Hivi sasa Mhe. Spika, mvua hii iliyopita mashimo yale yamejaa maji kibao. Sijui likija likifunguliwa soko wakati wa mvua tukitaka kwenda haja itakuwaje,lakini nasema tena Mhe. Spika, haya mashimo ni bora tukatafuta utaratibu mwengine wa kuchimba. Sio kama yale yaliyochimbwa kama visima, kwa sababu lile ni eneo la maji, na mashimo ukiyachimba kama kisima basi huendi hatua mbele maji utayakuta yapo karibu, lakini wangeyachimba kama mahodhi marefu basi yangesaidia japo ukafika wakati wa mvua ingekuwa mashimo yale hayajai kirahisi.

Mhe. Spika, tatizo jengine hii ilikuwa kampuni moja maskini ikatafuta wafanyabiashara pale wakawa wanawakopa saruji, mbao, mawe, kokoto na nondo. Fedha hizi za wananchi hawa wanyonge hadi leo hawajalipwa.

Pia Mhe. Spika, kuna yule aliyepewa ulinzi wa hili soko, toka lijengwe kuna mtu analinda anadai pesa karibu milioni 1.5 hata senti 5 hajalipwa. Sasa Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo sugu. Kwa hivyo, inaonesha kwamba wananchi wana uzalendo. Mtu halipwi lakini bado anaendelea kulinda pale lisije likatokea tatizo, lakini kwa mtu maskini shilingi milioni 1.5 si pesa kidogo.

Mhe. Spika, naiomba sana Serikali hili tatizo walimalize, ionekane kwamba tayari soko hili wananchi wanaanza kulitumia tuzungumze mengine, lakini inakuwa ni aibu, sijui labda Serikali ilikuwa haijawa tayari kulianzisha soko pale Tumbe.

Tunaona masoko yaliyojengwa na mradi wa *MACEMP* mengi yamemalizwa tayari yameshafunguliwa, lakini soko hili la Tumbe hadi leo. Na tukaambiwa kwamba hili soko limeshakuwa na mitambo yake ya kuja kuwekea pale samaki wanapovuliwa wasije wakaharibika. Wavuvi wanaopata samaki wengi waweze kuwahifadhi pale, lakini katika kitabu hichi mara hii hata kuelezewa habari za soko hili na hiyo mitambo hazipo. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba majibu marefu.

Mhe. Spika, la mwisho ni ukulima wa mwani. Mhe. Spika, katika jimbo linalozalisha mwani kwa wingi Zanzibar hii ni Jimbo la Tumbe. Mhe. Spika, Wanatumbe wameitikia wito huu wake kwa waume wanalima kilimo hichi cha mwani, tofauti na mawazo tunavyosikia hapa kwamba baadhi ya maeneo wanaozalisha mwani ni wanawake tu.

Nashukuru juzi nilisikia tetesi kwamba Serikali ina mpango wa kujenga kiwanda. Kwa kweli kama Serikali inataka kufanya shughuli hii kwa kuanzisha hichi kiwanda, nadhani wananchi wetu wengi watafaidika katika kilimo hichi. Na tutakapokuwa na hichi kiwanda huu utegezi wa wafanyabiashara wa kuwa na mwekezaji mmoja akawa ananunua mwani miaka 5, 6 hapandishi bei. Nadhani tutakapokuwa na hichi kiwanda basi wananchi watafaidika na hii bei ya mwani itaongezeka.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili la mwani tuwawekeni vizuri wananchi wetu ili wazidi kuimarisha hichi kilimo cha mwani. Kwa sababu kuna faida nyingi tunazisikia mnazitaja hapa kwamba mwani ni chakula, mwani unapata sabuni, unapata vipodozi mbali mbali. Kwa hivyo, ni faida hizo ambazo zitapatikana hapa nchini na huenda tukauza katika maeneo mengine ili kuongeza tija na faida kwa Serikali.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nashukuru, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kupata angalau dakika chache kutoa maoni yangu juu ya hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Pia nachukua nafasi ya kumpongeza kwa uwasilishaji wake ambao ulikuwa ni mzuri sana.

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni wizara muhimu sana kama walivyosema wenzangu wasemaji wa mwanzo. Ni muhimu kwa sababu inajenga afya katika viwiliwili vyetu, pia ajira nyingi zinapatikana kwa vijana wetu, na inaleta mapato ya nchi.

Mhe. Spika, inapaswa Serikali kuiangalia vyema wizara hii. Mhe. Spika, watendaji wa wizara hii kwa mujibu walivyo basi ni mategemeo yangu makubwa kwamba wanaweza kufanya kazi vizuri, kwa sababu ukimuangalia Waziri na Naibu wake ni vijana wenye nguvu. Kwa hivyo, wanaweza wakajituma vizuri sana kuleta maendeleo katika wizara hii, ili Serikali ikawawezesha vyema kuwapatia yale mapato ambayo yanahitajika.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 4 wa kitabu cha Mhe. Waziri katika changamoto za Sekta ya Mifugo. Nakwenda katika changamoto ya kwanza naomba kunukuu. "Kutowafikia baadhi ya wananchi wanaohitaji huduma za ugani kutokana na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi ikiwemo vyombo vya usafiri kwa watoa huduma wa ugani".

Mhe. Spika, hili ni tatizo, na kwa kweli tatizo hili kutokuwafikia watu wetu vijijini ambao wanahitaji elimu, mafunzo na maelekezo, lakini nimuulize Mhe. Waziri, tatizo hili litamalizika lini? Kwa sababu nikiangalia Kitabu cha Bajeti ya mwaka 2011/2012 limerudiwa tatizo hili hili la ukosefu wa vipando kwa ajili ya Maafisa Ugani kuwafikia wafugaji wetu.

Mhe. Spika, pia tatizo hili hili lilirudiwa tena katika bajeti ya mwaka 2012/2013 na leo 2014/2015 linarudiwa tena. Mhe. Waziri ni lini Maafisa Ugani watapatiwa vipando ili kuwafika wafugaji wanaofuga vijijini. Kwa sababu wengi wanaishi vijijini, lakini ikiwa ni bajeti ya tatu maneno ndio yale yale tu, kwamba kukosekana kwa nyenzo za Maafisa Ugani ikiwemo vipandio vya kuwafika wafugaji. Hili ni tatizo Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atupe maelezo ya kutosha kwa nini ni bajeti ya tatu maafisa hawa bado hawajawezeshwa kuwafika wafugaji katika maeneo yao ya mifugo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika changamoto hizo hizo za wafugaji nambari 4. "Kuongezeka kwa matukio ya wizi wa mifugo hali inayowarudisha nyuma wafugaji na kuwaongezea mzigo wa kazi kwa kuimarisha ulinzi".

Mhe. Spika, tatizo la wizi wa wanyama kwa kweli hapa Zanzibar limekuwa la muda mrefu. Sasa nimuulize Mhe. Waziri ni mipango gani endelevu ambayo itafanyiwa kazi ili kulipunguza suala zima la wizi wa mifugo katika nchi yetu.

Mifugo ni miongoni mwa ajira, lakini leo mtu anafuga ng'ombe, mbuzi au kondoo wake hajakaa vizuri watu wanakwenda kuwavamia. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atueleze mikakati gani ambayo ameipanga ili kuondoa tatizo hili la wizi kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukatili wa wanyama. Mhe. Spika, ukatili wa wanyama upo na umekua kwa kiasi kikubwa sana. Nikiangalia kitabu cha bajeti cha mwaka 2012/2013 katika Sekta ya Mifugo ukurasa wa 3 sehemu (b) anasema hivi. "Kuzifanyia marekebisho kanuni ndogo ndogo za udhibiti na ukatili dhidi ya wanyama ili kupunguza unyanyasaji wa wanyama uliokithiri".

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri kutokana na taarifa hii ambayo ameieleza mwaka jana imefikia hatua gani kuzifanyia marekebisho sheria hizi. Je, watu hawa ambao wanafanya ukatili wa wanyama ni hatua gani ambazo zinachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Spika, niende katika Mazao ya Baharini. Mhe. Spika, miongoni mwa watu ambao wameitikia wito wa Serikali kujiajiri katika kujitafutia mapato ni watu wa Jimbo la Chambani hasa katika ukanda ule wa Mashariki ya pwani.

Kule kuna vijana wengi ambao wamejikusanya pamoja katika kuitikia wito wa ufugaji wa samaki, lakini kutokana na uduni wa maisha, wanakuwa hawafikii lengo. Wana maeneo makubwa ya kufugia samaki lakini bado Serikali haijawaona kuwawezesha ili kupata tija inayotegemewa katika kutatua matatizo yao ya kila siku.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri bila ya kupoteza muda mrefu baada ya bajeti hii afanye ziara ya makusudi na kuniarifu mimi kufuatana naye katika ziara hiyo kwenda kuwakagua wafugaji wa samaki wa Jimbo la Chambani, ili aweze kuzitatua changamoto ambazo zinawakabili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapofika katika maeneo haya yeye mwenyewe ataona kwamba kweli vijana wamejituma na lengo lao ni kujinasua katika umaskini uliokithiri, lakini wanarudi nyuma kutokana na mtaji mdogo walionao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba ufanye ziara hizi na pia uwe na azma ya makusudi ya kuwawezesha wananchi hawa ili waweze kujikwamua katika maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, kwa sababu muda ni mchache sana niende kidogo kuhusiana na maslahi ya wafanyakazi katika wizara hii. Mhe. Spika, wizara hii ni wizara nyeti kama nilivyosema mapema, lakini Mhe. Waziri anahitaji kuwawezesha wafanyakazi wake.

Mhe. Spika, kuna Wakuu wa Idara hasa kule Pemba wanafanya kazi ya ziada, wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi takriban za kuwasaidia Wakurugenzi. Wanafanya kazi ya Ukurugenzi lakini bado inaonekana kwamba maslahi yao ni machache. Je, ni mpango gani madhubuti, mpango endelevu hawa Wakuu wa Idara kule Pemba na wao kujisikia.

Mhe. Spika, hili ni suala muhimu na kwa kweli inapaswa hawa na wao wajisikie kwamba wanapata angalau maslahi yenye kuendana na vyeo vyao.

Mhe. Spika, nimalizie mchango wangu kwa sababu ya dakika zilizopo kuhusiana na suala zima la chumvi. Hii chumvi nani mwenyewe, Serikali itwambie hii inakwenda Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Mifugo na Uvuvi au wapi. Kwa sababu kila mchangiaji anayechangia akifika suala la chumvi anababaika kwa kuwa hajui alipeleke wapi, lakini kwa sababu tunazungumza mazao ya baharini na chumvi inatoka baharini tunalipiga hapa hapa kwenye wizara hii. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali itueleze chumvi tuipeleke wizara gani. Nazungumza hivi kwa sababu wakulima wa chumvi wanatusikiliza hivi sasa wanaweza kuvunjika moyo kutokana na juhudi kubwa wanayoifanya ya uzalishaji wa chumvi lakini hawajui wanapokuwa na matatizo yao waende wapi. Kwa hivyo, mimi simuombi Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naiomba Serikali itupe jawabu ya kutueleza chumvi baba yake ni nani Serikalini.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii baada ya kupata majibu ya masuala ambayo nimeyaeleza. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa ujumla nawashukuru kwa kutumia muda vizuri na kumaliza mchango wa jumla kwa Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wameomba. Kwa hivyo, kesho asubuhi Mungu akipenda mara baada ya dua na kuwasilisha hati mezani, basi tutaanza majumuisho ya hoja hizi mbali mbali ambazo zimetolewa. Ataanza Mhe. Naibu Waziri na hatimaye Waziri mwenyewe.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo basi sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 20/06/2014 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:43 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 20/06/2014 saa 3:00 asubuhi)